# Nipashe

Jumanne Desemba 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580103

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wanandoa wauawa na watu wasiojulikana usiku mnene

UKURASA 3




# Hoja 4 kumng'oa Mbowe Chadema

**MWAMBE** ajinadi kuleta uwazi, kujenga ofisi mpya za chama... *Endelea ukurasa wa 2*



Cecil Mwambe

Freeman Mbowe

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**537 WAPATA MIMBA MKOA MMOJA 2018/19**

JUMLA ya wanafunzi 537 wa shule za msingi mkoani Morogoro wamepata mimba na kushindwa kuendelea...

UKURASA WA 3

**MAMA AZIRAI MBELE YA WAZIRI**

WAFUGAJI wa Wilaya ya Bukombe wameendelea kupaza sauti kulalamikia utaifishaji wa mifugo yao inayodaiwa kuingia kwenye Pori la Kigosi Moyowosi...

## JAMHURI KUMKATIA RUFANI MALINZI

UKURASA 3

# Wanafunzi wa UDSM watishia kuandamana

UKURASA 2




MICHEZO SIMBA, YANGA NJE NDANI MAPINDUZI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Hoja nne kumng'oa Mbowe Chadema

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Ndanda, Cecil Mwambe, amepitishwa kwenda hatua ya mwisho kumkabili Freeman Mbowe, mwenyekiti wa sasa wa Chadema, katika uchaguzi wa ndani wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam kesho.

Wakati Kamati Kuu ya Chadema imepitisha uamuzi huo, mbunge huyo ameanika hoja zake nne anazoamini zitamvusha katika azma yake hiyo, mojawapo akidai ni kuweka wazi matumizi ya ruzuku ya chama.

Ni matukio ya joto la uchaguzi, yanayoendana na kuwapo kwa uamuzi wa ghafla jana wa kujitoa kwa Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea, aliyekuwa anawania nafasi ya makamu mwenyekiti, kwa madai ya kumpisha Tundu Lissu.

Hata hivyo, Lissu ambaye katika nafasi hiyo amebaki na mshindani Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, hadi sasa yuko nje ya nchi kwa zaidi ya miaka miwili na kitendawili cha kurejea kwake nchini bado hakijateguliwa.

Mwambe aliwaambia waandishi wa habari jana kwenye Ukumbi wa Mlimani City jijini, muda mfupi baada ya jina lake kupitishwa, kwamba anaamini hoja zake nne ambazo ni ujenzi wa ofisi, uwazi katika matumizi ya ruzuku, kuboresha maslahi ya watendaji na kubadili sekretarieti, zitamvusha.

Alidai ofisi zilizopo za chama hicho kikuu cha upinzani nchini ni za kupanga, hivyo akichaguliwa kuwa mwenyekiti, atajenga ofisi mpya katika maeneo mbalimbali nchini.

"Ofisi tulizonazo nyingi ni za kupanga, kwa hiyo mimi nikichaguliwa, nitahakikisha tunajenga ofisi bora za chama chetu kwa kuanzia na makao makuu," alijinadi.

Mwambe aliahidi kuboresha maslahi ya watendaji wa chama hicho kwa ngazi za mikoa na wilaya, akiamini kufanya hivyo kutawapa ari zaidi ya kufanya kazi tofauti na sasa.

Alisema jambo la tatu atakalolifanya ni kubadilisha baadhi ya wajumbe wa sekretarieti ya chama hicho, akidai hawajabadilishwa tangu mwaka 2015.

INAENDELEA UK 8



Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier (kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma za Afya kutoka Hospitali ya Aga Khan, Dk. Gijs Walraven (kulia), wakisaini jana hati ya makubaliano ya Sh. bilioni 38 kutekeleza mradi unaolenga kuboresha tiba kwa kina ya saratani. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Wanafunzi UDSM watishia kuandamana

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dare es Salaam (Daruso), imeipa siku tatu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kutekeleza kwa hiari mambo manne, ikiwamo kupeleka mafungu ya fedha za mikopo kwa wanafunzi wa chuo hicho, vinginevyo wataandamana.

Kinyume cha hapo, Daruso imetishia wanafunzi wenye uhitaji huo, Alhamisi watakwenda kwenye ofisi za bodi hiyo kudai haki hiyo, ikidai kuwa sababu za kufanya hivyo wanayo, nia wanayo na uwezo wanao.

Msimamo wa Daruso umekuja zikiwa zimepita siku tano tangu bodi hiyo iiambie Nipashe kuwa ina fedha za kutosha na Desemba 10, mwaka huu ilipokea Sh. bilioni 186 kutoka serikalini kwa ajili ya malipo ya miezi mitatu iliyoanzia Oktoba.

Katika taarifa yake iliyotolewa jana, Daruso inaitaka HESLB ndani ya saa hizo, iwe imepeleka mafungu ya fedha za mikopo kwa wanafunzi wote ambao wamekaa chuoni tangu kifunguliwe bila fedha, ikidai hakuna sababu za msingi za wao kutaabika.

Jambo la pili, Daruso inaitaka bodi hiyo iwe imerudisha fedha zote za wanafunzi zilizokatwa kwa ajili ya vitabu, viandikwa, mafunzo kwa vitendo na utafiti.

"Jambo la tatu, tunaitaka bodi iwe imewapangia mikopo wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao rufani zao zimetupiliwa mbali ilhali ni wahitaji, hasa wanafunzi ambao ni yatima au wana mzazi mmoja.

"Wanafunzi wanaotokana na familia zinazolelewa na Tasaf, wanafunzi ambao wazazi wao ni walemavu na waliofadhiliwa elimu ya sekondari ambao wamewasilisha vielelezo vyote, wapewe mikopo," Daruso ilieleza katika taarifa yake hiyo.

Jambo la nne ambalo Daruso inaliainisha katika taarifa yake hiyo, ni HESLB kumbadilisha Ofisa Mikopo wake wa UDSM, Lugano Mwakyusa, ambaye inadai viongozi wa chuo hawaridhishwi na utendaji kazi wake. hasa lugha anayotumia kuzungumza na wanafunzi wanapokuwa na matatizo.

"Msimamo wa serikali ni kwamba wanafunzi wamevumilia vya kutosha, majadiliano yamefanyika ya kutosha, ahadi za uongo tumepewa za kutosha.

"Na endapo saa 72 zikiisha bila mambo haya kutekelezeka yote kwa pamoja, wanafunzi ambao wana matatizo tajwa pamoja na viongozi wa Daruso, tutakutana nje ya ofisi ya ofisa mikopo ili kwa umoja wetu tuelekee katika ofisi ya Bodi ya Mikopo siku ya Alhamisi saa mbili asubuhi kudai haki kwa kuwa sababu tunayo, nia tunayo na uwezo tunao," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Nipashe ilimtafuta Meneja wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa HESLB, Omega

INAENDELEA UK 8

## 537 wapata mimba mkoa mmoja 2018/19

**Na Christina Haule, MOROGORO**

JUMLA ya wanafunzi 537 wa shule za msingi mkoani Morogoro wamepata mimba na kushindwa kuendelea na masomo katika kipindi cha mwaka 2018/19.

Mwenyekiti wa Taasisi inayojishughulisha na Masuala ya Kulinda Haki kwa Watoto wa Kike wanaoshindwa kuendelea na masomo kwa kupata mimba ya Ngaiza Foundation, Elizaberth Ngaiza, alisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa sekta ya elimu mkoa, na kwamba utafiti mbalimbali unaonyesha watoto wengi hujikuta wakipata mimba kutokana na umaskini wa wazazi wao.

Alisema Ngaiza Foundation imeweza kufanya kampeni ya 'Niache Niishi Kwanza' katika wilaya ya Morogoro na Ulanga mkoani hapa, na kubaini changamoto zinazowakumba watoto wa kike na kusababisha kupata mimba na kuacha masomo.

Alisema jambo la umaskini uliopitiliza kwa wazazi limeonekana kushika kasi, na kusababisha watoto kujiingiza kwenye matendo yasiyofaa na kupata mimba zisizotarajiwa.

Ngaiza alisema watoto hao wamekuwa wakipata mimba na kukatisha masomo na kuwa wazazi au ndugu zao waliamua kufikisha kesi polisi na askari wanne wanahusika kuvuruga kesi kuwafanya watuhumiwa kutoroka.

Alisema anaandaa utaratibu wa kufikisha majina ya askari polisi hao wanne kwenye wizara husika ili wachukuliwe hatua kwa kuhusika na kufanya serikali kuonekana haitekelezi majukumu yake ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Naye Askofu wa Kanisa la Carvary Assemblies Of God, Zephania Lioba, alisema Ngaiza Foundation inafanya ufuatiliaji mzuri wa masuala ya mimba kwa watoto, na kwamba matatizo ya ukatili wa kijinsia hutokea hata kwa watoto wa mijini ambao wazazi wao hawana uwezo kwa kusaidiwa kuwasomeshwa na baadaye kuombwa kulipa fadhila.

Alisema kitendo cha watoto kukubali kulipa fadhila kwa kutoa miili yao ni sawa na kuharibu maisha yao kwa kufanya mambo yasiyompendeza Mungu.

Askofu Lioba alisema ana imani na Ngaiza Foundation kuwa itasaidia watoto mkoani Morogoro na nchi nzima kwa ujumla kujitambua na kuacha kutoa ahsante ya miili yao.

HABARI KITAIFA

# Mama azirai mbele ya waziri

Na Mwandishi Wetu, GEITA

WAFUGAJI wa Wilaya ya Bukombe wameendelea kupaza sauti kulalamikia utaifishaji wa mifugo yao inayodaiwa kuingia kwenye Pori la Kigosi Moyowosi, huku Nsangizyo Joseph akianguka na kuzirai kwenye mkutano wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, baada ya ng'ombe wake 45 kutaifishwa.

Wamesema shughuli ya ufugaji katika Wilaya ya Bukombe imekuwa kama laana kwao, wakidai kuwa hadi sasa, ng'ombe zaidi ya 10,000 wamekamatwa na kuuzwa bila wafugaji wenyewe kushtakiwa mahakamani.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Runzewe na baadaye kuanguka na kuzirai kwenye mkutano huo mwishoni mwa wiki, Mama Nsangizyo alimweleza waziri huyo kuwa licha ya serikali ya kijiji kuthibitisha kuwa ng'ombe ni mali yake, bado walikamatwa na kupigwa mnada kwa kisingizio kuwa mwenye mifugo hajulikani.

Alimwomba Waziri Mpina kumsaidia ili kurejesha mifugo yake kwa kuwa ndiyo rasilimali pekee anayoitegemea kuendesha maisha yake na kumuuguza mumewe ambaye amelazwa katika Hospitali ya Bugando kwa maradhi ya kupooza.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Bukombe, Masanja Simbi, alisema wafugaji wa wilaya hiyo wanapitia vikwazo vikubwa ikiwamo ukosefu wa malisho na idadi ya mifugo inayokamatwa siyo inayotajwa mahakamani.

Pia mifugo kukamatwa na mwenye mifugo kutohusishwa katika kesi ya mifugo yake na kesi ikitajwa kuwa mifugo haina mwenyewe na baadaye kuuzwa kwa kupigwa mnada bila mwenye mifugo kushtakiwa hata kama amejitokeza.

Masanja aliwataja baadhi ya wananchi ambao mifugo yao ilitaifishwa bila wahusika kufikishwa mahakamani na idadi ya mifugo yao kwenye mabano kuwa ni Shimomomo Miasita (1,089), Kazala Peter (276), Kaseko Kulwa (130) na James Wapi (140).

Wengine ni Masaga Makila (300), Mahya Kenda (226), Shije Subi (83), Moses Makimu (72), Ramadhani Pembewa (130) na Mizinga Malimi (280).

Akizungumza na wananchi hao, Waziri Mpina alieleza kusikitishwa na kitendo cha Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kuwatoza wafugaji faini ya zaidi ya Sh. 100,000 kwenye misitu ya asili ya halmashauri ukiwamo wa Ushirombo wenye ekari 18,880 na Msitu wa Runzewe wenye ukubwa wa ekari 80,000.

Alisema Halmashauri ya Bukombe inatambua ina mifugo zaidi ya 130,000, lakini imeshindwa kuwawekea mazingira mazuri ya malisho wafugaji hao ambao huchangia mapato ya Sh. milioni 350 kwa mwaka kutonana na ushuru wa mifugo kwenye minada.

Mpina aliwataka viongozi wa halmashauri hiyo kutambua mifugo ni rasilimali muhimu na ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi, hivyo wasisubiri mpaka Rais John Magufuli atenge maeneo ya wafugaji ilhali halmashauri husika inatambua mahitaji waliyonayo wafugaji.

Kuhusu malalamiko ya Mama Nsangizyo, Waziri Mpina aliagiza Mwendesha mashtaka wa Mkoa wa Geita kuhakiki nyaraka na taarifa zilizoko kuanzia ngazi ya kijiji ili kujiridhisha na malalamiko hayo na kama itabainika kuna ukiukwaji wa sheria, basi serikali itachukua hatua kwa watu wote waliohusika na dhuluma hiyo.

# Wanandoa wadaiwa kuuawa kikatili usiku

Na Gurian Adolf, MPANDA

JESHI la Polisi mkoani Katavi, linawasaka watu wasiojulikana kwa tuhuma za kuwaua kwa kuwachinja wanandoa Noel Mswanya (39) na mkewe Stella Noel (37), wakazi wa Mtaa wa Migazini Kata ya Nsemulwa Manispaa ya Mpanda.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Leonard Makona, tukio hilo lilitokea Jumapili saa 7 za usiku wakati wanandoa hao wakiwa wamelala nyumbani kwao.

Alisema wakiwa wamelalala ndipo watuhumiwa walipovunja mlango wa nyumba kwa kutumia jiwe kubwa maarufu kwa jina la 'Fatuma' na kuingia ndani katika chumba walichokuwa wamelala wanandoa hao.

Baada ya kuingia chumbani walianza kumshambulia Mswanya kwa kumchoma na visu sehemu mbalimbali za mwili kisha kumchinja shingoni, huku mkewe akiwa anaangalia.

Wakati wauaji hao wakiendelea kumchinja, Stella alianza kupiga kelele za kuomba msaada kutoka kwa majirani, lakini wauaji hao hawakuogopa waliendelea hadi walipomuua.

Alisema baada ya kumchinja kumuua, wauaji hao ambao hawakufahamika idadi yao, walianza kumshambulia Stella, lakini alifanikiwa kukimbilia nje ya nyumba, huku akipiga mayowe ya kuomba msaada kwa majirani.

Hata hivyo, Makona alisema wauaji hao waliamua kumfukuza, na kufanikiwa kumkamata umbali wa mita 50 kutoka nyumba yao kisha walimchukua na kumrudisha hadi uani ndani ya nyumba na kumuua kikatili kwa kumchinja.

Makona alisema baadhi ya majirani waliwashuhudia mauaji hayo kwa kuwachungulia kupitia kwenye madirisha ya nyumba zao, lakini hakuna aliyewatambua wala hawakuweza kutoka nje ya nyumba zao kutoa msaada kwa kuhofia usalama wao, kwa kuwa walihisi wana silaha za moto.

Makona alisema miili ya wanandoa hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Katavi kwa ajili ya uchunguzi.



Washiriki wa mafunzo ya msasa kuhusu uwezeshaji mashamba darasa kwa maofisa viungo wa mradi kutoka wizara na timu za uwezeshaji wakiwa katika mafunzo kwa vitendo yaliyoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika vijiji 15 kwenye wilaya za Mkalama, Nzega, Kondoa na Magu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamhuri kumkatia rufani Malinzi

Na Hellen Mwango

UPANDE wa Jamhuri katika kesi iliyokuwa inamkabili Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake, umewasilisha kusudio la kukata rufani kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Desemba 11, mwaka huu.

Hatua hiyo imefikiwa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, kuwasilisha kusudio hilo mahakamani hapo, akieleza kwamba Jamhuri haijaridhika na hukumu iliyotolewa.

Alhamisi iliyopita mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde, iliwahukumu Malinzi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine Mwesigwa, kulipa faini ya Sh. milioni 1.5 au kwenda jela miaka minne.

Malinzi na Mwesigwa walitiwa hatiani kwa makosa mawili ikiwamo moja la kughushi muhtasari na kuwasilisha mhtasari wa kughushi benki.

Pia mahakama hiyo iliwaachia huru mhasibu, Nsiande Mwanga na karani, Flora Rauya, baada ya ushahidi wa Jamhuri kushindwa kuwatia hatiani washtakiwa.

Ilielezwa kwamba waliwasilisha nia hiyo baada ya kutoridhishwa na hukumu pamoja na adhabu iliyotolewa katika makosa waliyotiwa hatiani washtakiwa hao.

Hakimu alisema washtakiwa wote wana hatia katika kosa la kughushi mhtasari na Mwesigwa ana hatia katika kosa la kuwasilisha nyaraka hiyo ya kughushi.

Alisema kosa la kughushi mhtasari washtakiwa watalipa Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili kila mmoja na kosa la kuwasilisha nyaraka hiyo, Mwesigwa atalipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili.

Hata hivyo walilipa faini hiyo na kuachiwa huru Desemba 12, mwaka huu.

# Meno ya tembo, kiboko yampeleka jela miaka 60

**Na Hellen Mwango**

HAIKA Mgao (26), mkazi wa Kimara, Dar es Salaam, amehukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 60, baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na nyara za serikali zenye thamani ya Sh. milioni 69.5.

Hukumu hiyo ilisomwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, baada ya kusikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kevin Mhina.

Alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi watatu wa Jamhuri bila kuacha shaka, imemuona mshtakiwa ana hatia.

Hakimu Isaya alisema mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka 20 jela, baada ya kutiwa hatiani katika kosa la kukutwa na vipande vinne vya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. 66, 210, 000.

Kadhalika atatumikia kifungo cha miaka 20 kwa kosa la kukutwa na meno mawili ya kiboko yenye thamani ya Sh. 3,310,500.

Katika kosa la tatu, mshtakiwa huyo atatumikia kifungo cha miaka 20 jela kwa kujihusisha na biashara ya nyara za serikali. Adhabu hiyo atatumikia sambamba ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama ya mshtakiwa.

Kabla ya kusomwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon akisaidiana na Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, aliiomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kwa sababu za kutoweka kwa tembo kutokana na ujangili, jambo ambalo linaathiri uchumi wa nchi.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anadaiwa kuwa katika kesi ya uhujumu uchumi namba 69/2018 kwa kujihusisha na biashara ya meno ya tembo na kiboko.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo Novemba 19, 2015 katika eneo la Kimara, Wilaya ya Kinondoni (kwa sasa Ubungo).

Ilidaiwa katika shtaka la kwanza, siku na eneo hilo, mshtakiwa alikutwa na vipande vinne vya meno ya tembo vyenye thamani ya dola za Marekani 30,000 sawa na Sh. 66,210,000, bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Pia siku na eneo hilo, Haika alikutwa na meno mawili ya kiboko yenye thamani ya dola za Marekani 3,310,500, bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Katika shtaka la tatu, mshtakiwa anadaiwa kujihusisha na biashara ya nyara za serikali, bila kuwa na leseni kutoka mamlaka husika.



Mafundi wakifanya matayarisho kwa ajili ya kuweka zege kwenye barabara ya Siwa inayoelekea kwenye nyumba za maofisa waandamizi wa serikali Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TMDA yajivunia mafanikio ya Nyanda za Juu Kusini

**Na Augusta Njoji, MBEYA**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imefanikiwa kuongeza maabara hamishika kwa ajili ya uchunguzi na kupima viashiria vya awali ambavyo si salama kutoka mbili hadi nne katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ili kuhakikisha kunakuwa na ubora na usalama wa dawa.

Imeelezwa kuwa maabara hizo zimefanikisha kukusanywa kwa sampuli za dawa mbalimbali, Mkoa wa Mbeya pekee kukipimwa sampuli 744 na moja kubainika kutokuwa na viwango vinavyotakiwa, hivyo kuondolewa sokoni. Kaimu Meneja wa kanda hiyo, Grace Kapande, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari waliofuatana na timu ya maofisa habari wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya katika kampeni ya 'Tunaboresha Sekta ya Afya' inayolenga kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Alisema mamlaka hiyo inahudumia mikoa mitano ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Rukwa na kwamba awali kulikuwa na maabara hizo mbili kwenye mikoa ya Mbeya na Iringa.

"Kwa kipindi cha miaka minne, tumefanikiwa kuongeza maabara mbili katika mikoa ya Rukwa na Songwe na kufikisha maabara nne ambazo zipo hospitali za mikoa zikisimamiwa na mamlaka, tunakusanya sampuli na kupeleka kwenye maabara hizo.

"Tumeongeza maabara hizo mbili na utendaji kazi umeboreshwa zaidi, pia mamlaka kwa kanda hii inasimamia halmashauri 27 katika kulinda afya ya jamii.

"Tunafanya usajili wa bidhaa ili mwananchi atumie bidhaa bora na salama, tunapofanya usajili wa bidhaa, tunaenda tunazipima, iwe ni kiwanda cha ndani au cha nje, tunahakikisha bidhaa tunasajili, tunapeleka maabara kuhakikisha zipo kwenye ubora," alisema. Aliongeza kuwa wamefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali yanayotengeneza, kuhifadhi na kuuza na wamefanikiwa kupima dawa za kila eneo kutokana na wafamasia wa halmashauri kutoa ushirikiano wanapofanya ukaguzi wao kukusanya sampuli hizo na kuziwasilisha.

"Tunakagua kwenye maduka, ubora na usalama wa dawa ambao unategemea uhifadhi, tunafanya ufuatiliaji wa bidhaa sokoni, tuna maabara hamishika nne ambazo kwa kipindi cha nyuma tulikuwa na maabara mbili Mbeya na Iringa. Kwa kipindi cha miaka minne, tumefanikiwa kuongeza maabara mbili Rukwa na Songwe," alisema.

Akizungumzia kuhusu mafunzo kwa wapimaji kwenye maabara hizo, Kapande alisema kabla ya serikali awamu ya tano, kulikuwa na wapimaji 15 kwa kanda nzima lakini sasa wameongezeka na kuwa 30.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Afya, Gerald Chami, akizungumzia kampeni hiyo, alisema itafanyika katika kanda tano nchini kwa taasisi zilizo chini ya wizara ili kuangalia mafanikio ya miaka minne yaliyopatikana katika serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Aliwataka wananchi kutambua sekta ya afya imefanyiwa maboresho makubwa kuhakikisha wanapata huduma bora.

"Nia ya kampeni hii ni kuonesha wananchi namna serikali ya awamu ya tano ilivyoboresha sekta nzima ya afya katika maeneo mbalimbali, ujenzi wa vituo vya afya, maabara, huduma za upasuaji, na wananchi wamerudisha imani yao katika vituo vya kutolea huduma vya serikali," alisema.

# DC Tarime atoa wiki 2 mgodi kulipa wafanyakazi

**Na Hellena Magabe, TARIME**

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, ametoa wiki mbili kwa mgodi wa dhahabu wa North Mara kuwalipa fidia ya kuumia kazini wafanyakazi 12 baada ya kuchelewa kuwasilisha majina ya wafanyakazi hao kuingizwa katika Mfuko wa Fidia (WCF).

Mkuu huyo alimwagiza Meneja Mkuu wa mgodi huo, atekeleze agizo hilo tangu Desemba 14, mwaka huu, vinginevyo hatua zitachukuliwa dhidi yao, baada ya kubaini kuwa ulifanyika uzembe wa kuchukua majukumu yake dhidi ya wafanyakazi hao walioachishwa kazi baada ya kuumia kazini.

Msafiri alitoa kauli hiyo alipokutana na wafanyakazi hao walioachishwa kazi wakiwamo madereva 20 kati ya 44 katika kikao chake na uongozi wa mgodi huo.

Aliyepokea agizo hilo na kukubali kutekeleza ni Meneja Uhusiano Jamii wa mgodi huo, Richard Ojendo na alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu kuchelewa kupeleka majina hayo katika mfuko huo, alisema kuwa yeye anatekeleza agizo la mkuu huyo wa wilaya na sio kujibu maswali ya waandishi.

''Mimi siwezi kuhojiwa, bali ninakwenda kuchukua action (hatua) ya mkuu wa wilaya alivyoagiza sio vinginevyo,'' alisema Meneja Ojendo, huku akiondoka.

Msafiri pia aliagiza askari polisi katika Kituo cha Polisi cha Nyamongo, kuwafunga pingu wafanyakazi wanaodai kupunjwa fidia za malipo ya kuumia kazini katika mifuko walioachishwa kazi baada ya kudaiwa kuwa walifoji tarakimu za hesabu za madai ya fidia katika nyaraka zao.

Waliotiwa pingu na kufikishwa katika kituo hicho cha Polisi ni Samson Masero na Joseph Isarara, ambao wanatarajiwa kupandishwa kizimbani kwa makosa hayo.

Mwenyekiti wa wafanyakazi walioachishwa kazi, Kinyara Nyankoba, walipokutana katika kikao cha wafanyakazi waliopat-

ENDELEA UK 8



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko, akisisitiza jambo wakati wa kikao cha Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa nchini, jijini Dodoma jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Kituo cha Taifa cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura, Ofisi ya Waziri Mkuu, Meja Selestine Masalamando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali yataka mpango bora wa ufungaji migodi

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema kati ya kampuni kubwa na za kati za uchimbaji madini 200 nchini, ni 10 tu zilizowasilisha wizarani mpango bora wa kufunga migodi.

Biteko alisema hayo jana alipofungua kongamano la siku mbili lililoandaliwa na Tume ya Madini Tanzania jijini hapa, akieleza kuwa idadi hiyo ni ndogo.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2018, wamiliki wa migodi wanatakiwa kutoa taarifa ya namna ya ufungaji migodi tangu siku ya kwanza wanapoanza kuchimba na si wanapomaliza uchimbaji.

"Naomba nitoe angalizo kwenu kuwa hayo ni matakwa ya kisheria kuwasilisha mpango wa ufungaji migodi mara mnapoanza shughuli za uchimbaji madini wala si mwisho wa uchimbaji huo," alisema.

Biteko alisema wachimbaji madini nchini wanatakiwa kuweka wazi gharama za kukarabati mazingira na namna ya kufukia mashimo, kinyume chake watachukuliwa hatua za kisheria.

Waziri huyo alisema uchimbaji wa madini popote duniani umekuwa si rafiki wa mazingira kama hausimamiwi vizuri, hivyo baada ya rasilimali inayochimbwa kutolewa, inatakiwa kurudishia mazingira katika hali yake ya awali ili kuyalinda.

Alisema Rais John Magufuli hafurahii kuona wachimbaji wanachimba madini na kuacha mashimo wazi na yanakuwa makaburi ya wananchi, hivyo lazima mkakati wa kurudishia mazingira ubainishwe ili kutoitia hasara serikali baadaye kutumia fedha nyingi kuyarudishia.

Alisema hata wachimbaji wa kati japokuwa ni Watanzania, nao wanatakiwa kutekeleza matakwa hayo ya kisheria ili kulinda mazingira badala ya kutekeleza jukumu hilo kwa tume.

Katibu wa Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila alisema kongamano hilo la kwanza la aina yake kufanyika tangu kuundwa wizara hiyo, limewakutanisha wachimbaji, wataalamu serikalini na taasisi za mazingira ili kujadiliana na kupeana uzoefu namna ya kulinda mazingira kwa kuandaa mpango wa kufunga migodi hiyo.

# Serikali sasa yamiliki KIA 100%

**Na Asraji Mvungi, ARUSHA**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwelwe, amesema Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), sasa unamilikiwa na serikali kwa asilimia 100 baada ya serikali kuwalipa fidia wadau waliokuwa na hisa katika umiliki wa uwanja huo.

Waziri Kamwelwe aliyasema hayo baada ya kuzindua Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Usimamizi wa Uwanja huo (KADCO).

Alifafanua kuwa awali uwanja huo ulikuwa unaendeshwa kwa ubia na wadau watatu tofauti ambao kwa sasa serikali imewalipa Dola za Marekani milioni 5.6 na kuufanya uwanja huo kwa sasa kumilikiwa na serikali kwa asilimia 100.

Aliipongeza menejimenti ya uwanja huo chini ya kampuni ya KADCO ambayo alisema imekuwa ikifanya kazi nzuri na inayoonekana.

Waziri Kamwelwe alisema pamoja na hatua hiyo, serikali imeanza kufanya ukarabati wa idara mbalimbali za uwanja huo ili kuujengea uwezo zaidi ikiwamo kuzifanyia matengenezo ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na kwamba tayari ukarabati wa eneo la kufanyia kazi hiyo unaendelea na ununuzi wa baadhi ya vifaa umeshafanyika.

Kuhusu hatua za kuuwezesha uwanja huo kuvutia mashirika na wadau mbalimbali duniani, pia uko mpango wa kujenga jengo maalumu kwa ajili ya huduma za wageni wanaotaka kuja na ndege zao binafsi, jengo ambalo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi ndege kubwa zikiwamo za Boeing huduma ambayo inapatikana kwenye nchi zilizoendelea.

Waziri Kamwelwe alisema serikali imeanza maandalizi ya kuviwezesha viwanja vya ndege vya Kilimanjaro Songwe na Mwanza kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo ikiwa ni hatua za awali za kuhakikisha kuwa mpango wa serikali wa kununua ndege wa mizigo unakuwa na tija.

Aliitaka bodi mpya ya shirika hilo kuendeleza kazi nzuri iliyofanywa na bodi iliyomaliza muda wake na kuhakikisha kuwa mipango yote iliyoanzishwa ukiwamo wa kuvutia ndege za mizigo unafanikiwa kwa asilimia 100.

Akizungumza baada ya kuzinduliwa kwa bodi hiyo, George Teu na Kaimu Mkurugenzi wa uwanja huo, Mhandisi John Mkoma, aliishukuru serikali kwa kutoa ushirikiano mkubwa wa kuboresha uwanja huo.

Mkoma alisema tayari wameshakamilisha ukarabati wa jengo la matengenezo ya ndege, chumba cha kuhifadhia mizigo na pia miundombinu muhimu ikiwamo mashine za kuzalisha umeme.

Mkoma alisema pamoja na changamoto zilizopo ikiwamo ya ushindani wa kibiashara, uwanja huo umeendelea kujiimarisha katika ukusanyaji wa mapato hatua iliyowezesha mwaka huu, KADCO kutoa gawio la Sh. bilioni moja kwenye mfuko wa serikali.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kibano hiki kitasaidia kudhibiti utoro shuleni

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema kwamba ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha waraka kudhibiti utoro shuleni ambao pamoja na mambo mengine, utapunguza siku na kuwa chini ya 90.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Msaidizi Msingi na Uendelezaji wa Sera wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Yesse Kanyuma, alibainisha kuwa siku zitapunguzwa ili kuwe na siku kidogo mwanafunzi asipoonekana shule hatua zichukuliwe haraka.

Kayuma aliyasema hayo alipomwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Akwilapo wakati wa kufunga kongamano la 14 la Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA).

Hatuna budi kuipongeza serikali kwa hatua hii kwani ni wazi inalenga kudhibiti tatizo la utoro katika shule zetu, na si kumfukuza mtoto bali ni kuwataka wamalize masomo yao.

Inaeleweka kila mzazi, mlezi makini na serikali kwa ujumla wanatamani kuona wanapoanza darasa la kwanza wafike wasome hadi la saba, na watakapoanza kidato cha kwanza wafike kidato cha nne.

Siku 90 zilizokuwa zimewekwa kwa mtoto asipoonekana basi anafukuzwa shule, ndiyo sasa zinatarajiwa kupunguzwa ili kudhibiti utoro ambao unasababisha hasara kwa jamii na serikali kwa ujumla.

Sasa waraka huo utaangalia ni namna gani mwalimu wa darasa, mkuu wa shule, mwalimu wa nidhamu wanaweza kutimiza wajibu wao katika suala zima la usimamizi katika suala zima la utoro shuleni.

Hivyo wakuu wa shule wametakiwa kuwa na kamati hai za nidhamu na ushauri, ili kuondoa hali ya sasa ya fukuza fukuza ya wanafunzi.

Serikali imeona mbali katika jambo hili kwa kuwa licha ya kwamba sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto kadhaa, lakini utoro ni miongoni mwa mambo ambayo yanarudisha nyuma taaluma ya elimu.

Tunaamini utoro ukidhibitiwa katika shule zetu, ni wazi kiwango cha ufaulu kitaongezeka, hivyo taifa litaongeza idadi ya wasomi kwa ujumla.

Tunasema hivyo kwa sababu yawezekana kabisa kwamba utoro umesababisha baadhi ya walimu kuvunjika moyo, kuwa wavivu, lakini hali hatua hiyo sasa italeta mabadiliko.

Ni wazi kwamba baadhi ya shule zimekuwa zikitajwa kufanya vibaya kwenye mitihani ya taifa, zikichunguzwa kwa karibu miongoni mwa sababu za matokeo hayo mabaya ni utoro.

Tunafurahi kuona utoro ukidhibitiwa kwa sababu licha ya kuharibu fursa ya watoto hao kupata elimu, lakini umekuwa ni miongoni mwa vyanzo vya kuzalisha makundi ya uhalifu katika maeneo mbalimbali.

Kuna makundi ya vijana wanaovuta bangi na kutumia dawa za kulevya, wengine wanajihusisha na ukabaji, uporaji na vitendo vya ukahaba, wengi wameibukia huko wakianzia kwenye utoro shuleni.

Kadhalika, utoro umekuwa ukikwamisha walimu katika programu zao za kuwafundisha wanafunzi wale ambao hawawi shuleni kwa kipindi kirefu.


Hali hiyo pia imekuwa ikiwaathiri walimu wakati wa kupimwa ufundishaji wao na wakaguzi kutoka serikalini, hivyo ni matumaini yetu kuwa hatua hiyo italeta tija katika maendeleo ya taaluma.

Kimsingi, siku 90 ni muda mrefu sana kwa mwanafunzi kukosekana shuleni, hivyo kutumia udhaifu huo kwenda kufanya shughuli nyingine zikiwamo za kilimo, uvuvi na nyingine ambazo hazimsaidii zaidi ya kumpotezea uwezo kitaaluma.

Tunatamani kuona taifa letu linakuwa ni taifa lenye kiwango kikubwa cha wasomi, ambao watakuwa wanamudu ushindani katika soko la ajira, hivyo kusaidia kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Abiria achague kinyaa cha 'helmeti' au kifo

Na Mwandishi Wetu

**LICHA** ya utetezi kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 haimlazimishi abiria wa bodaboda kuvaa kofia ngumu au helmeti, ni vyema watu kuvaa kofia hizo kwa ajili ya usalama wao.

Umuhimu unajitokeza zaidi wakati huu wa sikukuu za Noeli na Mwaka Mpya, ambazo zina changamoto nyingi barabarani kutokana na ulevi, uendeshaji mbaya unaosababisha ajali ambazo kwa upande wa pikipiki maisha yangeokolewa kwa kuvaa helmeti.

Ni wakati wa kuamua kupoteza maisha au kujidanganya kuwa unaionea kinyaa au kuivaa kofia ngumu kunakuweka kwenye hatari ya kuambukizwa magonjwa ya ngozi.

Ni upungufu ambao umezungumziwa mara kadhaa kuwa sheria hiyo, inamtaka dereva pikipiki au bajaji kuvaa kofia ngumu, lakini haisemi kuhusu abiria anayetumia vyombo hivyo.

Ndiyo maana pengine ni wakati wa watu kuwajibika na kuamua kulinda maisha yao hata kama kuna upungufu kisheria.

Ripoti za Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, zinaeleza kuwa kutovaliwa kwa kofia hizo, ni sababu za vifo kwenye ajali za pikipiki.

Kwa mfano mwaka 2017 kulikuwa na ajali 1,459 zilizosababisha vifo 728 na majeruhi 1,090, takwimu za ajali kwa mwaka 2018 zilikuwa 876 zilizosababisha vifo 366 na majeruhi 994.

Zaidi takwimu zinaonyesha kuwa kutovaa kofia ngumu kunachangia vifo hivyo.

Msimu huu wa sikukuu una hatari nyingi hivyo ni vyema kuepusha kuwaumiza watoto ambao wanapandishwa kwenye pikipiki lakini bila kofia.

Ni vyema mamlaka za usafiri ardhini Latra na kikosi cha usalama kufikiria uwezekano wa kuwahimiza waendesha pikipikia na wazazi pamoja na walezi kuwa na kofia kwa ajili ya watoto.

Pamoja na kuwahimiza walezi na wazazi kuwa na kofia hizo ni wakati wa mamlaka za kusimamia usafiri kuwa na mikakati ya ukaguzi inayowabana waendesha pikipiki kuwa wasafi na kusafisha kofia ili kuepusha vifo vya abiria wanaokimbia helmeti chafu.

Abiria wanakiri kuwa kofi ngumu wanazopewa na waendesha pikipiki ni chafu, zinanuka, zina ukoko na baadhi zina chawa.

Ni tatizo kwa watu walionyoa kipara wanapata magonjwa yakiwamo mapunye, upele na chawa na vimelea vingine vya maradhi hasa mba.

Licha ya kwamba watu wangependa kuzivaa, lakini waendesha pikipiki ni wazembe na wasiojali kuwa kofia zao zinahitaji kufanyiwa usafi pia na kwa ujumla abiria wao ni wakazi wa miji yenye watu wa aina mbalimbali.

Mathalani Dar es Salaam, Tanga na Pwani ni maeneo yenye joto usafi wa kofia hizo ni muhimu kwa sababu zinabakiwa na jasho la abiria wanaozitumia.

Hata hivyo bora kufanya maamuzi na kuepusha kupoteza maisha. Kama unakusudia kuvaa kofia ni vyema kutembea na kofia nyingine laini ndani badala ya kujidanganya kuwa utachafuka lakini ukapoteza maisha.

Licha ya bodaboda kuchukuliwa kuwa ni hatari na zinaweza kusababisha ajali msimu huu wa sikukuu unawahusu watumia barabara wote ili kujiepusha na ajali.

Ni wakati wa kuendesha kwa makini na kuachana na mazoea ya kutumia babarabara kwa uhuru kupindukia.

Ujeuri huu unaonekana kwa baadhi ya madereva ambao hawajali na kujifanya wafalme wa barabara.

Mbali na kujitumbukiza barabarani hata ndani ya njia za mabasi ya mwendokasi ya Dar es Salaam.

Ubabe na kutumia barabara bila kujali wengine unawaponza watu wasiokuwa na hatia wakiwamo watoto na wenye ulemavu ambao hujeruhiwa na wengine hupoteza maisha.

Polisi wanaweza kusaidia kupunguza athari kwa kutumia kipimo cha ulevi barabarani ili kuepusha hatari ya wengi kupoteza maisha.

## BARUA & MJADALA

# *Rais Magufuli tusaidie Mapinga kuondokana na adha ya daraja*

***Mhariri,***

*SISI wakazi wa Kata ya Mapinga hususan kitongoji cha Kiembeni Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, tunapenda kufikisha kero ya muda mrefu ya kukosekana kwa daraja katika Mto Mpiji, kwa Rais John Magufuli.*

*Kusema kweli kukosekana kwa daraja katika maeneo hayo kunatuathiri sana tunaoishi Kiembeni, Kialaka na maeneo mengine ya Kata ya Mapinga ambao tunatumia njia hiyo kwenda kazini, maeneo ya biashara, kijamii na kufuata huduma katika Jiji la Dar es Salaam kupitia Mbweni wilayani Kinondoni.*

*Wafanyakazi na wafanyabiashara wengi wanaofanya shughuli zao jijini Dar es Salaam wanaishi maeneo ya Kata Mapinga, hivyo mvua zinaponyesha kama hivi sasa eneo la mkondo wa bahari linalopokea maji kutoka maeneo mbalimbali yakiwamo Kibaha na Morogoro linakuwa na maji mengi, hivyo kuzuia wananchi kupita.*

*Mwaka jana wakati Rais Magufuli alipofika kuzindua Chuo cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) eneo la Kiembeni, alielezwa kero hiyo, na aliahidi kuwa atasimamia kuhakikisha daraja hilo linajengwa.*

*Kutokana na ukubwa wa tatizo lilikopo, tunamkumbusha Mheshimiwa Rais wetu kutukumbuka ili daraja hilo liweze kujengwa haraka kwa sababu inafika mahali hata watoto wetu wanashindwa kwenda shuleni maeneo ya Mbweni na Mpiji.*

*Tatizo hili licha ya viongozi wetu kulifahamu kwa muda mrefu akiwamo Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, hakuna jitihada ambazo zimechukuliwa kulitafutua ufumbuzi hadi ulipofika wewe mapema mwaka jana.*

*Ni matumaini yetu kwamba Mheshimiwa Rais anakumbuka kero hii inayotupata wananchi pamoja na askari na wafanyakazi wa Chuo cha JWTZ Kiembeni.*

*Tunaelewa kuwa kazi ya ujenzi wa daraja au kujengwa barabara ya uhakika kutoka Kiembeni kwenda Mingoyo ili kupotoa Bunju kunahitaji fedha nyingi, lakini inafika mahali tunaona kuwa ni bora angalau ukawekwa utaratibu na sisi wakazi tukachangia ili daraja likajengwa na tukaishi katika mazingira ya uhakika na usalama.*

*Sisi wakazi wa Kiembeni,*
*Mapinga, Bagamoyo*

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Wazazi, walezi msipuuze kampeni ya vitamini A

**Na Mary Geofrey**

UPUNGUFU wa vitamini A unatishia afya na uhai wa watoto na wanawake ambao hudhoofika kutokana na upungufu wa kinga ya mwili na kuongeza hatari ya kupata magonjwa.

Kutokana na changamoto hiyo, Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), inafanya kampeni ya kutoa matone ya Vitamini A kwa watoto kuanzia miezi sita hadi miaka mitano kwa watoto wote nchini.

Mikakati mbalimbali ya kukabiliana na upungufu wa Vitamini A imebuniwa na inatekelezwa kitaifa.

Lengo la TFNC kuweka mikakati hiyo ni kukabiliana na upungufu wa vitamin A na madhara yake kama vile magonjwa ya upofu, upungufu wa kinga ya mwili na vifo.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Elifatio Towo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Germana Leyna, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni kuhusu huduma za lishe ya mtoto kwa mwezi Desemba, anasema huduma kampeni hiyo inadumu mwezi mzima.

Anasema huduma hiyo inatarajiwa kuwafikia watoto takribani milioni 8.3 kwa Vitamini A na upimaji wa hali ya lishe na watoto milioni 7.3 kwa dawa ya kutibu maambukizi ya minyoo katika mikoa yote nchini kwa mwezi huu.

Jitihada zinazofanyika kukabiliana na upungufu wa vitamin A na madhara yake ni pamoja na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa vitamin A kupitia vipindi vya redio na televisheni, maonyesho mbalimbali na machapisho.

Aidha, anasema pia ni kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya, uhamasishaji jamii kuhusu uzalishaji, uhifadhi na ulaji wa vyakula vyenye vitamin A kwa wingi na utoaji wa matone ya vitamini A kwa watoto wenye umri kati ya miezi sita hadi miaka mitano mara mbili kwa mwaka.

Katika kampeni hiyo pia wanatoa dawa za minyoo kwa watoto. Kwa sababu maambukizi husababisha matatizo mbalimbali ya afya kwa watoto ikiwamo tatizo la upungufu wa damu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, upungufu wa damu kwa watoto husababisha madhara mbalimbali ikiwamo utapiamlo pamoja na ongezeko vifo vya watoto hususani wenye umri chini ya miaka mitano.

Miongoni mwa mikakati inayotekelezwa nchini ili kukabiliana na tatizo la maambukizi ya minyoo kwa watoto ni utoaji wa dawa za minyoo kwa watoto wa umri wa mwaka mmoja hadi miaka mitano.

Aidha, utoaji elimu kwa jamii kuhusu usafi wa mazingira ili kudhibiti maambukizi ya minyoo na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya.

Dawa zinazotolewa huua minyoo iliyojikita kwenye mfumo wa chakula, hivyo huboresha ufyonzaji wa virutubishi mwilini, hupunguza tatizo la upungufu wa damu kwa watoto na kuboresha ukuaji na maendeleo ya mtoto kwa kuongeza kasi ya ongezeko la uzito na urefu.

Huduma ya chanjo ya matone ya vitamin A na dawa za minyoo hutolewa kwa watoto wote wenye umri kunzia miezi sita kwa mtone ya vitamin A na miezi 12 kwa dawa za minyoo hadi miaka mitano kwa wote.

Anakumbusha kuwa ni wajibu wa kila Mtanzania kutoa elimu kwa wengine kuhusu huduma hii inayotolewa bure nchini kote na kuhamishana kupeleka watoto ili kuondokana na madhara.

Wazazi na walezi wanapaswa kutimiza wajibu wao kufuata ratiba na maelekezo wanayopewa na wataalam wa afya ili kuwakinga watoto wa umri chini ya miaka mitano dhidi ya maradhi mbalimbali.

Kwa mujibu wa TFNC, huduma hiyo inatarajiwa kuwafikia watoto takribani milioni 8.3 kwa vitamini A na upimaji wa hali ya lishe na watoto milioni 7.3 kwa dawa ya kutibu maambukizi ya minyoo katika mikoa yote nchini kwa mwezi huu.

Ili kufikia lengo lililoweka na taasisi ya lishe ni wajibu wa kila mzazi kuitikia wito kwa kupeleka watoto wao kwa ajili ya kuwakinga na maradhi na kusaidia ukuaji wao.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



HABARI KITAIFA

# RC aitaka Nida kuacha urasimu

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mdeme, ameitaka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuacha urasimu badala yake ijipange kikamilifu kwa kuongeza watumishi pamoja na vifaa ili kukamilisha kusajili laini za simu kwa njia za vidole kwa muda ulipangwa na serikali Desemba 31 mwaka huu.

Mdeme aliyasema hayo jana majini hapa wakati wa kilele cha usajili wa laini za simu kwa alama za vidole uliofanyika katika viwanja vya Zimanimoto ambapo mamia ya wakazi wa Manispaa ya Songea waliofika kusajili laini zao za simu.

Alisema wananchi bado wana uhitaji wa kusajili laini zao za simu, hivyo aliiomba Nida kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji kuona umuhimu wa kuangalia kwa makini kuwabaini watu wanaoandikishwa kupewa vitambulisho vya taifa ni raia halali wa Tanzania hasa ikizingatiwa mkoa wa Ruvuma unapakana na nchi za Malawi na Msumbiji.

Alifafanua kila mwananchi ana umuhimu wa kusajili simu yake kwa alama za vidole kwa kuwa mfumo huo utasaidia kuwabaini wahalifu ambao wamekuwa wakitumia simu hizo vibaya.

Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema kampuni zote za simu za mikononi za TTCL, Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel wote wapo katika kuhakikisha kila mwananchi anasajiliwa ipasavyo kwa alama za vidole.

Alisema hakuna mtu atakayeachwa bila laini yake kusajiliwa, na kusisitiza kuwa na ukomo wake ni Desemba 31, mwaka huu.

Aliwahimiza wananchi wa mkoa wa Ruvuma kujitokeza kwa wingi ili kusajili laini zao kwa alama za vidole kwa wakati, na kwamba zoezi hilo halitarudiwa.

Aidha, Mhandisi John aliwaonya mawakala vishoka wanaopita kuwalaghai wananchi na kuwaibia fedha kuwa wanasajili laini za simu pamoja vitambulisho feki vya uraia, na kwamba TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wameanzisha msako wa kuwakamata watu wanaojifanya kuwa ni wafanyakazi wa kampuni za simu za mikononi na TCRA na wanapita mitaani kusajili simu kwa alama za vidole wakati ni matapeli.



Wananchi wakipita kwa tabu kutokana na barabara ya waenda kwa miguu kujaa takataka zilizotelekezwa katika eneo la Tandale kwa Tumbo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hoja nne kumng'oa Mbowe Chadema

INATOKA UK 2

Alisema anaamini uamuzi huo utaleta ufanisi katika harakati za kuleta mabadiliko ya uongozi wa nchi na chama hicho kitapata ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Mwambe pia alisema kama atachaguliwa kushika nafasi hiyo, uongozi wake utahakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika mapato ya chama ili wanachama wafahamu kiwango cha ruzuku na mapato yanayotokana na michango mbalimbali ya wanachama wa chama hicho kilichoanzishwa rasmi Mei 28, 1992.

**HATIMA KINA LISSU**

Akitoa taarifa ya kikao cha Kamati Kuu kwa waandishi wa habari jijini jana, Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alisema kamati hiyo iliyokutana jana, imewapendekeza majina ya Mbowe na Mwambe kwenda Baraza Kuu kujadiliwa kama wanafaa kuwania nafasi ya uenyekiti.

Alisema wajumbe wa baraza hilo wanatarajiwa kuketi leo kwa ajili ya kujadili na kupitisha majina ya wagombea kwa nafasi za mwenyekiti na makamu mwenyekiti Tanzania Bara na Zanzibar.

Mrema alibainisha kuwa kwa nafasi ya makamu mwenyekiti, Kamati Kuu imepitisha majina ya Lissu na Mwakagenda kuwania nafasi hiyo kwa Tanzania Bara na jina la Issa Mohamed kwa upande wa Zanzibar.

Mkurugenzi huyo alisema Mbunge wa Ubungo, Kubenea, aliyekuwa amechukua fomu ya kuwania nafasi ya makamu mwenyekiti Tanzania Bara, ameandika barua ya kujitoa katika mchakato huo kwa madai kuwa anamwamini Lissu kushika nafasi hiyo.

Mrema alieleza kuwa watia nia wote watatu wa nafasi ya makamu mwenyekiti hawakufika mbele ya Kamati Kuu wakati wa kuhoji watia nia, ikielezwa kuwa Lissu yuko nje ya nchi, Mwakagenda yuko Uganda na Mohamed anauguliwa na mtoto wake.

Kutokana na hali hiyo, Mrema alisema kamati hiyo ililazimika kujadili wasifu wa kila mmoja na majina yaliyopendezwa yatakabidhiwa kwa Baraza Kuu linaloketi leo kwa ajili ya mchujo wa mwisho.

Baadhi ya wagombea nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu waliopendekezwa kwenda kujadiliwa na Baraza Kuu ni Patrick Sosopi, Suzan Kiwanga, Pamela Massay, Hemed Ali, Zeud Mvano, Sara Katanga, Betty Masanja na Ahobokile Mwaitenda.

Uchaguzi wa viongozi wa juu wa chama hicho umepangwa kufanyika keshokutwa jijini Dar es Salaam. Kabla ya kutangazwa kwa tarehe hiyo ya uchaguzi, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ilikuwa iliuandikia barua kadhaa uongozi wa Chadema kuukumbusha kuhusu uchaguzi wa viongozi ambao ni matakwa ya kisheria.

# DC Tarime atoa wiki 2 mgodi kulipa wafanyakazi

INATOKA UK 4

wa na majanga hayo na Mkuu wa Wilaya Msafiri na uongozi wa mgodi huo, pamoja na maofisa wa mifuko ya fidia katika ofisi za uhusiano ya jamii ya mgodi huo, alihoji kulipwa fidia zao kienyeji bila kusaini popote huku fedha zikiingia kwenye akaunti zao na kupata ujumbe mfupi katika simu zao za kiganjani.

Alisema walipofuatilia benki walikuta zimetoka mgodini bila maelekezo wala mchanganuo wowote.

Mmoja wa waathirika hao, Irene Suleiman, ambaye alitumikia mgodi huo tangu mwaka 2005 katika sehemu mbalimbali, alisema alianza kupata maumivu ya mgongo Juni 2015 na ilipofika Agosti 2018 hali ilibadilika na kuwa mbaya zaidi na vipimo vya hospitali vilibaini amelemaa na hataweza kufanya kazi ngumu.

Maitarya Masanda, alidai kupooza upande mmoja wa kushoto na kuomba haki itendeke kwa kuwa madai yao ni ya muda mrefu huku wakizungushwa na uongozi wa mgodi.

# Wanafunzi UDSM watishia kuandamana

INATOKA UK 2

Ngole, kuzungumzia suala hilo, akadai tayari walikuwa wamewasili chuoni hapo kwa ajili ya kikao na uongozi wa wanafunzi.

"Tupo hapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye kikao kinachohusiana na mambo hayo ya wanafunzi," alisema.

Jumatano iliyopita, Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP) kupitia Katibu wake, Joseph Malekela, ulisema kama serikali haitaingilia kati mikopo ya wanafunzi, mamia watashindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mikopo.

Malekela alitaja namna bora ya kukabiliana na tatizo hilo kuwa ni bodi kugharamia mahitaji ya wanafunzi ambayo ni ada, badala ya kutoa fedha hizo kwa wachache na wengine kukosa.

Siku iliyofuata, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema bodi ina fedha za kutosha na hadi Jumatano ya wiki iliyopita, ilikuwa imeshapokea Sh. bilioni 186 kutoka serikalini kwa ajili ya malipo ya miezi mitatu iliyoanzia Oktoba.

# Mil. 58/- kukamilisha vituo viwili vya afya

**Na Elisante John,** SINGIDA

BAADA ya serikali kuionyeshea kidole Wilaya ya Iramba mkoani Singida, kwa usimamizi dhaifu ujenzi wa vituo vya afya Ndago na Kinampanda, hatimaye imetenga Sh. milioni 58, kutoka vyanzo vyake vya ndani, ili kukamilisha kazi hiyo.

Mapema wiki iliyopita, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akiwa Manispaa ya Singida, aliitaka wilaya hiyo kufanyia kazi maagizo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, walipofanya ziara mkoani Singida, juu ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

Akizungumza na wanahabari, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Samuel Shilah, alisema baada ya maelekezo ya viongozi hao wa kitaifa kuhusu miradi hiyo, wilaya imepeleka fedha hizo ili zikamilishe kazi zilizokusudiwa.

Alifafanua kuwa kati ya fedha zilizopelekwa kwenye vituo hivyo, Sh. milioni 24 zimeingizwa katika akaunti ya Kituo cha Afya Kinampanda na kiasi kingine cha Sh. milioni 34 akaunti ya Kituo cha Afya Ndago, lengo likiwa kuukabili upungufu wote uliopo.

"Ili kuzidi kujenga imani kwa serikali yetu inayojali wanyonge, tumezingatia ushauri kwa baadhi ya majengo yaliyojengwa kwenye vituo hivi vya afya...tumepeleka fedha na tumenunua vifaa vyote muhimu kukamilisha mradi," alisema Shilah.

Hata hivyo alikemea tabia ya usimamizi dhaifu uliochangia kushindwa kukamilika mapema kwa ujenzi wa vituo hivyo kama ilivyokusudiwa, hali aliyodai ni hujuma kutoka kwa baadhi ya viongozi wa kuchaguliwa wanaorudisha nyuma maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Linno Mwageni, alifafanua kuwa ujenzi unaendelea kwa kasi ili kuondoa dosari zilizoonekana wakati wa ziara ya Samia na Majaliwa.

**Ili kuzidi kujenga imani kwa serikali yetu inayojali wanyonge, tumezingatia ushauri kwa baadhi ya majengo yaliyojengwa kwenye vituo hivi vya afya... tumepeleka fedha na tumenunua vifaa vyote muhimu kukamilisha mradi**

# Daktari kortini madai kuomba mgonjwa rushwa ya ngono

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA Kuu Chakechake, imempandisha kizimbani daktari Massoud Suleiman Abdalla kwa tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa aliyefika hospitali ya Chakechake kwa ajili ya matibabu.

Baada ya mtuhumiwa huyo kupanda kizimbani, alisomewa shtaka lake na mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ramadhan Suleiman Ramadhan.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa alitenda makosa mawili, ambapo kosa la kwanza alilitenda Novemba 21, mwaka huu kati ya saa 3:55 na saa 4:00 asubuhi katika hospitali hiyo, kwa kumdai mgonjwa rushwa ya ngono.

**Mgonjwa huyo alikwenda hospitalini hapo kwa ajili huduma ya uchunguzi wa Ultra Sound.**

Mgonjwa huyo alikwenda hospitalini hapo kwa ajili huduma ya uchunguzi wa Ultra Sound.

Kosa la pili alilosomewa mtuhumiwa ni kuwa siku hiyo hiyo, akiwa muajiriwa wa serikali katika Wizara ya Afya alitumia nafasi yake vibaya kwa kutaka kufanya mapenzi na mgonjwa wake.

Baada ya mtuhumiwa kusomewa shtaka lake na mwendesha mashtaka, alikana na kuiomba mahakama impatie dhamana kupitia mawakili wake, ombi ambalo lilikubaliwa na mahakama.

Hakimu wa mahakama hiyo alilikubali ombi la mtuhumiwa na kumtaka awe na milioni mbili za maandishi pamoja na watu wawili ambao ni watumishi wa serikali wenye kiasi hicho hicho kila mmoja.

Kesi hiyo itaendelea Februari 27, mwakani kwa ajili ya usikilizwaji wa awali.

Novemba 21 mwaka huu Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) kisiwani Pemba ilimkamata daktari huyo kwa tuhuma za kutaka kufanya mapenzi na mgonjwa wake, kama malipo ya huduma ya uchunguzi ya Ultra Sound.



Wanawake kutoka jamii ya wafugaji Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, walionufaika na mitaji ya kufanya biashara wakifuatilia mada za mbinu ya kufanyabiashara, ili waboreshe biashara zao baada ya kupewa fedha na Umoja wa Mataifa Kitengo cha Wanawake (UN Women) Sh. milioni 40 kupitia Baraza la Wafugaji Wanawake (PWC). **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Rai wanawake waliopata fursa kuonyesha njia wenzao mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE waliopata fursa na nafasi za uongozi, wametakiwa kuwainua na kuwaonyesha njia wenzao wanaotarajia kuwania kwenye uchaguzi mkuu mwakani.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wabunge Bungeni (TWPG), Susan Lyimo, ndiye aliyetoa wito huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwenye mkutano uliowakutanisha wabunge, madiwani, wanaharakati kujadili ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi.

Lyimo akizungumzia uzoefu wake wa miaka 15 bungeni katika mkutano huo ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alisema wanawake wajipange, wajiandae kuwania nafasi za uongozi bila kujali changamoto.

"Wanawake wajipange, msisubiri kupangwa, ukisubiri kupangwa utapangwa anapotaka anayekupanga na atakupanga mwisho, lazima tuweke mikakati ya kufikia asilimia 50, na si asilimia 30 iliyolengwa," alisema Lyimo.

Alisema yapo mabadiliko kwani mwaka 1995 wanawake wabunge walikuwa 45, na hivi sasa kuna ongezeko ambapo ni wabunge 145. Balozi Getrude Mongella akiwasilisha mada kuhusu kuimarisha ujasiri wa wanawake, kusimamia ajenda ya maendeleo na kuongeza idadi ya viongozi, alisema waondoe hofu na kujiandaa na mikikimikiki ya uchaguzi mkuu mwaka 2020.

"Tangu tulipoingia mfumo wa vyama vingi tulianza kupunguza ujasiri, wanawake wapya katika siasa na uongozi waache hofu cha msingi kujiandikisha," alisema Mongella.

Alisema jamii inayomzunguka mwanamke ikiwamo familia pamoja na majukumu ya kazi yamekuwa yakimjengea hofu mwanamke kufikia nafasi ya uongozi, hivyo wasishangae kukutana na udhalilishaji na kuombwa rushwa ya ngono.

"Wanawake muimarishe afya zenu kuelekea 2020, sio ifike uchaguzi mkuu afya zimelegalega mara upo kwenye kampeni unaanza kichefuchefu, watapata pa kusemea mwanamke huyu hawezi," alisema Balozi Mongella.

# 'Nitaendelea kuwataja hadharani wadhalilishaji wanawake, watoto'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Wilaya ya Micheweni, Salama Mbarouk Khatib, amesema hataacha kuwatangaza hadharani wanaowaharibu watoto na wanawake kwa kuwadhalilisha hadi hapo watakapoacha tabia hiyo.

Alisema ataendelea kuwatangaza wanaowadhalilisha wanawake na watoto, na kwamba na hiyo inaweza kuwa ni miongoni mwa njia muafaka kupungua kwa matendo hayo yanayoendelea kuwakumba kwa kasi wanawake na watoto wilayani humo.

Aliyasema hayo mbele ya masheha, waratibu wa wanawake na watoto, viongozi wa dini na wananchi wengine alipokuwa akifungua mkutano ulioandaliwa na Idara ya Msaada wa kisheria iliopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria huko Micheweni.

Alisema ameshaanza utaratibu wa kuwataja kwa majina hadharani wanaowadhalilisha au kuwakatili wanawake na watoto, hata kama wana cheo au watu maarufu au viongozi wa madrasa hadi hapo watakapotubu kufanya matendo hayo.

**Mimi nitaendelea kuwataja majina wale wote wenye tabia mbaya ya kuwadhalilishaji na kuwakatili wanawake na watoto na naamini hiyo ni njia moja wapo ya kutokomeza matendo hayo.**

"Mimi nitaendelea kuwataja majina wale wote wenye tabia mbaya ya kuwadhalilishaji na kuwakatili wanawake na watoto na naamini hiyo ni njia moja wapo ya kutokomeza matendo hayo," alieleza.

Katika hatua nyingine, Khatib, alisema matendo hayo yamekuwa magumu kuyaondoa kutokana na kufanyika kwa usiri mkubwa.

Aidha, alisema kitu kingine kinachokwamisha kukomesha vitendo hivyo ni wanafamilia kuendelea kuwa na rushwa ya muhali kwa kuvifanyia suluhu.

"Mtoto akishabakwa au kulawitiwa, hapo huanza kuombana radhi na kuelezwa kwamba aliyefanya tendo hilo ni mwalimu wetu, ni sheikh wetu wa mtaa, hivyo tuyamalize ndio kauli zinazojitokeza baada ya mtoto kubakwa," alisema.

Aliitaka jamii kukataa kuzifanyia suluhu kesi hizo na badala yake wawaripoti watuhumiwa wote kwenye vyombo vya sheria ili ichukue mkondo wake.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Katiba na Sheria Pemba, Mattar Zahor Massoud, alisema uanzishwaji wa Idara ya Msaada wa Kisheria Zanzibar ni njia moja wapo ya kuwasaidia wananchi hasa maskini kupata haki zao.

Alisema wananchi wamekuwa wakipata usumbufu wanapohitaji msaada wa kisheria na wakati mwingine huwajui, hivyo sasa serikali imeshaandaa mazingira rafiki.

Mwanasheria wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Pemba, Shaame Far-han Khamis, alisema sheria haijamkataza mzazi kumrudi mtoto wake anapomkosea, ila kinachokatazwa ni kumdhalilisha.

Baadhi ya washiriki wamelitaka kuharakishwa kwa kesi hasa za udhalilishaji mahakamani, kutokana na kuwavunja moyo mashahidi.



Mwenyekiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Asseny Muro, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kwenye warsha ya ilani ya uchaguzi ya wanawake wanamtandao wa katiba, uchaguzi na uongozi na ujenzi wa pamoja wa mpango mkakati wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mahiga: Kutimiza haki za binadamu kunahitaji mtaji

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Augustine Mahiga amesema kuwa ili serikali iweze kutimiza haki za msingi za binadamu kwa wananchi wake kikamilifu, inahitaji nguvu ya kifedha ili kujenga uchumi imara utakaoweza kutimiza haki hizo.

Balozi Mahiga alitoa kauli hiyo kwenye kongamano la kitaifa la kutathmini hali ya haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni lililofanyika jijini Arusha Desemba 13-14, 2019.

Alisema ili serikali iweze kutekeleza na kutimiza haki za binadamu, ni lazima ijenge mfumo wa uwajibikaji na uwazi ambao utajenga uchumi imara utakaosaidia kutekeleza haki za msingi za binadamu na utawala bora.

Waziri Mahiga alisema kwa kutambua hilo, serikali iliamua kwa dhati kabisa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji kodi kwa kuziba mianya yote iliyokuwa inapoteza mapato ili kupata fedha za kutosha kutoa huduma kwa jamii.

"Serikali imeleta sio tu mageuzi bali imeleta mapinduzi, kuna vitu ambavyo vilihitaji ujasiri wa pekee kuvitekeleza, huwezi kujenga uchumi kama huna fedha, bila kodi huwezi," alisema Mahiga.

Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alisema lengo la kongamano hilo ni kutathmini na kutafakari jitihada zilizofanywa na serikali ya awamu ya tano katika kuwakomboa Watanzania kwenye haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

**Serikali imeleta sio tu mageuzi bali imeleta mapinduzi, kuna vitu ambavyo vilihitaji ujasiri wa pekee kuvitekeleza, huwezi kujenga uchumi kama huna fedha, bila kodi huwezi.**

# NMB kushirikiana na serikali kukuza utalii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeahidi kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha inasaidia harakati za serikali kukuza utalii nchini, ili kuinyanyua zaidi sekta hiyo ambayo inaongoza katika kuchangia pato la taifa na kuingiza fedha nyingi za kigeni ukilinganisha na sekta nyingine.

Ahadi hiyo ilitolewa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na za Kati wa NMB, Filbert Mponzi, wakati wa chakula cha usiku, kilichoandaliwa na Chama cha Waongoza Watalii Tanzania (TATO) na kufadhiliwa na NMB, ikihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda.

Mponzi alibainisha NMB imeshaanza kutoa mikopo ya magari kwa waongoza watalii, lengo likiwa ni kuwawezesha waongozaji kurahisisha majukumu yao na kuvutia watalii zaidi na kukuza pato la taifa.

"Ni mikopo inayolenga kuwawezesha waongoza watalii kufanya biashara ya utalii bila kikwazo na kujiingizia kipato, ikiwa ni pamoja na kulinufaisha taifa kutokana na shughuli za utalii. NMB tumewekeza kwenye Sekta ya Utalii na imedhamiria kutoa rasilimali muhimu za kuwezesha ukuaji wa sekta hii.

Aliongeza kuwa, NMB wanashirikiana na Kampuni ya Hanspaul na RSA, huku akizitaja baadhi ya huduma walizojikita kuzitoa katika sekta ya utalii kuwa ni pamoja na 'Asset Financing,' Internet Banking, Makusanyo na Mapato ya Tanapa na NCAA na kurahisisha malipo kupitia Visa na Mastercard.

Prof. Mkenda alikiri NMB ni wadau muhimu wenye mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya utalii, ambayo inakua kwa kasi zaidi, hivyo aliipongeza benki hiyo kwa kushirikiana vyema na serikali katika kukuza sekta hiyo.

Alifafanua NMB imejipanga vya kutosha kuendeleza ushirikiano na serikali pamoja na wadau katika kukuza utalii nchini kwa kuwekeza zaidi kwenye sekta hiyo, ambayo ni kinara wa uchangiaji wa pato la taifa na kuingiza fedha nyingi za kigeni.

Mkenda aliitaja benki hiyo pamoja na Tato kuwa ni kati ya wabia muhimu katika maendeleo ya sekta hiyo na kwamba serikali itaendelea kushirikiana na wabia hao ili kuibakisha sekta ya utalii kuwa vinara wa uchagiaji wa pato la taifa.

Mwenyekiti wa Tato, Willy Chambulo, alisema chama hicho kitaendelea kushirikiana na benki hiyo, katika kukuza utalii na kuwawezesha waongoza watalii kutekeleza majukumu yao vema kwa ustawi wa sekta hiyo na ukuaji wa pato la taifa.

# CCM kuziba nafasi ya mwenyekiti leo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha leo kinafanya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Arusha, baada ya aliyekuwa anashikilia nafasi hiyo, Loata Sanare, kuteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro hivi karibuni.

Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, aliiambia Nipashe kuwa maandalizi yote yameshakamilika, na kwamba mgeni rasmi atakuwa Katibu wa Oganaizesheni ya CCM Taifa, Pereira Silima.

Kwa mujibu wa Matoroka, wajumbe zaidi ya 900 wanatarajia kushiriki uchaguzi huo utakaofanyika kwenye ukumbi wa Simba uliopo kwenye Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Arusha (AICC).

Aidha, Matoroka aliwataka wagombea watatu waliopitishwa na Kamati Kuu ya CCM ambao ni Dk. Batlida Buriani, Bakari Msangi na Zelote Steven kufanya kampeni za kistaarabu za kushindana kwa hoja na siyo kampeni za kupakana matope.

"Hawa wagombea wote watatu baada ya majina yao kuletwa ofisini kwangu tuliwaita na kuzungumza nao kisha tukawapa barua zenye maelekezo ya utaratibu mzima wa kufanya kampeni, na naendelea kuwasihi wagombea wote kufanya kampeni za kistaarabu," alisema.

Matoroka aliongeza kuwa mgombea atakayebainika kufanya kampeni za kumchafua mgombea mwingine, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake kwa kuwa wagombea wote wana sifa za kushika nafasi hiyo, na hakuna bora kuliko mwenzake, hivyo ni vyema wakaheshimu kanuni na taratibu wakati wa kampeni zao.

"Wagombea hawa watatu wana sifa za kushika nafasi ya uenyekiti, kikubwa wanatakiwa kutambua nafasi wanayopambania ni moja, hivyo ni vizuri wakaachia wapigakura wakafanya maamuzi kupitia sanduku la kura, badala ya kutumia mbinu chafu za kuchafuana kwa kuwa hazitakuwa na mashiko kwa sababu CCM ina intelijensia kali ya kutambua viashiria vyovyote vya kutaka kuvuruga uchaguzi ama kuchafuana," alisema.

Pia aliwataka wana-CCM wote mkoani hapa kuwa watulivu wakati wa mchakato wa kumpata mwenyekiti mpya wa kujaza nafasi hiyo, na chama chao kipo makini kuhakikisha kinatangaza atakayechaguliwa.

Utoaji fomu ulianza Novemba 25, mwaka huu na kuhitimishwa Novemba 27, mwaka huu.

# Mvua yakwamisha ujenzi wa mabweni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UJENZI wa mabweni ya Shule ya Sekondari Loksale wilayani Monduli umesimama baada ya vifaa vya kujengea kukwama kufika kutokana na mvua kuharibu barabara za vijiji vya kata hiyo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Idd Kimanta alipofanya ziara ya kukagua athari ya mvua hiyo kwenye Kata ya Loksale wilayani humo.

**Lakini kwa sasa tunafanya jitihada ili kurejesha mawasiliano na kufanikisha ujenzi wa mabweni wa shule hii kukamilika kwa wakati.**

Alisema mvua zinazoendelea kunyesha zimekwamisha ukamilishaji wa ujenzi wa mabweni ya shule hiyo uliotakiwa kukamilika Desemba 15, mwaka huu.

Alisema jitihada zinaendelea za kuweka vifusi baadhi ya maeneo ili kuunganisha mawasiliano na kuwezesha upitishaji wa vifaa hivyo.

Aidha, alisema mvua hizo zimeleta uharibifu mkubwa kwa kukata barabara inayounganisha kata hiyo na makao makuu ya Wilaya ya Monduli na maeneo ya jijini Arusha.

Kaimu Meneja wa Wakala Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) wa Halmashauri ya Monduli, Mhandisi Janeth Mhokera, alisema mvua hizo zimeleta uharibifu mkubwa wa barabara na kusababisha mawasiliano kukatika.

"Lakini kwa sasa tunafanya jitihada ili kurejesha mawasiliano na kufanikisha ujenzi wa mabweni wa shule hii kukamilika kwa wakati," alisema.

Mtendaji wa Kijiji wa Kata ya Loksale, Abeli Ulomi, alisema hali ni mbaya katika eneo lao kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kukwamisha ukamilishaji wa majengo ya mabweni, kutokana na barabara kuchimbika na baadhi ya maeneo kukatika.

"Mvua hizi zimetukwamisha mambo mengi, lakini kubwa tumeshindwa kukamilisha ujenzi wa mabweni haya ambayo tulitakiwa kukabidhi majengo haya Desemba 15, mwaka huu ili kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 6, mwakani 2020 wanafunzi wakapoanza masomo yao," alisema.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Lucy Laizer, alisema mvua zimeleta athari kubwa na kukwamisha jitihada za ukamilishaji wa mabweni ya Shule ya Sekondari ya Loksale.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na za Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza na wanachama wa Chama cha Waongoza Watalii Tanzania (TATO) kwa lengo la kuhimiza ushirikiano mwishoni mwa wiki jijini Arusha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mangariba wapewa mashine kusaga nafaka

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amesema mangariba 13 wa Kimasai wamenunuliwa mashine ya kusaga nafaka na Shirika lisilo la Kiserikali la Nafgem, ili waingize kipato na kuachana na vitendo vya kikatili vya ukeketaji wa watoto.

Mhandisi Chaula aliyasema hayo juzi, wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Lengast Kata ya Naisinyai, juu ya kupiga vita ukatili wa kijinsia wa kukeketa watoto wa kike.

Alisema mangariba hao wanatoka Kijiji cha Irkujit Kata ya Edonyongijape na alipopatiwa mashine hiyo ya kusaga nafaka, waliahidi kuachana na kazi hiyo, kwani walifanya hivyo ili kujipatia kipato.

Aliwataka wanawake mangariba wanaokeketa watoto wa kike kuacha tabia hiyo, kwani atawachukulia hatua kali watakaoendelea.

"Ebu mjitafakari juu ya madhara mnayosababisha kwa watoto wetu, acheni vitendo hivi na mgeukie shughuli nyingine za ujasiriamali, kuliko kuendelea na ukeketaji huu ambao sio mzuri," alisema na kuongeza:

"Wengi wanafanya hivyo kwa kukosa shughuli za kuwaingizia kipato, mangariba mnapaswa kubadilika kwani mnaweza kuuza hata maziwa kuliko kuendelea kukeketa watoto wa kike, kwani mtafungwa jela."

Hata hivyo, alisema amepata taarifa ya baadhi ya watoto wachanga kukeketwa baada ya kuzaliwa, ili isijulikane ila amemwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Jesca Lebba, ahakikishe wanachunguza hilo kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati zote.

"Bado kuna baadhi ya watu hili suala la ukeketaji halijawaingia kichwani, hivyo wanawakeketa watoto wachanga tukiwabaini tutawakamata na kuwatupa magereza," alisema Mhandisi Chaula.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lengast, Tulilo Paulo, alimuhakikishia mkuu huyo wa wilaya kuendelea kutoa elimu ya kupiga vita ukeketaji kwenye mikutano ya kijiji.

Alisema hivi sasa kwenye mikutano ya kijiji chao kunakua na agenda maalum ya kuzungumzia kupinga vita vitendo hivyo vya kikatili.

Mkazi wa Kijiji cha Lengast, Roza Lembris alisema wananchi wa eneo hilo kwa sasa wanaelimika juu ya ukeketaji na wengi wao wanaachana na tabia hiyo.

Alisema mila potofu zilizopitwa na wakati hazina nafasi tena kwa jamii hiyo ya kifugaji, kwani wanaona madhara yanayopatikana.





# Wanawake wanaonyanyasa wanaume zao waonywa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KUONGEZEKA kwa malalamiko ya idadi ya wanawake wanaotumia vibaya fedha wanazochuma katika vikundi vya benki za jamii vijijini (Vicoba) kunyanyasa waume zao, kumemchefua Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoa wa Kilimanjaro, Hilda Lauwo, na kuonya hali hiyo inavuruga kwa kasi ustawi wa familia.

Lauwo alikuwa akizungumza katika mkutano mkuu wa nane wa Shirika la Kiraia la Tusonge, ulioshirikisha wadau mbalimbali mkoani Kilimanjaro.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Tusonge, Agnatha Rutazaa, akitoa taarifa ya mwaka ya shirika hilo alisema kwa mwaka 2019 wamefanikiwa kuwasaidia watu 47 wenye ulemavu kuanzisha miradi ya pamoja kama vile ufugaji wa nyuki, kutengeneza batiki na sabuni.

**kwa sasa miradi yake katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ikiwamo miradi ya uchumi, haki za binadamu, vicoba shirikishi kwa watu wenye ulemavu na kupaza sauti kutokomeza ukatili.**

"Kupitia mfumo wa sekta ya viwanda, wajasiriamali 90 wakiwamo wanawake 67 na wanaume 23, wamefanikiwa kuanzisha biashara za pamoja kama vile kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku, sabuni, batiki na asali ili kukuza uchumi wao," alieleza Rutazaa.

Pia wamo wanufaika 252 wamefanikiwa kuweka nishati ya umeme wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), umeme jua pamoja na huduma ya majisafi na salama kwenye nyumba zao.

Aidha, Rutazaa alisema katika kuisaidia jamii kufikia malengo yao ya kiuchumi, jumla ya wanufaika 22 ambao ni wanawake wamefanikiwa kimiliki ardhi. Pamoja na mambo mengine, Tusonge imefanikiwa kuanzisha vituo vinne vya maarifa na kujifunza na hivi sasa vinafanya kazi katika maeneo ya mradi kupitia wawezeshaji wenza waliopo kwenye jamii (CBT).

Tusonge inatekeleza kwa sasa miradi yake katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ikiwamo miradi ya uchumi, haki za binadamu, vicoba shirikishi kwa watu wenye ulemavu na kupaza sauti kutokomeza ukatili.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, elimu kupitia miradi hiyo ilikuwa inalenga elimu ya ujasiriamali na ubunifu, vicoba na mfumo wa uendeshaji pamoja na elimu ya awali ya fedha.

Imo pia haki za binadamu ikijumuisha haki za watu wenye ulemavu, watoto, wanawake na jamii kwa ujumla pamoja na elimu ya vitendo inayohusu kilimo na ufugaji, urinaji wa asali, utengenezaji batiki na sabuni.

Kutokana na mkakati huo, Tusonge imefanikiwa kufikia idadi ya wanufaika 6,287, ambapo wanawake ni 4,087 na wanaume 314, huku wenye ulemavu wakiwa ni 314, vijana 943 na watoto 629.



.Askari Mgambo ambao walihitimu mafunzo yao wilayani Muheza Mkoa wa Tanga, juzi, wakipita kwa heshima mbele ya mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanasha Tumbo, katika kiwanja cha kijiji cha Kicheba. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hai yakabiliwa upungufu vituo afya 65%

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WILAYA ya Hai inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vituo vya afya kwa asilimia 65.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Irene Haule, alisema mpaka sasa kuna vituo sita kati ya 17 vinavyohitajika katika kila kata, ambavyo havijakidhi viwango licha ya vituo vitano kumilikiwa na serikali.

Hayo yamo katika taarifa yake aliyoitoa juzi kwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa kituo kipya cha afya cha Longoi kinachojengwa Kata ya Weruweru.

Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia kata tatu za Masama Rundugai yenye jumla ya wakazi 13,116, Kata ya Weruweru yenye wakazi 14,170 na baadhi ya vijiji kutoka kata ya Mnadani.

"Hakuna hata kituo kimoja kinachotoa huduma za dharura za upasuaji, hivyo kuleta hitaji kubwa la ujenzi wa vituo vya afya hasa katika ukanda wa tambarare.

"Katika kata zote nne zilizopo ukanda huo hakuna hata kituo kimoja cha afya. Hali hiyo ndiyo iliyoleta msukumo na maono ya kuwa na kituo cha afya Longoi."

Dk. Haule alisema Wilaya ya Hai ina jumla ya vituo vya kutolea huduma 60 ambavyo kati ya hivyo, vituo viwili ni Hospitali ya Wilaya hiyo na Hospitali Teule ya Machame.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Longoi, Juma Aron, alisema mchakato wa upatikanaji wa eneo hilo ulianza kwa kuzingatia mahitaji halisi ya eneo la kujenga kituo cha afya lenye ukubwa wa ekari 8.4.

Wakiwa katika eneo hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, aliwaonya wakazi wa vijiji vinavyouzunguka mradi huo wasithubutu kujaribu kuuhujumu kwa kuiba vifaa vya ujenzi.

Sintoo alieleza katika kituo hicho cha afya kilichopo umbali wa kilomita 23 kutoka Hospitali ya Wilaya, wanufaika wakubwa wa kituo hicho kipya ni wananchi wa vijiji vya Mbatakero, Longoi, Kikavu Chini na Kawaya.

# Mchungaji aiasa jamii kuhusisha watoto ngono

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MCHUNGAJI Elirehema Massawe wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, amewaonya wananchi wa Kata ya Gararagua, Wilaya ya Siha kuacha kuwaumiza watoto kwa kuwahusisha katika shughuli za ngono.

Alikuwa akihubiri jana kwenye ibada ya ubarikio wa kipaimara iliyofanyika Mtaa wa Wiri.

"Ndugu zangu washarika wa Wiri, nasikitika kusema hali ni mbaya huku Gararagua, juzi tumebariki watoto kule Mtaa wa Lengomu, mtoto badala ya kuwa faraja katika familia, ameachwa baada ya kubarikiwa amezunguka usiku kucha na amefanyiwa ukatili usioelezeka.

Mchungaji Massawe aliongeza: "Nawaambia hasa ninyi ndugu zangu kutoka jamii ya wafugaji, mtasukumwa ndani kwa kuchumbia watoto hawa katika umri mdogo. Miezi michache iliyopita mlisikia Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilisema ni marufuku mtoto chini ya miaka 18 kuolewa."

Alionya kuwa watoto hao licha ya kupata kipaimara, bado ni wadogo na wanahitaji malezi na makuzi sahihi ya kielimu na kiroho ili kutimiza ndoto zao za maisha.

Oktoba mwaka huu, Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilitupilia mbali rufani ya serikali iliyokuwa ikipinga hukumu ya Mahakama Kuu iliyobatilisha vifungu vya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto wa kike chini ya umri wa miaka 18 kuolewa.

Wakati uamuzi huo ukiwa umepitishwa, mkoa wa Kilimanjaro umeunda majukwaa ya vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi kwa kila wilaya ili kukabiliana na matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Kwa sasa wanawake wa Kilimanjaro chini ya Shirika la Kwieco linalojishughulisha na haki za binadamu na jinsia, wanaendelea kutoa elimu kuhusu haki za mwanamke na mtoto wa kike kupitia mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto.

Mratibu wa mradi huo, Veronica Ollomi, akizungumza na wanawake hao, alisema lengo hasa ni kuwaelimisha kwanza kutambua ukatili wa kijinsia upo lakini ni mikakati gani na mbinu gani wanayoweza kutumia ili kupambana na matukio hayo.

Zaidi ya wanawake 4,000 wa mkoa wa Kilimanjaro wanaandaliwa kutumika kama askari kanzu wa kuchimba na kuibua matukio ya ukatili wa kijinsia yanayotishia ustawi wa jamii katika halmashauri saba za mkoa huo kwa sasa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 17, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15




**Vyeti vya kuzaliwa, Takukuru kutumika kuufyeka 'muhali', ndoa utotoni Mafia**

Ukurasa 14




## JE, WAJUA?
Anastrozole tiba inayozuia kusambaa saratani ya matiti



Ukurasa 18

## Wakulima, wafugaji walivyonyweshwa dawa iliyokomesha migogoro ya ardhi



# KITETO BILA MITO WAANZA UMWAGILIAJI

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI
## CHARLES KAYOKA

# Polisi wavunja mtandao uliouza magari Malawi




Askari Polisi akifanya doria barabarani. **PICHA: MTANDAO.**

USHIRIKIANO ni suala la muhimu katika kutekeleza jambo lolote liwe la kijamii, au kiuchumi kwa lengo la kuwawezesha wanajamii kufikia malengo ya maendeleo wanayotarajia.

Ni kwa maana hiyo hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Hamis Issa, anawataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika operesheni, doria na misako mbalimbali ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao katika maeneo yao na mkoa mzima.

Anasema kufikiwa kwa malengo ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao mkoani Njombe kumetokana na ushirikino wa Jeshi la Polisi na wananchi ambao uliwezesha mafanikio ya operesheni mbalimbali.

Mathalani, kukamata bastola moja aina Chinese pistol ikiwa na kasha lenye risasi saba.

Kamanda Hamisi, alisema kuwa misako na doria zikifanywa kwa kushirikiana na wananchi zinakuwa na manufaa na mafanikio kwa kuwa raia huwafichua wahalifu hivyo kurahisisha ukamataji wao na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria jambo ambalo huwafanya wananchi wa mkoa wa Njombe kuendelea na shughuli zao za maendeleo bila hofu ya uhalifu.

Operesheni na misako na doria zinazofanyika katika maeneo mbalimbali mkoani Njombe kwa kushirikiana na wadau na wananchi zimefanikiwa kubaini na kuzuia mtandao wa wizi wa magari na pikipiki uliokithiri katika mikoa wa nyanda za juu kusini.

> Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, linatoa wito kwa wananchi kuendelea kuliamini na wasisite kutoa taarifa za siri zitakazowezesha kufanikisha, kutokomeza mtandao mzima wa uhalifu na wahalifu.

Mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Njombe Ruvuma, Katavi na Songwe.

Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa sita ambao wamekuwa wakijihusisha na matukio ya wizi wa magari na bodaboda katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Njombe na kwenda kuuza nchi za jirani ikiwamo Malawi.

Aidha, kufuatia mafanikio hayo, wananchi katika mkoa huo, walilipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa linayofanya kwa kuhakikisha kuwa mkoa unakuwa salama na wahalifu wanakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, linatoa wito kwa wananchi kuendelea kuliamini na wasisite kutoa taarifa za siri zitakazowezesha kufanikisha, kutokomeza mtandao mzima wa uhalifu na wahalifu.

Alisema ili kudhibiti matukio kama haya jeshi hilo mkoa wa Njombe litaendelea na operesheni, doria pamoja na misako pia watahusisha mikoa ya jirani kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia ili kuweza kuzuia na kubaini watuhumiwa wote wanojihusisha na vitendo vya wizi wa magari na pikipiki.

## JE, WAJUA?
# Anastrozole tiba inayozuia kusambaa saratani ya matiti

ANASTROZOLE ni dawa inayopunguza nusu ya hatari ya saratani ya matiti kwa mwanamke inayoendelea kufanya kazi muda mrefu hata pale mwanamama anapoacha kuitumia.

Watafiti wanasema kuwa dawa hiyo huzuia uzalishwaji wa homoni za oestrogen, zinazochochea uvimbe wa saratani ya matiti.

Tayari dawa hiyo inatumiwa katika hospitali za umma, nchini Uingereza lakini watafiti katika Chuo Kikuu cha Queen Mary jijini London wanasema ni wanawake 10 wanaoitumia.

Watafiti wa saratani nchini Uingereza wanasema kuwa matokeo ya uchunguzi wao yalikuwa ni ya kuaminika.

### ANAYEWEZA KUITUMIA

Anastrozole inaweza kutolewa tu kwa wanawake ambao hawana uwezo wa kujifungua kwani dawa hii haiwezi kuzuia utendaji kazi wa homoni za uzazi oestrogen miongoni mwa wanawake wenye umri mdogo.

Tayari Anastrozole inatumiwa sasa kama tiba pale saratani ya matiti inapogunduliwa, lakini majaribio ya dawa hii yanaangazia zaidi juu ya kuzuia kansa inayojitokeza kwa mara ya kwanza.

Utafiti wa awali, umeonyesha kuwa anastrozole huzuwia hatari ya saratani ya matiti kwa nusu wakati mwanamama anapoitumia kwa miaka mitano.

Lakini sasa, majaribio yaliyofanyika kwa wanawake 3,864 yanaonyesha kuwa kwa wale wanaoitumia asilimia 49 walikuwa na saratani, na hata miaka saba baada ya kuitumia.

Kwa maana nyingine faida za dawa hii zinadumu.

Matokeo ya utafiti huu yalichapishwa katika jarida la kitabibu la Lancet yaliowasilishwa katika Mkutano wa San Antonio wa saratani mjini Texas Marekani.

"Saratani ya matiti ni saratani inayowakumba zaidi wanawake na inaendelea kuongezeka kwa haraka," Prof. Jack Cuzick, Mkurugenzi wa Taasisi ya Wolfson ya dawa za kuzuia magonjwa katika Chuo Kikuu cha Queen Mary mjini London, aliiambia BBC: "Kwa sasa tuna dawa ambayo inaonekana kufanya kazi vema, ikiwa na athari kidogo."

### UPATIKANAJI

Wanawake walio na umri wa kuzaa walio katika hatari ya kupata saratani ya matiti, kutokana na historia ya familia na hatari nyingine wamekuwa wakishauriwa kumeza dawa hiyo tangu mwaka 2017.

"Idadi ya wanaozitumia imekuwa ni ya chini sana," anasema Prof. Cuzick.

"Kwa sasa ni takriban asilimia 10 ya wanawake hawa na tunafikiri idadi yao ingepaswa kuwa ni ya juu."

Moja ya masuala yanayofikiriwa ni kwamba kuna hofu ya madaktari kuhusu ukweli ikiwa kweli kuna faida ya muda mrefu ya dawa hii.

Suala jingine ni athari zake kama vile maumivu ya viungo, kutokwa na upele na ukavu sehemu za siri za wanawake.

Hata hivyo, utafiti ulionyesha kuwa asilimia 75 ya wanawake waliopewa anastrozole waliendelea na dawa hizo vema, ikilinganishwa na 77.

Wasomi wanasema hii inaonyesha kuwa athari za dawa hii sio mbaya za kuwafanya wanawake kuacha kuitumia dawa.

### KUZUIA SARATANI

Saratani ni seli zilizoharibiwa. Hata hivyo, seli zenye afya haziwezi kuwa na saratani mara moja. Badala yake hupitia mchakato mbalimbali wa kumeguka ambao hatimaye huzigeuza kutoka hali ya kuwa zenye afya na kuzifanya kuwa zenye saratani.

Anastrozole inaonekana kuwa na uwezo wa kuua baadhi ya seli ambazo zilianza safari ya kuwa na saratani.

"Inarudisha ugonjwa nyuma kwa miaka 20 na lazima uanzie mwanzo kutengeneza saratani tena jambo ambalo linaweza kuchukua muda mrefu," Prof. Cuzick anaiambia BBC.

Swali jingine linaloibuka hii itaondoa haja ya matibabu ya kuondolewa matiti? Hapana.

Dawa za kuzuwia saratani ya matiti inamaanisha kuondoa matiti sio njia pekee ya kuzuia saratani.

Lakini, baadhi ya wanawake wako katika hatari ya juu zaidi ya kupata saratani ya matiti kiasi kwamba hatari inaweza kuwa kubwa zaidi hata kwa dawa.

Wanaweza kuamua kufanyiwa operesheni ya kuondoa ambalo bado ni chaguo bora.

Siku zijazo inatumainiwa kuwa utafiti utaweza kubashiri ni nani mwenye uwezekano mkubwa wa kunufaika na dawa au kuwa na walau kupata athari kidogo za dawa, jambo ambalo litasaidia katika uchukuaji wa maamuzi ya aina hiyo kuwa rahisi.

***BBC***




Dawa ya kansa. **PICHA: MTANDAO.**

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Vyeti vya kuzaliwa, Takukuru kutumika kuufyeka 'muhali', ndoa utotoni Mafia



Wanachama wa Sauti ya Wanawake Mafia ya Sawama wa Kijiji cha Kiegeani, wakijadili mambo ya ustawi na maendeleo ya kinamama na watoto. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

KWA miaka mingi mabinti wakiwamo wanafunzi walipewa ujauzito na hatima zao kuvurugwa, lakini kesi hazifiki polisi wala mahakamani, kisa familia ya mwanaume na ya binti 'zilitengeneza.'

Kutengeneza huko ni kutafuta suluhu baina ya ndugu wa binti aliyebakwa na kupata mimba au mtoto aliyelawitiwa kinachoendelea watuhumiwa kulipwa fedha au kupewa zawaid ili wasichukue hatua.

Wengine pia hukubaliana kuwa kama wakifika mahakamani washtakiwa na washtaki wasijitokeze na hata wakafika kortini wasitoe ushirikiano hivyo kesi hufutwa kwa kukosa ushahidi.

Ndiyo 'muhali'. Kutengeneza mambo na kufichiana siri. Ndiko kumuonea haya au aibu mtuhumiwa na jamaa zake na kumsaidia kwa kila namna asiwajibike kwa makosa, licha ya kwamba kambaka binti au kulawiti mtoto, kumwambukiza maradhi, kampa mimba na kumkwamisha kimasomo na kimaisha.

Katika ziara ya hivi karibuni kisiwani Mafia, moja ya mambo yanayotajwa na wenyeji na wadau wa kutetea haki za wanawake na watoto ni kutawala kwa muhali ambayo ni desturi ya kufichiana siri kwa kisingizio cha kujuana, kufahamiana na kuepuka kuwa na maadui.

Miongoni mwa watetezi wa haki za mabinti, watoto na wanawake ni shirika la ActionAid, ambalo linathibitisha kuwa muhali ni tatizo na jitihada zimefanyika kuumaliza.

Samuel Meseiaki ni Mratibu wa Action Aid, wilayani Mafia, anasema mradi wa Kuhamasisha Usalama wa Wasichana Shuleni (Stop Violence Against Girls in Schools -SVAGs), ndiyo fimbo ya kutandika muhali.

"Ni mojawapo ya wilaya ambazo wanafunzi wasichana wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kuzifikia ndoto za elimu. Wasichana 10 hukatishwa masomo kila mwaka kutokana na mimba za utotoni na unyanyasaji na ukatili wa wanaokutana nao nyumbani na ndani ya jamii." Anasema.

Aidha, mmoja kila wasichana wanne hukutana na unyanyasaji wa kihisia kutoka kwa ndugu na jamaa zake, unaopunguza kujithamini na msukumo wa kusoma hivyo kuchangia kushusha elimu miongoni mwa mabinti kwa vile huchukuliwa kama ni kupoteza rasilimali.

"Si hivyo tu wasichana wanaohudhuria darasani wanakutana na changamoto kwani kila msichana mmoja kati ya 10 wanaripotiwa kunyanyaswa kingono, wakati zaidi ya nusu hunyanyaswa na walimu shuleni," anasema Mesiaki.

"Mwaka 2018 wasichana 8 wa sekondari walipatikana na mimba wakati mwaka 2019 walikuwa 10. Tatizo kubwa kwenye elimu hii ni umbali mrefu baina ya shule na nyumbani na kukosa mabweni yote yakichangia ukatili dhidi ya wasichana, mimba za utotoni na ufaulu wa chini miongoni mwa mabinti," kwa mujibu wa Mesiaki.

Wasichana kupata mimba, kuolewa utotoni, kunyanyaswa na kukwamishwa kitaaluma na kimaendeleo kumechangiwa na muhali ambao umefichiana siri watuhumiwa.

Kwa mujibu wa Mohamed Mahadhi, Mtendaji Kata ya Miburani wilayani Mafia muhali unatokana na wazazi au jamaa za mabinti au watoto walionyanyaswa kutanguliza huruma kwa mhalifu.

"Mzazi anafikiria eti nikimshtaki mtuhumiwa atanitazamaje? Familia yake itanichukuliaje jamaa zake watanionaje? Ndiyo mbeleko iliyoubeba na kuulea ukatili wa kijinsia uliosababisha mimba na ndoa za utotoni Mafia na kwingineko nchini."

Wengine huhofia iwapo aliyempa binti ujauzito atapelekwa gerezani binti atakosa mume na mtoto atakayezaliwa hatamfahamu baba yake anasema.

"Wakazi wa Mafia wanapenda ndoa. Wanadhani huo ubakaji unaleta ndoa bila kujua kuwa kijana huyo hakuwa na nia bali anarubuni mabinti ili kuwatumia kingono," anasema Mahadhi.

Anaungwa mkono na Selemani Haji, Ofisa Mtendaji wa Mibulani, anayesema kuwa katika familia nyingine wanaoshikia bango kufichiana wanaotaka kuwashitiki watuhumiwa na kuyamaliza kiundugu.

Anasema wapo wengine wanaowabembeleza na kuwashawishi mabinti wasiwataje na kukana kuwa wamepewa mimba na kijana au mwanaume anayetuhumiwa, hivyo kesi hukwama kuendelea.

Haji anasema kesi nyingi hufika kwenye ofisi za vijiji, lakini zikifikishwa kwa viongozi wa elimu kata na polisi mambo yanageuka pengine baada ya mabinti na kinamama kupewa fedha na ahadi za ndoa au malezi ya mtoto akizaliwa.

Nipashe inazungumza na Sauti ya Wanawake Mafia (Sawama), asasi ya kinamama inayowaunganisha wanawake kisiwani humo iliyoundwa na Action Aid, ambayo pia inashirikiana na shirika hilo kutekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wasichana shuleni wa SVAGs.

Katika mjadala huo uliofanyika kwenye katika kijiji cha Kiegeani kinamama wanasema jamii inalea muhali kwa kuwaficha na kuwatorosha wabakaji na wanaolawiti watoto.

Wanasema Mafia ni kisiwa na hakuna namna ya kuondoka bila kutumia boti au mitumbwi na kinachofanywa ni kuwasaidia kutoroka kwa kuwaficha chini ya majahazi na boti ili wasionekane.

> "Si hivyo tu wasichana wanaohudhuria darasani wanakutana na changamoto kwani kila msichana mmoja kati ya 10 wanaripotiwa kunyanyaswa kingono, wakati zaidi ya nusu hunyanyaswa na walimu shuleni," anasema Mesiaki.

Wengine huwapeleka kwenye visiwani vingine kwa kutumia mashua zao, lakini kabla ya hayo kinamama wengine huwafuata watuhumiwa na kuwaambia watoroke na kukimbia kwa vile wanasakwa na watakamatwa na kushtakiwa.

Wanasawama wanasema licha ya wazazi na jamaa za watuhumiwa kuwatorosha vijana wao ili kuondoa ushahidi jamii nayo inasaidia kuwatetea na kutoa kila msaada ili wasishtakiwe.

### KUKOMESHA MUHALI

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mafia, Yohana Lwenda, anasema zama hizi wadau wengi wanahusika kwenye kutokomeza muhali wakiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) ambayo inachukuliwa hatua ya kuficha watuhumiwa kuwa ni sawa na rushwa.

Anasema Takukuru inachunguza inakuwaje nje ya mahakama kuwe na maelezo yanayotofautiana na ushahidi unaotolewa kortini na kushirikiana na polisi kuujua ukweli na kuendeleza kesi, utaratibu unaotokomeza muhali.

Licha ya kwamba Ofisi ya Takukuru wilayani Mafia, haikutaka kuzungumzia suala ilipoulizwa na Nipashe, ukweli ni kwamba ushiriki wa Takukuru kitaifa kwenye kesi hizo zilizokuwa zinakwamishwa na jamii inayokataa kutoa ushahidi, huenda ukaleta pambazuko jipya la kuutokomeza.

### VYETI VYA KUZALIWA

Pamoja na serikali na asasi binafsi viongozi wa dini nao wamejiunga kwenye vita vya kuficha siri za washtakiwa wa ubakaji na kunyanyasa watoto.

Hakuna ndoa bila cheti cha kuzaliwa, anasema Mjumbe wa Sawama na kueleza kuwa hayo ni makubaliano yaliyofikiwa na viongozi wa kijamii na kiserikali wilayani humo.

Anapoulizwa utaratibu huo, Padri Francis Macrello Massawe wa Parokia ya Teresia wa Mtoto Yesu Mafia, anasema viongozi wa dini wamekubaliana hakuna kufunga ndoa bila kuhakiki vyeti vya wanandoa hao.

Anasema hata hivyo, hawajawahi kukutana na wanandoa watoto katika kanisa hilo, hata kabla ya viongozi wa dini na wa serikali kukubaliana kuwasilisha vyeti vya kuzaliwa.

### USHAURI

Ili kutokomeza muhali kinamama wanachama wa Sauti ya Wanawake Mafia, wanashauri Bunge kutunga sheria zinazorekebisha taratibu za ndoa za kimila na kuziwekea pia kipengele cha umri wa kuolewa ili uwe zaidi ya miaka 18.

Kutunga sheria ndogo ndogo kwa vijiji na halmashauri kuwabana wanaowapa mimba wanafunzi na wanaonyanyasa watoto kingono.

Aidha, sheria hizo zitumike kuwabana wazazi na walezi wanaoficha taarifa za unyanyasaji na ubakaji watoto.

Aidha, kujengea mabweni shuleni na kuwapatia wanafunzi chakula, maji na mahitaji muhimu ili kuwaepusha na mitego inayosababisha warubuniwe mitaani.

Pia wadau na serikali waendeleze juhudi za kukemea unyanyasaji na kuhamasisha haki za watoto.

TEKNOLOJIA

# Kiteto bila mito waanza umwagiliaji

## Wachimba visima virefu, 1,000 kufaidi

**Na Crispin Samson**

SEKTA ya kilimo ni mojawapo ya vipaumbele vya serikali ya awamu ya tano ili itoe mchango chanya wa kuchochea ukoaji wa uchumi wa kati na maendeleo ya viwanda.

Kwa mujibu wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kinachangia asilimia 28.7 ya pato la taifa na kuajiri asilimia 65.5 ya Watanzania hadi mwaka 2017.

Hata hivyo, sekta hiyo inakabiliwa na changamoto lukuki kama kutegemea mvua, teknolojia hafifu, ulimaji holela, pembejeo duni, ukosefu wa mitaji na magonjwa ya kitropikali.

Kata ya Matui iliyopo Kiteto Mkoa wa Manyara ni mojawapo ya maeneo yanayokabiliwa na changamoto hizo kama kutegemea mvua, pembejeo duni, ukosefu wa mitaji na upungufu wa masoko.

Ili kumaliza tatizo hilo, viongozi wa Kiteto kwa kushirikiana na kampuni ya Jenga Afya Tokomeza Umaskini (Jatu), inatoa fursa kwa watu kuwekeza kwenye sekta ya kilimo kwa mfumo wa kununua hisa.

Jenga Afya Tokomeza Umaskini kampuni hiyo ya wazawa imeanzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwa teknolojia ya maji ya kisima.

**MAJI KISIMA**

Wakulima wengi wanadhani kuwa kilimo cha umwagiliaji kinafanyika kutoka kwenye chanzo asilia kama mto, ziwa au mabwawa. Kutokana na maendeleo ya teknolojia miundombinu ya kumwagilia inaweza kuchimbwa na kuandaliwa kutoka sehemu yeyote bora iwe na mwamba wa maji.

Hivi karibuni, akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji uliofanyika Kiteto mkoani Manyara eneo ambalo linatekeleza mradi wa kilimo cha kisasa, Mkurugenzi Mtendaji wa Jatu, Peter Isare, anasema wameuanzisha kwa matarajio ya kujenga visima vya maji ya ardhini vitakavyochimbwa na kuwekewa mabomba na mitambo ya umwagiliaji ya kisasa ili kufikisha maji kwenye mashamba ya wakulima wanachama wake.

Visima hivyo vitakavyotumia teknolojia ya kisasa ijulikanayo kama `centre pivot irrigation system' ya umwagiliaji, vitakuwa na ukubwa wa mita 300 kwenda chini uwezo wa kuhifadhi lita 300,000 za maji kwa mara moja yatakayotumika kumwagilia mashamba yenye ukubwa wa heka 500.

Aidha, anasema mitambo mikubwa ya umeme yenye uwezo wa kurusha maji mbali hadi kufikia yalipo mashamba itafungwa kwenye visima hivyo ili kuwezesha umwagiliaji kufanyika kikamilifu.

Uchimbaji wa visima vikubwa na vya kisasa vitakavyotumika kwenye umwagiliaji, umeanza anasema Isare na kuongeza kuwa kuna faida nyingi kwenye mradi huo ikiwa ni pamoja na wataalamu kusimamia mashamba, kupatiwa mikopo isiyo na riba na uhakika wa soko.

"Kupitia mradi huo, wakulima wa Wilaya ya Kiteto watapata fursa ya kupewa mafunzo maalum ya mbinu za kilimo bora kitakachowasaidia kupata mazao mengi na yenye tija, tofauti na kilimo cha sasa ambapo wengi wao wanalima bila kuzingatia kanuni za kilimo bora za kilimo," alifafanua.

Isare anaeleza kwamba wakulima wa wilaya hiyo wamekuwa na dhana kwamba kulima kwenye eneo kubwa ndipo utapata mazao mengi, jambo ambalo sio kweli, bali unaweza kulima kwenye heka moja na kupata mazao mengi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kampuni imejipanga kujenga kiwanda cha kuchata mahindi na alizeti na kutengeneza vyakula vya aina mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jatu, akizungumza kwenye uzinduzi huo , anasema wamedhamiria kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kuwakomboa wakulima na wananchi wa maeneo hayo na umaskini unaowakumba.

"Ipo fursa ya uwekezaji kwenye eneo hilo kwa kuwa ardhi yake ina rutuba lakini ukosefu wa mvua ndilo tatizo na kwamba wanatarajia kuanza kilimo cha umwagiliaji mapema mwaka ujao, ambapo kwa awamu ya kwanza wataanza mahindi na alizeti kwenye eneo la hekta 500 zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo.



Kazi ya kuchimba kisima kwa ajili ya umwagiliaji ikiendelea kwenye maeneo ya mradi huo mkoani Manyara.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jatu PLC Peter Isare, akizungumza na wananchi pamoja na wakulima watakaonufaika wakati wa uzinduzi wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwa visima katika Wilaya ya Kiteto mkoani humo. :**PICHA CRISPIN SAMSON.**

"Kampuni inatarajia kutumia Sh. bilioni 7.5 kunufaisha wakulima zaidi ya 1,000 wa wilaya hii na ya Kiteto," anasema Isare na kuongeza kuwa umwagiliaji utawapa fursa wakulima wa wilaya hiyo na wengine wanaotoka nje ya sehemu hiyo kulima mara tatu ndani ya mwaka mmoja, na hivyo kukuza kipato kwa haraka.

Si hivyo tu pia ni kuendeleza sekta ya kilimo nchini na kuchangia maendeleo ya viwanda yanayotokana na kuzalisha malighafi zitokanazo na kilimo.

Isare anafafanua kwamba kwa awamu ya kwanza wataanza kulima kwenye heka 500 na kuongeza eneo hadi kufika heka 1,500.

"Wakulima wa Wilaya ya Kiteto wanakabiliwa na tatizo la ukame unaoathiri kilimo na ufugaji na kusababisha kukosekana kwa tija kwenye mazao wanayoyalima," anasema.

Pili wakulima wa wilaya hii hawana elimu ya kilimo bora kinachozingatia kanuni na vipimo vya ulimaji wa kisasa unaosaidia kupata mazao mengi na bora kwenye heka moja.

"Kwa mfano, wakulima wamekua wakipata takribani magunia matatu au manne kwenye heka moja ya mahindi, tofauti na ambavyo mradi umelenga kupata magunia 40 hadi 45 kwenye heka moja kwa kutumia njia bora na ya kisasa," alieleza.

Mkurugenzi anasema lengo la mradi huu ni kuchochea tija kwenye mazao ya biashara ikiwamo mahindi na alizeti ili yaweze kuzalishwa kwa wingi na kupata soko kwa walaji," Mkurugenzi anasema.

**WILAYA KUNUFAIKA**

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Wilaya ya Kiteto, Tamim Kambona, anasema mradi huu umekuja wakati muafaka kwani utawasaidia wakulima wa Matui kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua na kuhamia kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Anaongeza kuwa Wilaya ya Kiteto inakabiliwa na ukame wa muda mrefu unaoathiri uzalishaji wa mazao na kusababisha wakulima kukosa kipato cha uhakika.

Mbali na hayo, Mkurugenzi anasema, uwepo wa ukame kwenye wilaya hiyo umeathiri upatikanaji wa mapato ya halmashauri ya wilaya kwani imekua ikitegemea kilimo kwa asilimia 95 kwa ajili ya mapato ya ndani na ufugaji wa asilimia 35.

Kambona anasema ujio wa mradi huu wa umwagiliaji utatoa fursa kwa vijana wa kata ya Matui kuboresha maisha kwa kujipatia ajira kwenye viwanda vya kuchakata mazao vitakavyoanzishwa ikiwa ni sehemu ya mradi.

Bali pia, mradi utawanufaisha wakazi wa Matui na sehemu nyingine kwa kupata fursa ya kujifunza mbinu bora za kilimo cha kisasa ili kulima kwa tija.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, mradi umelenga kuwawezesha wakulima kupata mikopo isiyo na riba kwa ajili ya kilimo ili waweze kulima na kuondokana na mawazo ya ukosefu wa mitaji ya kilimo.

"Uongozi wa Wilaya ya Kiteto utatoa ushirikiano wote unaohitajika kwenye mradi huo ili kusaidia kufikia malengo ya mradi ipasavyo," anasema.

**SOKO LA MAZAO**

Kwa mujibu wa Meneja Masoko wa Jatu PLC, Mary Chulle, mradi huo umetengeneza mazingira mazuri ya kuwawezesha wakulima kupata soko la uhakika la mazao yanayozalishwa, kupitia utaratibu

**Inaendelea Uk. 19**

HAKI, UWAJIBIKAJI NA VITA YA RUSHWA

## HUYO NDIYE KIJANA, MWENENDO WAKE



Vijana wakiwa katika matukio yanayowahusu. **PICHA: MTANDAO.**

NENO kijana limekuwa na maana pana na linapata tafsiri mbalimbali kutoka katika kila jamii na Taifa. Kwa kuzingatia mifumo na maisha ya jamii, imezaa tafsiri kadhaa.

Inaweza kuchukua dhana ya kisheria, kiafya, kijamii na hata kiimani. Kuna jamiii na mataifa wanayotafsiri kuwa umri kati ya miaka 15 hadi 24, kwa mujibu wa mtazamo wa Umoja wa Mataifa.

Nchini Tanzania inatawala umri kati ya miaka 18 hadi 35, ikibeba mtazamo umri baada ya balehe na mabadiliko ya maumbile toka utoto kuelekea ukubwa.

Ikirejewa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, anaangaliwa katika umri kuanzia miaka15-24.

Hata hivyo, ujumla wake unabebwa zaidi na mtazamo kwa mwenye umri wa miaka 18-35, ambaye kwa mujibu wa mifumo ya kijamii au kitamaduni, kisiasa na kisheria ana uwezo wa kujitegemea na kufanya uamuzi binafsi.

Mambo muhimu ya kuangalia katika kutia tafsiri na maana ya kijana ina maeneo kadhaa. Mosi ni katika suala la utambuzi, kwamba kijana ni lazima awe na utambuzi binafsi, wa jamii yake na mazingira yanayomzunguka.

Kujitambua, ndiko kunamwezesha kufanya mambo sahihi na kwenda sawa na maadili ya jamii na Taifa.

Pili ni ukomavu wa akili. Katika umri wa miaka 18, vijana wengi wanakuwa na akili ya kufanya mambo yanayoendana na umri, kijana pia ataweza kuwa mshauri kwa wenzake, familia na jamii yake. Hapo anakuwa anamudu kupanga malengo yake na kuyafuatilia.

Uelewa Tatu, anapaswa kutambua changamoto alizo nazi na namna ya kuzikabili, kama vile tatizo la ajira na kifamilia na nne ni uwezo wa kujenga hoja zenye mashiko, ikiendana na suala la tano, kuwa na ushawishi.

Kijana ni lazima awe na ushawishi kuhusu jambo fulani na ndipo nguvu yake iweze kuleta msukumo.

Pia kuna mambo anayopaswa kufahamu, yanayojumuisha; kujitambua na kujikubali kwa maana ya kupokea mambo yote yanayomhusu, hali inayomsaidia kusonga mbele zaidi.

Lingine, ni kuwa na wajibu, shauku na kiu kuhusu mambo mbalimbali, awe mzalendo anayejiuliza sana na kujua nafasi ya uwapo wake.

Miasha ya ujana yanaambatana na tabia ya kadhaa:

Mwenye nguvu na amechangamka.

Kutokomaa kifikra vya kutosha.

Kuwa na nguvu nyingi kimwili na kiakili.

Kuwa na majukumu machache na uhuru mwingi.

Kuwa na muda wa kutosha kufanya mengi.

Ana shauku ya kufanya mazuri katika maisha.

Mara zote ana muda wa kushirikiana na vijana wengine katika maendeleo.

Ili kutimiza hayo anahitaji yafuatayo: Nidhamu, heshima, kuwajibika, kuwa na msingi wa maisha, kuchagua marafiki sahihi na kujenga uhusiano mzuri.

**KWA MUJIBU TOVUTI**

ELIMU

# Wakulima, wafugaji walivyonyweshwa dawa iliyokomesha migogoro ya ardhi



Baadhi ya wanawake wa Kijiji cha Nkongo wilayani Ulanga, wakishiriki kikao cha kujali masuala ya umiliki ardhi hususani, unaojali haki za mwanamke. **PICHA MASHAKA MUGETA.**

**Na Mashaka Mgeta, MOROGORO**

MIAKA ya 2000 Taifa lilishuhudia taathira ya migogoro baina ya wafugaji na wakulima ambayo ni kupoteza maisha ya watu na mifugo, uharibifu wa mali hasa mazao, makazi, vifaa kama matrekta na kuharibu mazingira.

Migogoro ilitikisa Morogoro, Pwani, Iringa na Mbeya. Mifugo ililishwa mazao kwingineko wanyama walikatwakatwa na kwa ujumla kuvurugana makundi haya kulichafua vyanzo vya maji, kuharibu misitu na porini, lakini wanyama waliingia hadi ndani ya hifadhi za wanyama pori.

Matatizo ya ardhi na changamoto zake ziliwaamsha wadau pamoja na serikali na kuanzia mwaka 2016, serikali ilianza utekelezaji wa mradi wa Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (LTSP) kwa wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi za mkoani Morogoro.

Mradi huo wa miaka mitatu uliosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ulifikia ukomo wake Septemba mwaka huu, lakini shughuli za mtandao wa mashirika ya utetezi wa rasilimali ardhi (Tala) ziliendelea zikitarajiwa kuhitimishwa mwishoni mwa mwezi huu.

Wizara hiyo kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya hizo, walishughulikia mpango wa matumizi bora ya ardhi, upimaji na utoaji wa hati miliki za kimila, wakati washirika wa Tala wakihamasisha na kuielimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za ardhi.

Wahisani mbalimbali wakiwamo, mashirika ya DFID la Uingereza, Sida la Sweden na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Dermark la Danida yalifadhili mradi huo.

Hivi karibuni Mwandishi wa makala haya alishiriki ufuatiliaji na tathmini ya mradi huo na kutembelea vijiji 11 vilivyonufaika ambavyo ni pamoja na Misegese, Sofi Majiji, Mtimbira vya wilayni Malinyi, Nkongo, Mwaya, Isiyaga, Libenanga na Chirombola vilivyoko Ulanga, Siginali, Kisegese na Nyamwezi vya Kilombero.

Wakati wa ziara ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea wilaya hizo Januari mwaka huu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ilionyesha mipaka ya vijiji 127 iliyopimwa na vipande 263,028 vilihakikiwa kwa ajili ya kupimwa.

**KUPUNGUA MIGOGORO**

Kupungua kwa migogoro ya ardhi kunashuhudiwa mara kwa mara na wakazi wa vijiji hivyo, kuwa ni moja ya mafaniko makubwa ya utekelezaji wa mradi huo.

Zipo kadhia mbalimbali zinazohusishwa na migogoro ya ardhi iliyokuwapo awali na hivyo kusababisha mafarakano, machafuko na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Lakini hali hiyo imepungua au kutoweka kwenye maeneo kadhaa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Misegese wilayani Malinyi, Novatus Mvogo, ni miongoni mwa wanaoishuhudia hali hiyo, akitoa mfano kuwa kabla ya LTSP, ofisi yake ilikuwa ikipokea taarifa za migogoro angalau 15 kwa siku, kisha kuiwasilisha kwenye baraza la usuluhishi wa migogoro ya ardhi kijijini humo.

Anasema hivi sasa, idadi ya migogoro hiyo iliyohusu zaidi mipaka ya mashamba na viwanja vya makazi, imepungua kufikia kati ya miwili na mitatu kwa siku.

"Awali, ilipotokea mtu kuingia na kulima kwenye eneo lisilokuwa lake au ambalo hawajakubaliana na jirani yake kuhusu mpaka halisi, ilikuwa chanzo cha ugomvi uliosababisha kutishana kwa mapanga," anasema.

Kupungua migogoro kumetoa fursa kwa uongozi kushughulikia masuala ya maendeleo na ustawi wa wananchi.

Beata Adam ni kiongozi wa Kituo cha Wasaidizi wa Sheria wilayani Malinyi, anatoa mfano kuwa Januari hadi Machi mwaka huu, walipokea migogoro 17 iliyohusiana na ardhi, 11 ikitoka kwa wanaume na sita kwa wanawake.

Takwimu hizo zinaonyesha kuongezeka katika robo ya pili ya Aprili hadi Juni, mwaka huu kufikia 84, ambapo migogoro 44 iliwasilishwa na wanawake na 40 wanaume.

Hata hivyo ilipungua kati ya Julai na Septemba na kufikia 54 na kwamba ya wanaume ilikuwa 20 na wanawake 34.

Beata anasema hayo ni matokeo ya uelewa mpana wa masuala ya ardhi baada ya uelimishaji uliofanywa na Tala kwenye utekelezaji wa mradi wa LTSP. Migogoro mingi ya wanawake ilihusu kudhulumiwa umiliki ardhi kutoka kwa wanaume wa waliowataliki, ndugu wa wanaume waliofariki ama familia, wakati ya wanaume ilihusu mipaka ama eneo moja kumilikiwa na watu zaidi ya mmoja.

Yasmine Nyoni mkazi wa kijiji cha Mwaya wilayani Ulanga, anasema kabla ya mradi alikuwa na mgogoro na jirani uliosababisha kutishiana maisha.

"Baada ya elimu kutolewa, alinifuata na kunitaka tusahau tofauti zetu na kukubaliana pa kuweka mpaka ili tupimiwe ardhi na kupata hati miliki za kimila," anasema na kuongeza kuwa sasa yamekwisha.

Raimunda Fussi, mkazi wa kijiji cha Isiyaga wilayani Ulanga, anasema kabla ya mradi huo, mashauri yaliyohusu migogoro kijijini hapo yalikuwa kati ya 10 na 15 kwa siku, lakini sasa ni wastani wa miwili.

Kushamiri kwa migogoro hapo awali, kulisababisha kukosekana amani kati ya majirani, kushindwa kulima, ugomvi na kutishiana mapanga na silaha za jadi.

**UTATUZI**

"Tumeshuhudia kupatikana kwa suluhu kwenye maeneo yaliyokuwa na migogoro ya mipaka kati ya wafugaji na wakulima, sasa kila upande unaomba ridhaa ya kutumia eneo jingine badala ya kuvamia kama ilivyokuwa awali," anasema mkazi wa kijiji cha Nyamwezi, Boni Nangireki.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chirombola wilayani Ulanga, Novatus Ntyangiri, anasema awali, mashauri ya migogoro yalikuwa kati ya 10 hadi 20 kwa siku, lakini baada ya mradi yanapokelewa matatu hadi matano, mengi yakihusisha wanandugu kumiliki ardhi ya familia.

Hoja ya migogoro kuwahusu wanandugu inaungwa mkono na wakazi wa kijiji hicho, Klotida Mkongeni na Hotuba Mparangondo na Rashid Omar wa Kijiji cha Siginali.Wanataja mgogoro wa familia wa Kilombero uliosababisha kupigana, kujeruhiana na mmoja kuvunjwa mkono wakigombea ardhi, lakini ulisuluhishwa na amani kurejea, anasema Mtendaji wa Kijiji cha Chirombola, Elpidius Ndumba.

Jamal Juma, Ofisa Programu wa Tala, anasema ardhi ni rasilimali inayotegemewa na kila mmoja hivyo ina umuhimu wa pekee unaosababisha mafarakano ya umiliki.

**UELEWA**

Mwenyekiti wa Baraza la Usuluhishi wa Migogoro wa Kijiji cha Misegese, Peter Myolele, anasema mafunzo yamekuza uelewa na baadhi yao wanatafuta suluhu kabla ya kufikia mabaraza ya usuluhishi.

Msaidizi wa sheria wilayani Malinyi, Martha Nandika, anasema utoaji elimu na uhamasishaji umechangia kupungua migogoro ya ardhi.

Hoja hiyo inaungwa mkono na Mkurugenzi wa Kituo cha Wasaidizi wa Sheria wilayani Ulanga, Rashid Kiding'a, anaposema sehemu kubwa ya migogoro hiyo inahusu wanawake kudhulumiwa na ndugu katika mirathi, mipaka na umiliki wa mtu zaidi ya mmoja.

**MIGOGORO YA MIPAKA**

Mipaka ya ardhi kati ya watu binafsi, vijiji na vitongoji imetajwa mara nyingi kuwa sababu ya migogoro ya ardhi kabla ya LTSP.

Samora Makwaya mfugaji wa kijiji cha Misegese, anasema lipo eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, lakini 'limevamiwa' na wagufaji kutoka mikoa mingine wanaojishughulisha na ukulima, hivyo kulifanya lisitosheleze mahitaji.

Anasema, wafugaji hao wanapowasili kijijini hapo, wanajisajili pasipo kuelezea hali yao ya ufugaji, lakini baada ya kupata ardhi wananunua ama kuingiza mifugo kwa wingi kutoka kwenye maeneo yao ya asili.

Kwa mujibu wa Makwaya, mfumo wa kilimo kinachofanywa na wafugaji na wakulima kinachukua eneo kubwa la malisho kwa vile hawafanyi makadirio ya ukomo wa maeneo wanayoyatumia kwa uzalishaji mazao.

Mfugaji wa kijiji cha Biro katika Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Oki Bulegi anasema ukosefu wa alama la kudumu za mipaka unachangia kuibuka kwa migogoro ya ardhi kijijini humo.

"Alama zinazotumika kwa kupaka rangi kwenye miti ya mpakani ama kuweka mawe madogo hazifai kwa vile miti ile inakatwa na mawe kuondolewa," anasema. Mkulima wa Kijiji cha Biro, Seleman Myumbaniki, anasema wafugaji wamekuwa na kasumba ya kukaidi mpango wa matumizi bora ya ardhi uliotenga eneo la malisho kuwa takribani 57 kutoka katikati ya kijiji hicho.

Eneo hilo ndilo linaloelezwa kukaliwa na wafugaji wengi wanaojishughulisha pia na ukulima wa mpunga.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Omar Seif, anasema jamii za wafugaji wanaalikana kuingia kwenye eneo hilo kupitia 'njia za panya'.

"Kuna taarifa zisizotiliwa shaka kuwapo kundi kubwa la wafugaji, wanaposhuka kwenye mabasi wanasikika wakipiga simu kuwaulizia jamaa zao wawaelekeze...hilo limechangia ongezeko la watu na mifugo kwenye eneo lililotengwa kwa malisho," anasema.

Kwa mujibu wa Seif, hali hiyo inadhibitiwa kwa kufuatilia wanaoingia na kuishi na kuweka sheria ndogo za vijiji.

***0754691540***

# Kiteto bila mito waanza umwagiliaji

Inatoka Uk. 17

wa kampuni kununua mazao hayo na kuyapeleka katika viwanda vya mradi na kuchakata na baada ya hapo huuzwa kwa wanachama na kupatiwa gawio la faida.

Lakini kampuni imewaunganisha wanachama wake na masoko kwa njia ya mitandao inayorahisisha biashara kwa kuwa wateja wanaweza kutoa oda ya bidhaa popote pale walipo kwa kutumia simu ya kiganjani na kampuni ikawafikishia mpaka walipo.

Kampuni pia inatoa fursa ya biashara kwa wanachama wake kwa kuwapa uwakala kwa waliokidhi vigezo, mawakala hao hufanya kazi ya kutoa elimu na kuuza bidhaa kwa wateja waliopo maeneo yao na kupata hadi asilimia 10 ya faida kwa kila bidhaa wanayoiuza.

"Mbali na hilo la kufanya mauzo katika mitandao, mkulima atakuwa na nafasi ya kupata taarifa haraka kuhusu bidhaa zetu na vitu vinavyoendelea ndani ya kampuni yetu," anasema.

Anawashauri watu mbalimbali kujitokeza na kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa kwa kuwa kinasaidia kuongeza kipato cha mwananchi mbali na shughuli nyingine za kila siku.

Lakini uwekezaji wa kwenye kilimo cha umwagiliaji unatoa fursa kwa mkulima kukuza mtaji wake na kuzalisha mazao bora kwa tija yanayoweza kuuza kwenye soko la nje.

Chulle anaongeza kuwa soko la biashara ni njia ya kisasa ambayo inamuunganisha mteja moja kwa moja na soko kutoka shambani au kiwandani hadi kumfikia mteja.

# Inakuwaje 'meno ya tembo' wakati ni pembe za ndovu?

**Na Michael Eneza**

MOJA ya matatizo ya kimantiki ya usahihi wa Kiswahili au usanifu wake vile vile, au usawiri kama kuna suala la kuunda maneno ni kutokujengeka dhana ya matumizi tofauti na badala yake inakuwa kila mara matumizi sahihi.

Mara nyingi zaidi matumizi sahihi ni yale ambayo kwa uzoefu wa namna moja au nyingine yanakubalika kwa wataalamu wa Kiswahili, hali ambayo inaleta utata wa kitaaluma kama kuna utaalamu wa lugha au mwelekeo fulani wa lugha unaotawala katika nyakati tofauti.

Ni kawaida ya uchambuzi wa kisayansi kutofautisha hisia na ufahamu. Mojawapo ya vyanzo vya mabadiliko ya matumizi ya maneno au hisia za usemi sahihi au 'sanifu' katika Kiswahili ni muda, kuwa matumizi ya maneno yanabadilika kutoka wakati mmoja kwenda kipindi kingine, hali inayoleta tatizo la ziada la kupambanua kati ya ufahamu wa lugha kuongezeka au hisia kubadilika katika kipindi hicho.

Dhana ya kusanifu maneno kwa maana ya kuyakubali kwa mpangilio wa kitafiti kwa upande mmoja na utawala kwa upande mwingine haikidhi mahitaji ya kupambanua tofauti hizo.

Inapendelea kudakia upande mmoja na kuunga mkono mwelekeo wake katika matumizi ya lugha, na siyo usahihi halisi wa kitaaluma, vielelezo.

Ndiyo maana haijasikika hata siku moja wataalamu wa lugha katika Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kukumbusha kuwa 'nyara za serikali' zinazozungumziwa kila uchao siyo 'meno ya tembo' kama watu waliyozoea kueleza, ila ni pembe za ndovu.

Katika miaka takriban 10 baada ya uhuru dhana hiyo ya pembe za ndovu ndiyo ilikuwa inatumika, hata mnyama mkubwa katika kielelezo cha kinywaji chenye jina hilo anaitwa 'ndovu,' tembo ikawa maarufu zaidi baadaye. Ila hakuna tatizo kuhusu matumizi ya ndovu au tembo, nje ya kuzungumzia pembe kuwa ni 'meno.'

Ingekuwa kuna kutafuta mambo kwenye mtandao 'Google Search,' upembuzi wa kidijitali wa linakotoka neno hili au matumizi haya au yale, ingekuwa rahisi kujua labda ni nani alianza kutumia dhana hiyo potofu, na ikaanza kukubalika kwa sababu gani.

Inawezekana ni waziri akitoa hotuba kwa mfano ya bajeti bungeni, au mtu mwingine mwenye nafasi kijamii, ambaye bila shaka alikosea lakini kwa sababu moja au nyingine matumizi hayo yakaanza kusambaa. Hapo pia ingesaidia kujua, kifaa cha aina hiyo kingekuwapo, kama usemi huo ulisambaa kwa mzaha wa aina fulani au kama matumizi sahihi.



Tembo. **PICHA: MTANDAO**

Kinachoonekana ni kuwa miaka ilivyozidi kupita matumizi hayo yakawa yamezoeleka kiasi ambacho hakuna mtumiaji mwenye nafasi katika majukwaa au vyombo vya habari anayeanza kwa kuhoji matumizi hayo. Ni kama vile kuna mazingaombwe au mchezo wa kuigia ambako polisi anakamata mtu na pembe za ndovu, anaingiza kesi mahakamani kuwa amemkuta na meno ya tembo halafu mtuhumiwa anaachiwa huru, kwani shtaka lilikosewa. Katika mchezo huo wa kuigiza angekutwa na pembe za ndovu angekuwa na hatia kwani zina thamani katika masoko.

> Katika miaka takriban 10 baada ya uhuru dhana hiyo ya pembe za ndovu ndiyo ilikuwa inatumika, hata mnyama mkubwa katika kielelezo cha kinywaji...

Hata hivyo Waingereza wana usemi kuwa hali halisi au ukweli ni wa kustaajabisha zaidi kuliko hadithi au riwaya, hivyo ikiwezekana kugundua ni vipi pembe za ndovu zilibadilishwa na kuwa meno ya tembo, huenda uhalisia wa kilichotokea ukawa unashangaza au kufadhaisha zaidi kuliko riwaya tunaweza kubuni sasa.

Lakini bado ni jambo la kustaajabisha kuwa taifa zima lilidaka mzaha kuwa meno ya tembo yana urefu wa takriban mita moja, huku aliyeanzisha mzaha huo si ajabu alikuwa anacheka na kuumia mbavu akiona mzaha umekuwa 'sanifu.'

Na imebaki hivyo hadi leo kwani hisia za udadisi si kali katika Bakita za zaidi ni ujumuiya wa matumizi ya maneno ya Kiswahili, jinsi wamavyojisikia wakiyatumia, na wakiridhika wote inakuwa 'sanifu.'

Hoja hii haimaanishi kuwa watu waache kutumia dhana ya meno ya tembo endapo wanajisikia raha kusema hivyo ila kuinua udadisi wa jambo hilo kwa kiwango fulani. Udadisi huu unafaa kwa sababu hakuna suala hapa la matumizi tu ya maneno bali usahihi wa kinachotajwa, kama ni meno au ni pembe, kwa sababu hakuna ubishi kuwa hakuna hata mtu mmoja amewahi kutiwa pingu kwa kuwa na meno ya tembo ila pembe zake. Siyo rahisi kuona kwanini watu wanaongea kama vipofu wasioona wanachozungumzia, ni kama waliambiwa tu ni kitu gani hiyo wanarudia.

Wakati suala la kutumia dhana ya meno ya tembo badala ya pembe za ndovu ni la kila mtu kivyake au katika vyombo vya habari, waweke 'sera' kuwa sisi tunataka uandike au useme ni meno ya tembo au pembe za ndovu, bado tatizo la msingi linabakia.

Ni hili linalogusa usanifu kama taaluma, kuwa inatakiwa kuainisha matumizi tofauti ya maneno na siyo kujipatia kazi ya kuratibu matumizi, kwani watu wanatumia maneno kwa hisia inayotokana mara nyingi zaidi na kudakiza, kwa mfano 'kusepa' (kutokana na kuondoka kwa Kifaransa), linalotumiwa na wageni wanaopiga muziki,'se part' ambako 'part' inatamkwa kama paaaa kwa msisitizo, ndiyo ku-sepa.

Hivyo angalau tuanzie hapo kuwa maneno ni matokeo ya matumizi na siyo kusanifiwa au kuwe na vikao vya kuyakubali kwani vikao vya matumizi ya lugha ni vijiwe vya wasomi, kuwa havina tofauti ya kina na wazungumzaji wa kawaida.

Ndiyo maana baadhi ya wapenda usanifu tayari wanahoji neno 'kuji-mwamba-fai' ambalo ni mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza, kwa kuweka chumvi tu ya 'kujifanya mwamba' ambako wako baadhi wangeudhika hivyo aliyetoa hisia hiyo anaikarabati ili iwe na ladha, isiudhi. Ni kama neno la kawaida la kuleta kitu fulani 'fasta,' siyo kwa sababu mtumiaji hajui neno 'haraka' bali anakwepa kuwa na ukali na kulazimisha au kushurutisha badala yake anatumia 'fasta.' Njoo 'fasta' badala ya uje haraka.



# WADAU SABATO KASIKA

**Katika kongamano la ushiriki wa vijana kwenye uongozi na mapinduzi ya nne ya viwanda, lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), washiriki wanapendekeza wanafunzi waruhusiwe kuwa na simu janja shuleni, ili teknolojia isiwaache nyuma. Wadau wanasemaje?**



**GRACE MGUMBA (MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

MATAIFA yaliyoendelea yamepiga hatua zaidi kwenye suala la teknolojia kwa kuruhusu raia wake wakiwamo watoto kutumia simu, ili wajifunze wangali wadogo na hadi wakiwa wakubwa wawe na uelewa wa kutosha na kuwa na mchango katika maendeleo ya teknolojia nchini mwao. Lakini hapa kwetu bado haiwezekani mwanafunzi kwenda na simu shuleni, kwa sababu sheria haziruhusu. Kwa mtazamo wangu ni kwamba umefika wakati sasa kuangalia upya suala hili, kama kweli hatutaki kuachwa nyuma na teknolojia. Tunaweza kuwa na mjadala mpana kwa kuhusisha wadau wote wa elimu ili kuangalia uwezekano wa kuruhusu wanafunzi kuwa na simu, lakini ni lazima wazitumie katika matumizi sahihi badala ya mambo mengine ambayo hayaendani na malengo, kwani lengo kuu ni kutaka wanafunzi wajifunze teknolojia kupitia simu na kompyuta wangali wadogo, ili baadaye waitumie kwa maendeleo ya nchi yao. Lakini vilevile ni vyema kujadili suala la ukombozi kwa mtoto wa kike, hili ninaweza kusema kuwa ukombozi wake unategemea yeye mwenyewe kutambua kuwa anaweza. Lazima mtazamo hasi juu yake aanze kuuondoa kwake yeye mwenyewe na hatimaye jamii itamtambua.



**MWAJUMA IDRISA (MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

TATIZO lililopo kwa vijana na wanafunzi kwa ujumla, ni kutumia simu zao za kisasa, katika mitandao ya kijamii na kupongezana kwa uzembe na mambo mengine ya ovyo, ambayo hayafai. Sasa katika mazingira kama hayo bado ni tatizo kuwafikia wenzetu, ambao wanaruhusu watoto wao kutumia simu na kompyuta, kwa sababu wao wanazitumia kwa malengo maalum yanayohusu maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa maana hiyo kama na sisi tunataka kufikia hapo, ni lazima tubadilike, kwani wapo baadhi ya vijana, ambao wamejikuta katika matatizo makubwa hadi kufikia kupoteza maisha, kwa matumizi mabaya ya simu hasa ambayo yanahusu masuala la mahusiano. Simu hizi zimefikia kuwaingiza vijana kwenye mahusiano ya kingono na mwisho wake wanapoteza maisha kwa kuambukizwa Ukimwi.

Wakati huu siyo tena wa kutumia simu kwenye mitandao ya kijamii kupongezana kwa uzembe, bali tuchukue hatua za kutuwezesha kufikia kwenye soko la ushindaji katika ajira, kwa kuandaa vijana wajue matumizi sahihi ya teknolojia. Tusiwe watu wa kupokea kila kitu na kukitumia kinyume na malengo yaliyokusudiwa.



**BARAKA LAMECK (MWANAFUNZI CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE)**


SUALA la teknolojia lina upana wake na hasa kwenye ajira za dunia ya leo ambayo ni wa sayansi na teknolojia. Maana yake ni kwamba ni lazima nasi tusibaki nyuma bali tuifuate dunia inavyokwenda, vinginevyo tutakuwa wa mwisho. Lakini pia ni lazima tutambue madhara ya simu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Hawa wote kimsingi bado ni wadogo, wanatakiwa kufundishwa ili wajue madhara ya matumizi mabaya ya teknolojia ndipo kama inawezekana, basi waruhusiwe kuzitumia. Hatua hizo zikichukuliwa, nina uhakika hatutakuwa nyuma, katika ushiriki wa vijana kwenye uongozi na mapinduzi ya nne ya viwanda.

Nishukuru TGNP kwa kuleta kongamano hili kwa wakati ili vijana tupeane uzoefu kwenye suala la teknolojia, ambalo kimsingi limekuwa na changamoto nyingi kutokana na jinsi linavyopokelewa. Tunapozungumzia Tanzania ya viwanda maana yake tunazungumzia teknolojia kuanzia kwenye simu ambazo kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikitumika hata kwenye unyanyasaji wa kijinsia. Ninaamini wengi wetu tumewahi kusikia baadhi ya wanawake na wasichana wamekufa au kuumizwa kupitia simu hizi kwenye mambo ya mapenzi. Ushauri wangu ni kwamba tuwe makini na matumizi ya simu yasitutoe kwenye mwelekeo, tuwe na mkakati wa kuelimisha umma wa Watanzania wakiwamo wanafunzi kuhusu matumizi sahihi ya simu hizi za mkononi.



**ALPHONSINA AMBROSE (MHITIMU CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)**

KUNA haja ya kujiuliza ni kwa jinsi gani watoto wanapewa elimu shuleni kuhusiana na matumizi ya sayansi na teknolojia, hasa maeneo ya vijijini? Elimu hii ni muhimu sana, ili kusaidia watoto kujua matumizi sahihi ya simu na hatimaye kuwa na mchango mkubwa kwenye suala zima la maendeleo ya teknolojia nchini. Ni kweli kwamba tunapozungumzia suala la maendeleo ya teknolojia, ni muhimu sana kuwagusa watoto hasa shule za msingi na sekondari, lakini bahati mbaya wale wanaosoma shule za vijijini, siyo wote ambao shule zao zina umeme, kwa hiyo wanaweza kuachwa nyuma katika matumizi ya teknolojia. Kwani hawawezi kutumia kompyuta hata kama zipo shuleni, kwa sababu ya ukosefu wa nishati ya umeme. Lakini pia kuna suala la matumizi yasiyo sahihi ya taknolojia, ambayo hufanywa na baadhi ya wanafunzi. Ni kweli taratibu na sheria haviruhusu mwanafunzi kuwa na simu shuleni, lakini bado ipo haja kuwaelimisha wale walio nazo ili wajue umuhimu wa matumizi sahihi ya simu hizo. Lengo ni kuwafanya wasichwe nyuma bali wajifunze kitu kutoka katika simu ambacho kitakuwa na manufaa kwao na hata kwenye jamii kwa ujumla. Hapa ninamaanisha kujifunza matumizi sahihi ya teknolojia ambayo yanaweza kuwafanya wakaingia kwenye soko la ajira.



**GODFREY THOMAS (MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

MAPINDUZI ya nne ya viwanda yanawahusu vijana moja kwa moja. Je, wanatambua umuhimu wa uhusika wao na faida zake kwa maendeleo endelevu ya jamii zao? Vijana tuna mchango mkubwa sana katika utatuzi wa hizi changamoto zinazotuzunguka. Sababu ni moja, sisi ndiyo tunazijua vyema. Vijana wa Tanzania tusidhani kwamba bado tuna miaka mingi zaidi ya kujifunza matumizi ya sahihi ya simu za mkononi, dunia inakwenda haraka kwenye taknolojia, hivyo nasi tuwe tayari kwenda na wakati na kujifunza matumizi sahihi ya taknolojia ili iweze kutusaidia kufikia maendeleo endelevu. Tusikubali kupotea kwa kutumia vibaya simu au intaneti. Ninatambua kuwapo kwa taarifa za matumizi mabaya ya teknolojia na hasa kwa wanafunzi ambao baadhi ya hukamatwa na simu na hata kusimamishwa au kufukuzwa shule. Kwa sisi vijana ambao tumetoka huko, ni wakati wa kujitafakari na kutambua kuwa mapinfuzi nne ya viwanda yanatuhusu vijana moja kwa moja, hivyo tujifunze matumizi sahihi, ili tuweze kutumiwa au kupata ajira zinazoendana na taaluma tulizonazo kupitia teknolojia. Nirudi kusema kuwa vijana tuna mchango mkubwa sana katika utatuzi wa hizi changamoto zinazotuzunguka kwani tunazijua, hasa kwenye suala zima la matumizi ya teknolojia.



# Wazee wasiojiweza 9,883 watambuliwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAZEE 9,883 wasiojiweza wametambuliwa katika Wilaya ya Chunya na baadhi yao kukabidhiwa vitambulisho kwa ajili ya kutibiwa bure katika hospitali na vituo vya afya vya serikali, ukiwa ni utekelezaji wa sera ya wazee nchini.

Hayo yalisemwa na Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Theresia Mwendapole, alipokuwa anazungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii zikiwamo shughuli za kisera.

Alisema kati ya wazee hao waliopewa vitambulisho vya kutibiwa bure ni zaidi ya asilimia 100 na wanaendelea kupata matibabu katika vituo vya afya na hospitali za serikali bila malipo.

Kwa mujibu wa Mwendapole, mbali na kuwatambua wazee hao na kuwakabidhi vitambulisho hivyo, pia wameendelea kusisitiza hospitali zote za serikali, vituo vya afya na zahanati kuwa na dirisha maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wazee.

"Tunachokifanya ni utekelezaji wa sera za nchi, sasa tumeagiza kuwapo na madirisha ya kuwahudumia wazee ili wahudumiwe kwa wakati na bila malipo yoyote," alisema Mwendapole.

Alisisitiza wazee ni kundi muhimu katika taifa kwa maelezo kuwa walishafanya maendeleo makubwa katika taifa kabla ya kufikia umri wa kutojiweza.

**Kati ya wazee hao waliopewa vitambulisho vya kutibiwa bure ni zaidi ya asilimia 100 na wanaendelea kupata matibabu katika vituo vya afya na hospitali za serikali bila malipo.**

# Bil. 1.5/- kukamilisha ujenzi wa hospitali tatu wilaya

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali tatu za wilaya katika Mkoa wa Mbeya, ambazo ujenzi wake umebakia kidogo kukamilika ili zifunguliwe na wananchi waanze kupata huduma kuanzia Januari mwakani.

Hospitali zilizotengewa fedha hizo ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mbarali na Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe ambazo awali serikali ilitoa Sh. bilioni 1.5 kwa kila moja kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbarali.

Alisema serikali inaridhishwa na maendeleo ya miradi ya hospitali hizo pamoja na matumizi ya fedha za awali, hivyo Rais John Magufuli ameamua kutoa fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha kuboresha huduma za afya.

**Nimeridhishwa sana na ujenzi wa hospitali hii pamoja na zile za Mbeya Dc na Busokelo kule Rungwe, lakini huko juu inaonyesha mliezeka kwa ule mfumo wa zamani, fanyeni utaratibu wa kutafuta rangi moja muweke ili iwe na mwonekano wa aina moja.**

"Nimeridhishwa sana na ujenzi wa hospitali hii pamoja na zile za Mbeya Dc na Busokelo kule Rungwe, lakini huko juu inaonyesha mliezeka kwa ule mfumo wa zamani, fanyeni utaratibu wa kutafuta rangi moja muweke ili iwe na mwonekano wa aina moja," alisema Jafo.

Alisema ujenzi wa hospitali hizo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 kwa maelezo kuwa chama hicho kiliahidi kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliongozana na Waziri Jafo kukagua mradi huo, aliahidi kuhakikisha fedha za vituo hivyo zinatumika vizuri na miradi yote inakamilika kwa wakati.

Alimshukuru Jafo kwa kufuatilia mara kwa mara miradi hiyo kwa ajili ya kujiridhisha kwa maelezo kuwa usimamizi wa aina hiyo unasaidia miradi kukamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa.

Aidha, alisema mbali na hospitali hizo za wilaya ambazo serikali imetoa fedha nyingi, pia vipo vituo vya afya ambavyo pia fedha nyingi zimetukika katika kuvijenga, na kwamba yeye kama msimamizi mkuu wa shughuli za serikali katika mkoa huo, atahakikisha hakuna ubadhirifu unaotokea.

"Katika Mkoa huu tumepewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizi tatu, lakini tuna vituo vya afya 14 ambavyo vinajengwa katika maeneo mbalimbali na vingi vina hadhi ya hospitali," alisema Chalamila.

Vilevile, alisema wananchi wanaendelea na ujenzi wa zahanati kwenye vijiji vyao, na kwamba serikali itaendelea kuwahamasisha wajenge mpaka kufikia usawa wa kuezeka ili serikali imalizie.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Francis Mtega, alimshukuru Rais Magufuli kwa kutekeleza ahadi aliyoahidi alipofanya ziara wilayani humo ya kukamilisha ujenzi wa hospitali.

Alisema yeye kwa kushirikiana na watendaji wa halmashauri, watahakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati na bila kuwa na dosari za aina yoyote.



Mmoja wa wajasiriamali wa Jiji la Mbeya akimshawishi mteja kununua mti wa Krismasi ambao alikuwa anauuza katika eneo la Posta katikati ya Jiji hilo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 20,000 wapya kusajiliwa mfumo wa vifurushi NHIF

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) katika Mkoa wa Mbeya, unakusudia kusajili wanachama wapya 22,000 kupitia mfumo wa vifurushi vya Bima ya Afya katika awamu ya kwanza.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa NHIF Mkoa wa Mbeya, Mbala Shitindi, wakati wa mkutano wa viongozi wa mfuko huo na wanahabari wa Mkoa wa Mbeya uliokuwa na lengo la kutoa elimu kuhusu vifurushi hivyo.

Alisema makundi yatakayohusika ni watu wazima, watoto na wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu huku akisisitiza kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali juu ya umuhimu wa kujiunga na mfuko huo.

Shitindi alisema watahakikisha wananchi wote wa mkoa huo wanahamasika kwa maelezo kuwa wanatarajia kutoa elimu hiyo mpaka maeneo ya vijijini na kwa kuyafikia makundi yote.

"Mpaka sasa tumeshawafikia wakulima wote 6,000 wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya, tunatarajia pia kuwaandikisha wanafunzi zaidi ya 11 na watoto 500 katika awamu ya kwanza, tunaendelea kuyafikia makundi mengine," alisema Shitindi.

Alisisitiza kuwa watavifikia vikundi vyote vya wakulima wa mazao ya kimkakati wakiwamo wakulima wa kahawa katika Wilaya ya Rungwe, kakao, chai na mazao mengine pamoja na vikundi vya waendesha pikipiki maarufu 'bodaboda'.

Hata hivyo, alisema ofisi yake itaendelea kushirikiana na wadau wakiwamo wanahabari katika kuhamasisha wananchi kujiunga na vifurushi hivyo.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema mpaka sasa asilimia nane ya Watanzania wote wameshajiunga na mfuko huo kupitia mfumo wa vifurushi kuanzia Septemba na kwamba hiyo ni hatua kubwa.

Alisema kabla ya kutumia mfumo huo mfuko ulifanya utafiti na kujiridhisha kuwa una tija zaidi kuliko wa awali ambao baadhi ya makundi yasiyostahili yalikuwa yanajichomeka na kuongeza matatizo kwenye mfuko.

Alisema katika mfumo wa kikoa ambao wananchi kupitia vikundi walikuwa wanachangia Sh. 76,800 kuna baadhi ya watu walikuwa wanajichomeka wakiwamo matajiri na watu wasiokuwa na sifa, hivyo mfumo wa vifurushi unatatua matatizo hayo na mengine.

Alisisitiza ni muhimu kila mwananchi akawa na bima ya afya na kuhakikisha wanachangia ili kurahisisha huduma za matibabu wakati wanapougua kwa maelezo kuwa gharama za matibabu ni kubwa kuliko viwango vilivyowekwa.

"Michango ya vifurushi hivi haiendani kabisa na gharama za matibabu, kuna magonjwa kama moyo, kusafisha figo na matibabu ya saratani, ni gharama kubwa ambayo mwananchi akitibiwa kwa kutoa pesa mkononi anaweza akauza kila kitu," alisema Konga.

Hata hivyo, alisema viongozi wa mfuko huo, wanatamani kila Mtanzania ajiunge na mfuko huo na awe anachangia kama ilivyo kwa Rwanda ambayo ni lazima kila mwananchi achangie na kwamba kwa sasa wataendelea kuboresha mfumo wa vifurushi.

Baadhi ya wanahabari mkoani hapa waliomba mfumo huo usiingilie sera za nchi ikiwamo matibabu bure kwa wazee wasiojiweza pamoja na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano.



# Hofu chakula cha sumu yamwibua DC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobasi Katambi, amewapa angalizo wananchi kuwa makini na vyakula wanavyopika kuvikagua kama vimepita muda wa kutumika ili kuepusha jamii kupata maradhi ya mlipuko.

Katambi alitoa angalizo hilo wakati akizungumza na wananchi wa Mtaa wa Mtumba waliolazwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wanaosadikiwa kula chakula kinachosadikiwa kuwa na sumu.

Tukio hilo lilitokea katika msiba wa Edward Madumba (75), aliyefariki dunia kutokana na kusumbuliwa na homa kwa muda mrefu.

Katambi alisema ili kuepusha hatari hiyo, jamii inapaswa kuwa makini na vyakula wanavyopika ili kuisaidia jamii kuepuka sumukuvu inayotokana na vyakula vilivyokaa muda mrefu.

**Akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ameunda timu kwa ajili ya kwenda kuchunguza mabaki ya vyakula ambavyo watu hao walikula.**

Alisema akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ameunda timu kwa ajili ya kwenda kuchunguza mabaki ya vyakula ambavyo watu hao walikula.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Best Magoma, alisema wagonjwa waliopokelewa hospitalini hapo wanaendelea na matibabu wakati uchunguzi ukiendelea kubaini kilichosababisha watu hao kuanza kuharisha na kutapika baada ya kula chakula hicho.

Dk. Magoma alisema hatua za awali zilizofanyika ni wagonjwa hao kupata tiba ya huduma ya kwanza, huku taratibu za kupima unga uliotumika kupika chakula pamoja na maharage na chanise walizokula katika msiba.

Hata hivyo alisema wameunda timu ambayo imeenda kuchukua mabaki ya vyakula kwa ajili ya kupima ili kama ni sumu kuvu au ni ya kuwekwa na mtu.

"Tunashukuru hakuna kifo kilichotokea, na hivi sasa wote wanaendelea na dripu za maji na dawa walizowekewa," alisema Dk. Magoma.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Morroto, alisema mpaka sasa idadi ya wagonjwa imeongezeka na kufikia 45.

Alisema baada ya kutembelea wodini amebaini wagonjwa waliokutwa na dhahama hiyo ni 45, na kwamba idadi hiyo inaweza kuongezeka.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema anashukuru jitihada madaktari wa hospitali hiyo waliofanikiwa kuokoa maisha ya watu hao.

Kwa upande wa mtoto wa marehemu Lista Madumba alisema chakula walichokula ni ugali maharage na mboga ya chainizi.



Hakimu Mohamed anayejishughulisha na uuzaji wa viatu vya wanafunzi katika soko la Sabasaba akipanga tayari kuviuza kwenye msimu wa shule zitakapofunguliwa. **PICHA PETER MKWAVILA**.

# Uzalishaji mbegu zabibu waipaisha Tanzania

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

UZALISHAJI wa aina 86 za mbegu za zabibu uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI-Makutupora) Dodoma kwa ajili ya kusaidia malighafi zitakazotumika katika uchumi wa viwanda umeifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili wa zao la zabibu katika nchi za ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na gazeti hili, Mkurugenzi wa TARI Makutupora, Dk. Corlen Massawe, alisema mbegu hizo zenye ukidhani na wadudu zimefanyiwa majaribio katika maeneo tofauti ya mashamba ya wakulima na kuonyesha tija, huku baadhi ya maeneo wakulima wakianza uzalishaji kwa kutumia mbegu za kisasa.

Dk. Massawe alisema Mkoa wa Dodoma ndio umekuwa mzalishaji mkubwa wa zabibu, huku likilimwa kwa wingi Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Jiji la Dodoma, huku mikoa mingine nayo ikipatiwa mbegu hizo kwa ajili ya kuanza uzalishaji.

Alisema uzalishaji wa zabibu unakua kwa kasi kutoka tani 10,000 mwaka 2016 hadi 15,000 mwaka 2018, ambalo ni wastani wa ongezeko la asilimia 48.

Alisema kutokana na uzalishaji huo katika mkoa wa Dodoma, baadhi ya wakulima wameanzisha viwanda vyao vidogo kwa lengo la kusindika zao hilo, huku wengine wakitengeneza mvinyo, kula kama matunda pamoja na kutengeneza pombe kali.

Naye Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano kutoka TARI Makutupora, Vidah Mahava, alisema katika mpango wa kuliendeleza zao hilo la zabibu katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma wamekuwa wakifundisha wakulima pamoja na wanafunzi wa sekondari na vyuo kuhusu teknolojia mpya za mbegu za zabibu.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Goefrey Mkamilo, alisema lengo la taasisi hiyo ni kuzalisha mbegu kwa kila zao linalolimwa hapa nchini na kuna vituo 18 ambavyo vimepewa majukumu ya kuzalisha mbegu za teknolojia za kisasa na zenye kuongeza tija na uzalishaji.

# Wenye ulemavu waomba mbinu kuendeleza kilimo

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WENYE ulemavu wa macho wanaoishi kwenye kituo cha wasioona cha Matembe bora cha Buigiri Wilaya ya Chamwino, wameomba kupatiwa mbinu zaidi ya kuendesha kilimo cha mboga na matunda ili shughuli wanazofanya ziwe na tija.

Walisema hayo wakati Chama cha Wanafunzi wa Tanzania waliosoma Australia wakiongozwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya ya Chamwino, Sophia Swai, kufanya uwezeshaji wa chakula, nguo na sabuni katika kituo hicho.

Kituo hicho kilichoanzishwa mwaka 1992, kina jumla ya kaya 11.

Mwenyekiti wa kituo hicho, Yohana Kapingo, alisema kituo kilianzishwa na Keneth Dende pamoja na ushirika wa wanafunzi wa Kendal Lee kutoka Uingereza kwenye umoja wao uliojulikana kama Village Aid na walipatiwa visima vya maji ili kuendeleza kilimo cha mboga.

Alisema tangu wakati huo wamekuwa wakiendesha miradi ya kilimo cha bustani.

"Lakini sasa changamoto ni nyingi tangi la maji tunalotumia kwa ajili ya umwagiliaji halikidhi mahitaji lina lita 6,000 na kuna masuala ya mbolea kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Pia alisema kuna changamoto ya mboga kushambuliwa na wadudu, hali inayowafanya wafikirie kuacha kilimo hicho na kujihusisha zaidi na kilimo cha mapapai na migomba.

Alisema wafugaji wa ng'ombe waliokuwa wakiwapatia mbolea wengi wamehama, hivyo mbolea kutopatikana kwa urahisi.

"Wenye mifugo sasa wanaipeleka mbali na mji, yaani changamoto ni mbegu dawa na mbolea... tumeomba mkopo halmashauri kiasi cha Sh. milioni sita, fedha hizo zikipatikana tunaweza kutatua changamoto nyingi, lakini kilio chetu tupate wafadhili watuletee matangi ya maji," alisema.

Alisema waliwahi kupeleka maombi yao kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf ) kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini kuomba tangi la lita 30,000, lakini maombi yao hajajibiwa mpaka sasa.

# SMZ yasaka dawa vijana kukosa ajira

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeahidi kuendelea na juhudi za kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayowakabili vijana, likiwamo la upungufu wa ajira.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Malum ya SMZ, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo wakati akifungua maonyesho ya wajasiriamali vijana wa Walaya ya Magharibi A Unguja.

Maonyesho hayo yaliyoandaliwa na mabaraza ya vijana ya wilaya hiyo ni moja ya majukwaa yakuwahamasisha vijana kujiajiri.

**Serikali kwa kuthamini juhudi za vijana katika kuwaimarisha kiuchumi, imetenga zaidi ya Sh. milioni 800.**

Alisema serikali kwa kuthamini juhudi za vijana katika kuwaimarisha kiuchumi, imetenga zaidi ya Sh. milioni 800.

Alisema watapata fedha hizo kupitia mfuko wa kuwezesha wananchi kiuchumi na wenye masharti nafuu ili kuwanufaisha vijana wa Unguja na Pemba waweze kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi.

Aidha, aliwataka kuachana na tabia za kulalamika na badala yake kuzitumia fursa hizo zilizopo ili waweze kubadili maisha yao.

Aliwataka wajasiriamali kutengeneza bidhaa zenye viwango ili zikabiliane na ushindani wa kibiashara na kupata masoko ya uhakika.

Kadhalika, Waziri wa Vijana Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ali Abeid Karume, aliwahakikishia vijana wa mabaraza ya vijana kwamba wizara itakua mstari wa mbele katika kuwawezesha kuhusu masuala yao mbalimbali ya kujikwamu kiuchumi ili kuona kwamba wanapiga hatua za maendeleo.

Katika risala yao vijana hao walisema baraza la wilaya hiyo limeandaa mipango ya kuanzisha miradi mbalimbali ikiwamo usarifu (kusindika) mazao ya baharikuanzisha kampuni ya usafi na utunzaji wa mazingira ambazo ni jitihada za kuzalisha ajira za vijana takribani 200.



Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, akizungumza katika kongamano la kupinga udhalilishaji lililowashirikisha wasaidizi wa sheria wa mikoa ya Zanzibar lililoandaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), lililofanyika katika Ukumbi wa Sanaa Rahaleo. Wa kwanza kutoka kushoto ni Mjumbe wa Bodi ya Zafela, Fatma Gharib Haji na Mkurugenzi wa Zafela, Jamila Mahmoud. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Serikali kuandaa tamasha la masoko

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kuwawezesha wafanyabiashara kutangaza bidhaa zao ndani na nje ya nchi na kupata soko la uhakika, Wizara ya Biashara na Viwanda imewaandaliwa tamasha la kujitangaza.

Tamasha hilo la sita la biashara linatarajiwa kufanyika Januari 2 hadi 15 mwaka 2020 katika kiwanja cha Maisara Mjini Unguja.

Akizungumza na wanahabari Waziri wa wizara hiyo, Balozi Amina Salum Ali, alisema madhumuni ya tamasha ni kutoa nafasi kwa wafanyabiashara kuzitangaza bidhaa ili kupata masoko.

Aidha, linalenga kuadhimisha Mapinduzi ya Zanzibar pamoja kuwasaidia wajasiriamali, wafanyabiashara na wananchi kuona na kununua bidhaa na huduma. Kadhalika, alisema ukuaji wa sekta ya biashara ndiyo chanzo cha kuongeza ajira nchini na kunyanyua pato la mwananchi pamoja na nchi kwa ujumla.

"Tamasha hili pia linatoa nafasi kwa taasisi za serikali, mashirika, taasisi binafsi kuweza kutangaza huduma ambazo wanazitoa na namna gani wananchi wanaweza kuzifikia taasisi zao ili kuweza kupata bila ya kupata usumbufu," alisema.

Pia alisema mafanikio yaliyopatikana katika matamasha yaliyopita kwa mwaka 2019 katika tamasha la tano jumla ya washiriki 290, ambapo kati ya walitoka nchi ya Rwanda, Kenya, Burundi, Uganda pamoja na Misri.

Alieleza kuwa takwimu zilizokusanywa mwaka jana zimeonyesha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma ikilinganishwa na maonyesho ya mwaka juzi 2018.

Aliwaambia wanahabari kuwa mbali na siku hizo maalum wanatarajia kuwa na kliniki ya biashara itakayozinduliwa katika tamasha hilo kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za papo kwa papo pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili wafanya biashara katika uendeshaji wa biashara zao.

# Zanzibar kuwa na sheria na sera za Diaspora

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ameahidi kuwa hadi atakapomaliza muda wa uongozi suala la Diaspora litakuwa limekaa sawa kimkakati, kisera pamoja na kisheria.

Rais Shein aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati akifungua Kongamano la Sita la Diaspora.

Aliwaambia wa Diaspora Zanzibar imeiweka mazingira uongozi wa awamu inayofuata ya nane katika kulisimamia vizuri suala hilo.

Aidha, alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kusimamia kwa karibu utayarishaji na ukamilishaji wa rasimu ya Sheria ya Diaspora ili iweze kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kabla ya mwezi Mei, 2020.

Alieleza kuwa kuwepo na kutumika kwa Sera ya Diaspora iliyoizindua rasmi mwaka jana kumerahisisha juhudi zinazoendelea hivi sasa za kutayarisha sheria ya diaspora na amefurahishwa na matayarisho yaliyofikiwa.

"Katika mazungumzo yangu niliyoyafanya na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hivi karibuni Desemba 7, 2019, walinieleza kwamba inakuwa rahisi kwao kujadili na kupitisha sheria kwa masuala ambayo tayari yameshatungiwa sera," alisema Dk. Shein.

Alieleza kuwa katika kuhakikisha masuala ya kuuimarisha ushirikiano wa Wanadiaspora na nchi yao ya asili unakuwa endelevu, aliagiza ofisi yake kutenga fedha kila mwaka katika bajeti ya serikali, kwa ajili ya kufanya makongamano hayo ambapo hapo mwanzo yalikuwa yakitegemea michango ya wafadhili.

Aidha, alieleza kufurahishwa kwake na wanadisapora kwa kuzipokea vizuri juhudi zinazochukuliwa na serikali zote mbili za kuanzisha diaspora kwani wamekuwa wakishiriki vizuri katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Aliishukuru timu ya wataalamu ya wanadiaspora walioshiriki katika kuanzisha masomo ya uzamivu (PHD) ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ambapo mafanikio yake yamekuwa makubwa na hivi sasa wanafunzi 39 wanafanya (PHD) ya Kiswahili chuoni hapo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Issa Ussi Haji Gavu alieleza jinsi ya washiriki wa kongamano hilo wanavyoongezeka kila mwaka na kumpongeza Rais kwa juhudi alizozichukua katika kuhakikisha suala la diaspora linaimarika hapa nchini.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global) Norman Jasson, alitoa pongezi kwa Rais Dk. Shein pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Magufuli kwa kuendelea kuwaletea maendeleo Watanzania wote bila ya kujali itikadi, dini au hali zao za kijiografia.

Mwenyekiti huyo alieleza umuhimu wa kuwapo kwa Sera ya Diaspora, huku akitaja changamoto inayokumba vizazi vya diaspora vyenye nasaba za Tanzania ambavyo vimetawanyika duniani kote.

Alisema vimetawanyika kutokana na Watanzania kuolewa na kuoa mataifa mengine na pia wakiwa tayari wamebadilisha uraia.

Alieleza kuwa kizazi hicho ni muhimu sana kwa taifa hilo hata hivyo, kwa sasa wanakuwa na changamoto moja kubwa ambayo wanapokuwa ughaibuni wanahesabika kama ni wageni na wanaporudi nyumbani Tanzania ambako wazazi wao ndipo walipotokea napo wanakuja kama wageni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, George Simbachawene, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamangamba Kabudi alieleza hatua zilizofikiwa katika mchakato wa Sera ya Diaspora kwa upande wa Tanzania Bara.

# Chenge ajinadi kwa utekelezaji wa ilani

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MBUNGE wa Bariadi, Andrew Chenge, amewasilisha taarifa ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa muda wa miaka minne toka 2015 hadi 2019 mbele za wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

Katika taarifa hiyo ambayo ilikuwa na kurasa 73 na kutumia muda wa saa moja kuiwasilisha, muda mwingi aliutumia kuelezea michango mbalimbali ambayo ameitoa kutoka mfukoni mwake pamoja na mfuko wa jimbo.

Mbunge huyo ambaye amekuwa akiitwa kwa majina ya utani ya 'Nyoka mwenye makengeza' na 'Mzee wa vijisenti', alisema kuwa kwa kipindi cha miaka minne, ameweza kutumia kiasi cha Sh. milioni 899.3, ambapo kiasi cha Sh. milioni 650 ni pesa kutoka mfukoni mwake na Sh. milioni 241.7 zikiwa ni fedha kutoka mfuko wa jimbo.

Alisema kuwa fedha hizo zimetumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo kama elimu, afya, maji, barabara, kilimo pamoja na shughuli za kijamii na kiroho, hivyo kufanikiwa kutekeleza ilani kwa zaidi ya asilimia 90.

**Toka zamani kipaumbele changu kimekuwa elimu, ndiyo maana nipeleka maendeleo mengi kwenye elimu, bila ya elimu hakuna maendeleo, na nimekuwa nikipambana sana na utoro pamoja na mimba za wanafunzi.**

Chenge alisema kuwa katika kipindi cha muda huo changamoto kubwa kwake ilikuwa mimba za wanafunzi pamoja na utoro uliokithiri, hali ambayo alieleza kuwa alimua kusaidia zaidi kwenye sekta ya elimu.

"Toka zamani kipaumbele changu kimekuwa elimu, ndiyo maana nipeleka maendeleo mengi kwenye elimu, bila ya elimu hakuna maendeleo, na nimekuwa nikipambana sana na utoro pamoja na mimba za wanafunzi," alisema Chenge, ambaye amewahi kushika nafasi kubwa kadhaa serikalini tangu uongozi wa awamu ya pili hadi ya nne.

Miongoni mwa nafasi hizo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (awamu ya pili na tatu) na Waziri wa Miundombinu (awamu ya nne).

Aliwataka wajumbe hao kuendeleza ushirikiano na kusaidia katika kupunguza utoro, na mimba za wanafunzi, huku akibainisha kuwa chama hicho bado kina nguvu sana na kinakubalika zaidi kwa wananchi.

Awali akifungua mkutano huo Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bariadi, Juliana Mahongo, alimpongeza mbunge huyo kwa kazi kubwa ambazo amezifanya katika kipindi cha miaka minne hasa kuwasaidia wananchi.

Mahongo alisema kuwa kazi kubwa ambazo zimefanywa na Chenge ni katika kuhakikisha sekta ya elimu inakua kwa kiwango kikubwa pamoja na kushirikiana na wananchi kupunguza uhaba wa madarasa, madawati na nyumba za walimu.

Aidha, Mwenyekiti huyo aliitaka serikali kutafuta ufumbuzi wa haraka wa kulipa madeni ya wakulima wa pamba, huku akitaka kuangaliwa upya vyama vya ushirika kwani baadhi yake vinatuhumiwa kwa ubadhirifu.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana ya CCM Taifa, Kheri James, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema kuwa wale wote ambao wameanza kampeni za kutaka ubunge katika chama hicho kabla ya muda, wanaweza wasifanikiwe.

James aliwaonya pia wale wapambe wao ambao wanawasaidia kuchafua viongozi waliopo, kuwa na wao nafasi zao za kurudi ziko hatarini kwani chama hicho kina taratibu zake za kuwapata viongozi.



Wahitimu wa fani mbalimbali katika Chuo Kikuu cha St Joseph Kibamba jijini Dar es Salaam, wakila kiapo cha uadilifu kwenye fani zao wakati wa mahafali ya 12 ya chuo hicho mwishoni mwa wiki, wahitimu 853 walitunukiwa shahada mbalimbali. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wagonjwa wa mifupa, mgongo kuchunguzwa

**Na Mwandishi Wetu**

MTAALAMU wa maradhi ya mgongo na mifupa kutoka India, anatarajiwa kuwasili nchini wiki hii, ambapo watawafanyia uchunguzi watu mbalimbali wenye maradhi hayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Hospitali ya Regency, mtaalamu huyo ni Dk. Viral Shah ambaye amebobea kwenye maradhi ya mgongo na mifupa.

Alisema mtaalamu huyo anatoka taasisi kubwa ya tiba ya Shalby, Ahmedabad-Gujarat ya India ambayo ni moja ya hospitali kubwa barani Asia na atafanya uchunguzi huo kwa siku mbili kuanzia Desemba 19 na 20, mwaka huu.

"Hii ni fursa kubwa kwa Watanzania kuhudumiwa na wataalamu bingwa wa maradhi ya mgongo, magoti na nyonga, hivyo tunawaomba watumie fursa hii kuwaona wataalamu hawa," alisema na kuongeza kuwa wale wanaotaka kuwaona wataalamu hao waje na X-ray zao za hivi karibuni na ripoti za madaktari walikokuwa wakitibiwa.

"Watu 200 wa kwanza ndio watakaopata fursa ya kuwaona wataalamu hao, hivyo tunawahamasisha wenye matatizo kama hayo waende kuwaona wataalamu hao ili wapate tiba na ushauri," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema watakaofika watapata fursa ya kupata ushauri wa maumivu ya shingo, taratibu za upasuaji, maumivu ya mgongo na matatizo ya uti wa mgongo.

**Watu 200 wa kwanza ndio watakaopata fursa ya kuwaona wataalamu hao, hivyo tunawahamasisha wenye matatizo kama hayo waende kuwaona wataalamu hao ili wapate tiba na ushauri.**

# Viongozi waombwa vita ukatili wa kijinsia

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SHIRIKA la kiraia la Kutetea Haki za Wanawake, Watoto mkoani Mwanza (Kivulini), limewaomba viongozi wa dini kutoa ushirikiano katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya makundi hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo mkoani Mwanza, Yasini Ally alitoa ombi hilo katika kikao cha kujadili na kuweka mikakati ya pamoja kuhusu kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kilichofanyika jijini Mwanza.

"Ibada zisizo na muda maalum katika makambi, mikesha ya usiku zinaweza kuchangia vitendo viovu, kama ubakaji, ulawiti, mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto," alisema Ally.

Ally aliiomba pia serikali na wadau wengine kutoa ushirikiano, katika kuweka mikakati madhubuti ya pamoja kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa katika Mkoa wa Mwanza, ambapo kiwango chake ni asilimia 60.

Ally alisema kuwa changamoto zingine zimekuwa zikisababishwa na baadhi ya viongozi wa familia kutokana na kutelekeza familia zao na kuoa wanawake wengine katika maeneo mbalimbali wanayoishi, jambo ambalo linavunja maadili ya kidini na sheria za ndoa.

Sheikh wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, alisema kuwa vitendo hivyo vinatakiwa kukemewa vikali kupitia misikiti na makanisa, serikali, wadau kwani ni udhalilishaji mkubwa wa haki za binadamu.

"Tunaiomba pia serikali kuchukua hatua kali kwa wale wanaojihusisha na vitendo vya udhalilishaji wa haki za wanawake na watoto...sisi tuko tayari kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa," alisema, Kabeke.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Philadelphia Gospel Assembly jijini Mwanza, Zenobius Isaya, alisema kuwa vitendo hivyo ni kumkufuru Mungu katika matendo mema anayoyataka, ambaye alikemea pepo hilo kwa kutaka washindwe na kulegea.

HABARI KIMATAIFA

# Watu 33 wadaiwa kuuawa na waasi ADF

**KINSHASA,** Congo

WATU 33 wamedaiwa kuuawa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wakati wa shambulizi la watu wanaoshukiwa kuwa waasi wa ADF usiku wa kuamkia jana katika Wilaya ya Beni Mashariki mwa nchi hiyo karibu na mpaka wa Uganda.

Viongozi wa eneo hilo wanadai kuwa waliohusika na mauaji hayo ni wanamgambo wa kundi la waasi wa Allied Democratic Forces (ADF) kutoka nchi jirani ya Uganda.

**Wanamgambo hao wanadaiwa kuwalenga wanavijiji kama hatua ya kuwazuia wasiwasaidie wanajeshi.**

Wanawake 13 ni miongoni mwa watu 22 waliouawa na waasi wa ADF usiku wa Jumamosi.

Mauaji ya wanavijiji hao ni msururu wa ukatili na vifo vinavyoendelea kuwapata raia wasiokuwa na hatia katika mkoa wa Kivu Kaskazini, licha ya serikali kuanzisha operesheni mahsusi ya kijeshi ya kutokomeza makundi ya waasi yaliyo na ngome zake eneo hilo.

Zaidi ya raia 180 wameuawa tangu mwezi Oktoba mwaka huu, wakati jeshi lilipotangaza operesheni dhidi ya makundi ya wanamgambo wenye silaha wanaotuhumiwa kutekeleza mashambulizi dhidi ya raia.

Wanamgambo hao wanadaiwa kuwalenga wanavijiji kama hatua ya kuwazuia wasiwasaidie wanajeshi.

Mashambulio ya hivi karibuni yamezua hasira na maandamano makali miongoni mwa wakazi ambao wanalaumu vikosi vya kulinda usalama vya umoja wa mataifa kwa kutowahakikishia usalama.

Jambo linalozua mjadala ni kwamba Rais Felix Tshishekedi amezuru eneo hilo mara kadhaa na kutoa ahadi za kufanya kila liwezekanalo kuwalinda raia na mali zao.

Mji wa Beni, wenye idadi ya watu laki mbili ndio umelengwa sana na mashambulizi ya waasi.

Operesheni za Jeshi la Taifa na za vikosi vya Umoja wa Mataifa vya kulinda amani zina ngome zake katika mji huu wa Beni.

Mnamo mwezi Novemba mwaka huu, raia wenye hasira waliandamana mjini Beni, baada ya mauaji ya kinyama ya watu nane na kuwashtumu askari wa Umoja wa Mataifa kwa kutowalinda dhidi ya mashambulizi ya waasi.

Ofisi ya Meya wa mji huo, Masumbuko Nyonyi, pia ilichomwa wakati wa maandamano hayo.

Mara kadhaa meya huyo alinukuliwa akisema kuwa kinachojitokeza bayana ni kwamba waasi wanaonekana kuwashinda maarifa wanajeshi wa serikali na wale wa Umoja wa Mataifa ambao wametumwa kuwasaka wapiganaji wa kuvizia hasa wale wa kundi la Allied Democratic Forces (ADF) kutoka Uganda. **BBC**



Makaburi ya watu waliouawa wakati wa shambulizi la wanaoshukiwa kuwa waasi wa ADF usiku wa kuamkia jana katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: DW**

## Waziri mkuu awekwa kiporo

**BEIRUT,** Lebanon

RAIS wa Lebanon, Michel Aoun, ameahirisha mashauriano ya bunge ya kumpata waziri mkuu mpya yaliyopangwa kufanyika jana baada ya maombi kutoka kwa mgombea pekee wa nafasi hiyo Saad Hariri.

Taarifa ya Ofisi ya Rais iliyotolewa jana, ilisema hatua hiyo imekuja baada ya Hariri kutaka kuwapo nafasi ya majadiliano zaidi juu ya suala la kuundwa serikali na sasa mashauriano hayo yatafanyika Alhamisi.

Tangu Oktoba 17 Lebanon inaandamwa na maandamano ya umma ya kudai mageuzi katika serikali na uchumi wa nchi hiyo yaliyosababisha kujiuzulu kwa Waziri Mkuu Saad Hariri.

Hariri anatarajiwa kutangazwa tena kuwa waziri mkuu kwa idadi ndogo, lakini waandamanaji wanapinga kiongozi huyo wa zamani kuongoza tena serikali mpya. **DW**

# Marekani yaitaka Korea Kaskazini kurejea kwenye mazungumzo

**WASHINGTON,** Marekani

MWANADIPLOMASIA wa ngazi ya juu nchini Marekani amesema nchi hiyo haitokubali muda wa mwisho uliowekwa na Korea Kaskazini wa kufikia makubaliano kuhusu mazungumzo ya nyuklia yaliyokwama.

Ameitaka nchi hiyo ya Asia kerejea haraka mbele ya meza ya mazungumzo ili kupata suluhu ya tatizo hilo.

Stephen Biegun ambaye ni mjumbe maalum wa Marekani kwa Korea Kaskazini, alisema kwamba ingawa wanatambua kuwa Korea Kaskazini inaweza kufanya uchokozi katika siku zijazo, hilo halitosaidia kutafuta amani ya kudumu kwenye rasi ya Korea.

Biegun ambaye alikuwa mjini Seoul, Korea Kusini kwa mazungumzo na maofisa wa taifa hilo, aliitaka Korea Kaskazini kurejea katika mazungumzo ili kukamilisha mafanikio yaliyopatikana. **DW**

## Mkutano wa tabianchi wamalizika bila malengo

**MADRID,** Hispania

MKUTANO wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi umemalizika juzi mjini Madrid, nchini Hispania bila kuwapo malengo mapya ya kufikiwa, huku tishio kubwa likiwa ni ongezeko la joto duniani kuzua maandamano ya umma duniani.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutteres, alisema Jumuiya ya Kimataifa imepoteza nafasi muhimu ya kuonyesha dhamira pana zaidi katika makabiliano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Guterres alisema anampango wa kuongeza juhudi za kutimiza matakwa ya mkataba wa Paris unaohimiza kiwango cha joto duniani kuwa chini ya nyuzi mbili ili kuzuia athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi duniani.

Wajumbe wa mkutano huo wa COP25 wamekubaliana kuyakumbusha mataifa yote 200 yaliyowakilishwa kutimiza ahadi za kufikia malengo ya kupunguza uchafuzi ifikapo mwaka 2020.

Hata hivyo, mjadala mkuu kuhusu kanuni zitakazoongoza biashara ya gesi ya kaboni umeahirishwa hadi mwakani. **DW**

# Ofisi ya CAG yawezesha wananchi kupata taarifa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIKA kipindi cha miaka mitano Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imewezesha wananchi kufikiwa na taarifa za ukaguzi, hivyo kuwa na uelewa mpana kuhusu rasilimali za nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu CAG, Benjamin Mashauri, wakati akifungua warsha ya siku mbili kwa asasi zisizo za kiserikali, taasisi na waandishi wa habari ambayo inafanyika jijini Dodoma.

Mashauri alisema tangu mwaka 2012, ofisi ya CAG imekuwa ikitoa machapisho na elimu kwa wananchi hata kuwafikia watu kupitia vyombo vya habari, hivyo kuamsha ari ya wananchi kujua kuhusu taarifa za ukaguzi.

"Toleo maalumu kwa wananchi limekuwa likiandaliwa na ofisi kila taarifa ya ukaguzi inapofanyika na ikibainisha kwa lugha nyepesi kili kilichopatikana kwenye ukaguzi ili wananchi waweze kuelewa na kisha kufanya ufuatiliaji," alisema.

Alitaja mafanikio mengine yaliyopatikana ni kufanya kazi kwa pamoja na asasi za kiraia na vyombo vya habari kwa karibu zaidi, jambo ambalo limesaidia kuboresha kazi za ukaguzi ambazo zinasaidia kuleta maendeleo ya nchi na hasa kuangalia thamani ya kodi zao.

"Ushirikiano huu umesaidia kuboresha kazi za kikaguzi ambazo zinasaidia kuleta maendeleo ya nchi kwa sababu kila mmoja anajifunza jinsi ya kutumia na kulinda rasilimali ambazo zinatokana na kodi zetu sisi wenyewe."

Mashauri aliwahakikishia washiriki kuwa kufanyika kazi na kuendelea kufanyiwa kazi mapendekezo yaliyotolewa kwenye warsha hiyo na zile zilizotangulia ili kuboresha upatikanaji wa taarifa kuhusu ripoti za CAG.

Katika warsha hiyo, wanapata fursa ya kupitia taarifa za ukaguzi kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2018, ambapo mada kadhaa zilijadiliwa ikiwa ni misingi ya sheria inayoongoza ofisi ya CAG na hati za ukaguzi.

Mada zingine ni ripoti ya ukaguzi wa miradi, ripoti ya ukaguzi wa ufanisi, ukaguzi wa serikali za mitaa, ripoti ya ukaguzi wa mifumo, ukaguzi wa serikali kuu na masharika ya umma na uandikaji wa habari za ripoti za CAG.





Mkurugenzi wa Wateja wa Kampuni wa Benki ya NBC, Linley Kapya (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi wa Fedha wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Abdallah Mwaduga, katika hafla iliyowaandalia wateja wake jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni ofisa katika kitengo cha wateja binafsi wa benki hiyo, Rehema Chonde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 38/- kupambana na saratani mwakani

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Taasisi ya Huduma za Afya Aga Khan na serikali ya Tanzania zimetia saini hati ya makubaliano ya Sh. bilioni 38 kutekeleza mradi wa Tiba ya Kina Saratani nchini (TCCP).

Mradi huo unaotarajia kuanza mwakani utatekelezwa kwa ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi na utahusisha Hospitali ya Aga Khan, Taasisi ya Kansa ya Ocean Road, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Hospitali ya Bugando, Mwanza.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akizungumza kwenye hafla hiyo jana, alisema ugonjwa huo ni tatizo Tanzania na umekuwa ukiongezeka.

"Mkurugenzi wa Taasisi ya Ocean Road ameniambia sasa hivi wanawaona wagonjwa takriban 64,000 kwa mwaka. Hili ni ongezeko la wagonjwa takribani 30,000 kutoka mwaka 2015 ambapo walikuwa wanaona wagonjwa 34,000.

"Wagonjwa wengi wanaokuja katika taasisi hii wanakuwa wamechelewa, asilimia 70 wanakuja saratani ikiwa ipo katika hatua mbaya zaidi," alisema.

Dk. Ndugulile alisema vifo vinavyotokana na ugonjwa huo ni vingi kwa sababu wengi huchelewa.

"Takribani Watanzania 42,000 wanaugua lakini waliopita katika vituo vya huduma ya afya ni takribani watu 13,000 pekee, kuna changamoto ya uelewa katika jamii na nyingine ni ya matibabu kupatikana kwa urahisi na kufika kwa haraka.

"Kwa sasa ni taasisi chache ambazo zinatoa matibabu ya saratani ndiyo maana wagonjwa wengi wanaopokelewa katika taasisi hii wanatoka sehemu mbalimbali. Gharama nazo ni kubwa.

"Kumtibu mgonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi mpaka apone ni zaidi ya Sh. milioni tano na kwa mgonjwa wa saratani ya matiti ni Sh. milioni 10."

Dk. Ndugulile alisema kutokana na changamoto hizo, serikali ilichofanya ni kupanua wigo wa kupima na kutoa chanjo kwa mabinti kuanzia miaka tisa hadi 14.

Pia alisema huduma hizo zinatolewa bure na serikali licha ya gharama kubwa ya kutibu ugonjwa huo na wameongeza bajeti ya dawa ambapo taasisi hiyo inatumia Sh. bilioni 10.

Kadhalika alisema wamefanya uwekezaji kwa kununua vifaa vya kisasa ambapo moja ya mashine iliyonunuliwa ndani ya miezi minne, huduma itapatikana Tanzania.

Dk. Ndugulile alisema serikali imeona inafanya vizuri katika magonjwa yanayoambukiza lakini changamoto kubwa itakayoikabili miaka michache ijayo ni magonjwa yasiyoambukiza.

"Huko mbele ya safari tujipime kwa kiasi gani tumezuia watu wasijie hospitali siyo kwa kiasi gani tumetibu Watanzania, hili ni jambo kubwa ambalo tunatakiwa kulifanyika kazi, tuwekeze kwenye kinga," alisema.

Kuhusu mradi huo, Dk. Ndungulile alisema unaonyesha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi zenye lengo moja la kukabiliana na tatizo hilo.

"Mradi huu utajielekeza kujenga uelewa ndani ya jamii kuhusu saratani, nisisitize, mjielekeze katika kukinga zaidi kuliko kutibu, mjielekeze nguvu zaidi katika kubaini saratani katika hatua za awali kwa sababu nyingi zinakuja zimechelewa sana," alisema.

Pia aliwataka wajenge uwezo wa utambuzi ugonjwa kwa sababu moja ya vikwazo kwenye matibabu ya saratani ni huduma za maabara, huchelewa kutoa majibu mapema.

"Hii inatokana na kwamba tuna wataalamu wachache sana haya ni maeneo ambayo tunahitaji tuwekeze mtu anakaa miezi miwili hadi mwaka bado hajapata majibu tunataka tuboreshe zaidi na tuwe na wataalamu wengi, tujielekeze kwa wataalamu ambao wataweza kutoa huduma za mionzi na kwa ajili ya watoto," alisema.

Aliwataka wajielekeze kwenye utafiti kwa kuangalia aina za saratani, wanaopata na watumie takwimu za ndani ya nchi ili ziisaidie serikali katika kuandaa bajeti na mambo mengine.

Mkurugenzi wa Idara ya Matibabu ya Saratani Aga Khan, Dk. Harrison Chuwa, ambaye ndiye Mkurugenzi wa mradi huo, alisema mradi huo una malengo makuu manne ambao ni uboreshaji wa miundombinu na vifaa tiba, kuendeleza na kukuza rasilimali watu, kuboresha huduma na uhamasishaji wa saratani katika jamii na kudumisha ushirikiano wa utafiti.

Alisema mradi huo utatekelezwa katika wilaya 13 za mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam katika kipindi cha miaka minne na utaleta manufaa nchi nzima.

"Tunatarajia kuwafikia takribani asilimia 60 ya wananchi, kusogeza huduma za saratani kwa wananchi hususani za uchunguzi wa awali, kuongeza idadi ya wagonjwa watakaofika hospitali kwa matibabu kutoka asilimia 20 hadi asilimia 40," alisema.

Alisema katika mradi huo, AFD imetoa Sh. bilioni 29 na Aga Khan imechangia Sh. bilioni tisa.

Naye Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la AFD nchini Tanzania, Stephanie Mouen, alisema mradi huo ni wa kimkakati unalenga kuboresha tiba ya saratani kwa ujumla Tanzania.

"Mchango wa fedha kutoka Mfuko wa Aga Khan utasimamia na kuendesha mradu huu na kujenga uwezo wa wafanyakazi katika wigo mpana wa kutoa tiba kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Kifaransa na kimataifa zinazotoa rufani ya mafunzo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, alisema wamekuwa wakipokea wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali nchini ambapo kila mwaka wamekuwa na wagonjwa wapya 42,000 na wanaopelekwa vituo vya afya na hospitali ni 13,000 tu.

Alisema mradi huo utasaidia kuwafikiwa wagonjwa wengi ambao wameshindwa kufikiwa na huduma za afya, ambapo zaidi ya asilimia 50 watafikiwa na mradi huo katika hospitali mbalimbali.

Naye Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier, alisema wameunganisha nguvu ili kufanikisha makubaliano ya kihistoria kwa malengo ya kuiboresha sekta ya afya husussan saratani ambayo bado ni tatizo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

### VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 078653304 0629478005.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA CHETI



115557202

**ERASTO AARON MTELEKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1487-0175** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BOKO SEKONDARI mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/TAB/RB/550542/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI



115557502

**Abdallah Mohamed** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0534/0538** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia St. Anthony's Sec. School Mbagala mwaka 2004. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/550629/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI



115558202

**ERICA STONE TENGA** anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kuzaliwa kilichotolewa na RITA Dar es salaam mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/TAB/RB/107578/2019.**

### KUBADILISHA UMILIKI WA GARI

**JOSEPH MERUMA MGERI** anatangaza kubadilisha umiliki wa gari yenye namba za usajili **T 276 CSR** na kwenda kwa mmiliki mpya mwenye jina la **NEMES KRISIPINI MROSSO.**

115552501

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASUBISYE OBEL MWAMFUPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 983 DRS TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP600026047.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910810998373.**

115556802

### KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

Mimi **Mshihiri Yakubu Mwangome** ambaye ndiye msimamizi wa mirathi ya Mariam Khalifan Kubo natangaza kupotelewa na wa Hati ya nyumba (offer) kiwanja namba 57 Kitalu C Msambweni Tanga. Yeyote atakayeiona atoe ripoti kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0715 193242.** Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/529343/2019.**

115557402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Elizaphan Lutende Marembo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Aina ya Toyota Land Cruser yenye namba za usajili **T 181 BES.** Chassis No. **VZJ950006520.** Engine No.5VZFE44002. Rangi Silver. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/553565/2019.**

115555802

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAMUD SEIF MOHAMED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADIYA GARI AINA YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 618 AUN** NA CHASSIS NAMBA **A109365.** KWAYOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KHM/RB/882/2019.**

115558102

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENBROS MOTORS LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 752 BGW TOYOTA CAMI.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/544895/2019.**

115557802

### KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 456 CGP, MC 802 CFL, MC 638 CGY, MC 720 CGR, MC 971 CJJ, MC 973 CJJ, MC 974 CJJ, MC 738 CHG, MC 825 CHG, MC 321 CHL, MC 294 CHH, MC 244** BGM. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/545096/2019.**

115534902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALOME FRUMENCE MASSAWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 840 DGY NISSAN CARAVAN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/8044/2019.**

115557102

### MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, KATEMANA AUCTION MART & GEN SUPPLIES** tutauza kwa mnada wa hadhara viwanja vya wadaiwa sugu kuanzia saa nne Asub. **Ndugu JAMES MASHAURI KATEMI** - Kilichopo Mbugani Nyankumbu Geita na Ndugu **JULIUS ELIAS JOHN** –(Kilichopo Ishinde –Geita). Lengo ni kufidia/ kupunguza madeni ya mikopo wanayodaiwa. Minada yote itafanyika Tarehe 20/12/2019, mahali dhamana zilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi. **Katemana A/ mart: 0763452525; Tujijenge Tanzania Ltd: 0718116306.**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LJUNGBERG SASA KUMSHUGHULIKIA OZIL




**LONDON,** England

KOCHA wa muda wa Arsenal, Freddie Ljungberg amesema "atadili" na Mesut Ozil baada ya kiungo huo kuonyesha hasira wakati alipotolewa nje.

Kiungo huyo wa zamani wa Ujerumani alivua glovu zake na kuzipiga kwa teke wakati alipotolewa nje, huku timu yake ikichapwa 3-0 na Manchester City.

Tukio hilo lilikuja saa chache baada ya klabu hiyo kujiweka mbali naye juu ya maoni ya Ozil aliyoyatoa kwenye mtandao wa kijamii kuhusu kile wanachofanyiwa waislamu wa Uighurs nchini China.

"Kile anachofanya ni juu yake na nitadili naye baadaye," alisema Ljungberg.

"Nipo hapa kila siku, lakini bila shaka wachezaji wawe na nidhamu. Nilitaka nguvu zaidi kwa timu."

Ozil mwenye umri wa miaka 31, alizomewa na mashabiki wake wakati akitembea kuelekea benchi na nafasi yake kuchukuliwa na Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 19 katika dakika ya 59 kwenye mchezo huo wa Jumapili.

Ljungberg, ambaye alikuwa kocha msaidizi chini ya Unai Emery, alichaguliwa kuwa kocha wa muda baada ya Mhispania huyo kutimuliwa mapema Novemba.

Bado hakuna maamuzi yaliyofanyika na bodi ya Arsenal kuhusu nani wa kuchukua mikoba hiyo, huku Carlo Ancelotti, Nuno Espirito Santo na Mikel Arteta wamekuwa wakihusishwa na kazi hiyo.

# Carragher: Mabeki wanaiua Arsenal

**LONDON,** England

WALINZI wa Arsenal walionekana kama wasio na uzoefu wakati wakifungwa na Manchester City, huku kiwango chao kikiwa sehemu ya "ugonjwa", amesema Jamie Carragher akiiambia Sky Sports.

"Washika Bunduki' hao walifungwa mabao matatu katika kipindi cha kwanza kwenye Uwanja wa Emirates wakati Manchester City ikipata ushindi wa mabao 3-0 kirahisi.

Arsenal imeruhusu mabao matano machache zaidi kuliko timu inayoshikamkia ya Watford na wakicheza mechi mbili tu bila kuruhusu bao msimu huu, huku Carragher akishangazwa na kiwango cha timu hiyo.

"Kila wakati nawaangalia wao wakicheza, kila wakati mpira ukija kwenye kushambulia wanashindwa kuondoa haraka," alisema.

"Kumbuka bao la Norwich ambapo (Shkodran) Mustafi na (David) Luiz akimuacha (Teemu) Pukki akikimbia na kugeuka.

"Ni kitu ambacho wanahitaji kubadilika wakiwa kwenye mazoezi. Kulinda lango na kusukumiza mashambulizi mbele. Nilisema wakati wa uchambuzi wangu kuhusu hilo.

"Wanakaa na mpira badala ya kusukumiza mashambulizi mbele. Inaonekana ni kama hawajui wanachokifanya.

"Wakati mwingine unaona makosa makubwa golini; Calum Chambers anapoteza mpira kipindi cha pili, Manchester City wanakwenda kwenye goli kirahisi.

"Kila mmoja anaweza kuona hilo. Lakini kuna vitu vinaiua timu. Kuna wachezaji wanaiumiza timu na ndio maana David Luiz hachezi."






# *Ronaldinho amkataa Messi kimtindo*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa zamani wa Barcelona, Ronaldinho amesema hawezi kumchukua Lionel Messi kuwa mchezaji bora wa muda wote kuwahi kutokea kwenye mchezo wa soka.

Na badala yake, fundi huyo wa mpira kutoka Brazil, Ronaldinho alisema Messi anapaswa tu kufurahia kwa kuambiwa kuwa ni mchezaji bora katika wakati wake.

Baada ya kumshuhudia Messi akibeba tuzo ya sita ya Ballon d'Or, Ronaldinho alisema: "Nimefurahishwa na Messi kwa sababu ni rafiki yangu na zaidi ya hilo amekuwa kama bango la Barcelona.

"Sipendi sana kulinganisha kwa sababu ni ngumu kumpata mtu bora zaidi katika historia ya mchezo wa soka, kuna watu kama Diego Maradona, Pele, Ronaldo, hapo siwezi kusema Messi ni bora zaidi yao.

"Messi ni bora katika zama zake, bora katika wakati wake."

Ronaldinho alicheza soka la mafanikio makubwa akiwa na Barcelona na hata Brazil, ambapo alikuwa kwenye kikosi kilichobeba ubingwa wa Kombe la Dunia 2002 huko Japan na Korea Kusini huku akiwahi pia kunyakua tuzo ya Ballon d'Or.

HABARI MICHEZO

# Tuchel ampoza Neymar akikosa penalti

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel amemsifia Neymar kufunga penalti yake ya pili, akisema mshambuliaji huyo alikuwa na "huzuni" kukosa ya kwanza dhidi ya Saint-Etienne.

Neymar alifunga penalti ya kipindi cha pili wakati PSG ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Jumapili.

Hiyo imekuja siku chache baada ya raia huyo wa Brazil kumkabidhi Edinson Cavani majukumu ya kupiga penalti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Galatasaray.

Lakini Tuchel bado anaimani na Neymar, ambaye alitoa pasi mbili za mwisho kwenye ushindi huo mzuri.

"Mara zote zina woga nikiwa kama kocha, hiyo ni kawaida," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati anapiga, kwa kawaida nakuwa na uhakika kwamba atafunga. Ana uchungu kwa sababu bado anataka kufunga, ilikuwa ni nafasi nzuri kwa upande wake.

"Lakini anakwenda kupiga penalti inayofuata, na nina uhakika atafunga tena."

Wakati tayari wakiwa nyuma kwa bao la uongozi la Leandro Paredes, Saint-Etienne walibakiwa na wachezaji 10 uwanjani wakati Jean-Eudes Aholou alipoonyeshwa kadi nyekundu dakika ya 25.

Kylian Mbappe, alitengeneza mabao mawili kwa Neymar, na akafunga mara mbili na Mauro Icardi akifunga wakati PSG wakipata ushindi wao wa tano mfululizo kwenye Ligue 1.

"Tulilinda vizuri, timu ilikuwa na nguvu, mara zote tulicheza kwa umoja," alisema," Tuchel.





# BENZEMA ATAKA LA LIGA AKIINUSURU REAL

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amesema anataka kuiongoza Real Madrid kushinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu baada ya kuwaokoa 'Los Blancos' hao kufungwa na Valencia.

Madrid ilipata sare ya 1-1 na Valencia Jumapili shukrani kwa bao la dakika za majeruhi la kusawazisha la Benzema.

Baada ya bao la Luka Jovic kukataliwa kwa madai ya kuotea, Benzema alisawazisha dakika za lala salama kwenye Uwanja wa Mestalla, hivyo Madrid ikabaki na pointi sawa na Barcelona kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

"Nataka kushinda taji la ligi hii, kama nitaweza kuwasaidia wachezaji wenzangu kucheza na kwa maneno, nitafanya hivyo," alisema Benzema, ambaye amepitwa bao moja tu na Lionel Messi kwenye orodha ya wafungaji wanaoongoza La Liga msimu huu.

"Mimi ni nahodha namba tatu na natakiwa kuwasaidia.

"Nafikiri ni pointi nzuri kwa upande wetu. Inaweza kuwa muhimu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na kuangalia tunafanya vizuri.

"Kilichobadilika ikilinganishwa na misimu mingine ni idadi ya mabao. Mara zote nitajaribu kuisaidia timu uwanjani na ninajiamini kweli kweli.

"Kuwasaidia wachezaji wenzangu pia ni muhimu kwangu kwa sababu wananipa mpira na kutengeneza nafasi ya kufunga mabao zaidi."

Benzema alifunga bao hilo baada ya golikipa, Thibaut Courtois kukaribia kusawazisha kwa kichwa.

Courtois alipanda kwa ajili ya kusaidia wakati wa kona wakati Madrid wakitafuta bao la kusawazisha na mpira wa kichwa aliopiga ulipanguliwa na golikipa wa Valencia, Jaume Domenech kabla ya Benzema kuuwahi na kuupiga.



# Klopp: Van Dijk, Gomez watatulinda

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Virgil van Dijk na Joe Gomez wanaweza kucheza "kwa utulivu vizuri " pamoja wakati Liverpool ikikabiliwa na majeruhi katika safu ya ulinzi.

Huku Joel Matip na Dejan Lovren wakiwa majeruhi, Van Dijk na Gomez walianza kwenye safu ya ulinzi kwenye mchezo dhidi ya Watford ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 Jumamosi.

Gomez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akicheza mara kwa mara chini ya Van Dijk kabla ya kuumia mguu Desemba mwaka jana.

Klopp amesema amekuwa akizungumza mara kwa mara na Gomez na anaamini upatina wa mchezaji huyo wa England na Van Dijk unaweza kukua zaidi.

"Tunazungumza, tunazungumza mara nyingi," alisema kocha huyo wa Liverpool akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.


"Kwenye timu nzuri, ambayo ndio iko hivyo, treni haiwezi kusubiri. Kwa maana kwamba wachezaji wameonyesha kujituma, na sidhani kama mtu yeyote anaweza kufikiri kwamba tunaweza kumuweka benchi Joel.

"Ni wazi kwamba vijana wana vipaji vya kweli.

"Kijana bado mdogo, hiyo si sababu, ni suala tu la kwamba anaweza kucheza vizuri pamoja. Lakini hawa wawili, Joe na Virg, wanapendana kila mmoja na wanaweza kucheza kwa utulivu mkubwa."

Gomez na Van Dijk waliisaidia timu yao kuwazuia Watford wakati Liverpool ilipopaa kileleni na kuongoza kwa tofauti ya pointi 10.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LJUNGBERG: ARSENAL TAFUTENI KOCHA HARAKA

## ●●● Kwangu ni heshima kubwa kufanya hili, lakini Mertesacker anafanya kazi mbili...

**LONDON,** England

FREDDIE Ljungberg anaamini kwa sasa Arsenal inahitaji kufanya uamuzi wa haraka katika kutafuta kocha mpya.

**Arsenal ilikubali kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Manchester City juzi, Jumapili na Kevin De Bruyne aking'ara kwa kucheka na nyavu mara mbili na kutoa pasi ya mwisho moja.**

'Gunners' wameshinda mechi moja tu kati ya 12 kwenye mashindano yote, huku Ljungberg akihusika katika mechi tano zilizopita kama kocha wa muda baada ya Unai Emery kutimuliwa.

Hata hivyo, utafutaji wa kocha mpya hauonekani kukaribia kukamilika, na taarifa zikidai kocha msaidizi wa Man City, Mikel Arteta bado ndiye anayewindwa, na Ljungberg ameishauri Arsenal kufanya maamuzi haraka.

"Sote tunapaswa kujitazama katika kioo. Nilichohisi ni kwamba mechi dhidi ya West Ham [Arsenal iliyoshinda mabao 3-1] ilikuwa ni hatua kubwa katika mwelekeo sahihi," Ljungberg aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Sijaliona hilo kutoka kwa timu katika muda mrefu. Leo [juzi dhidi ya City] wao walikuwa timu kubwa, walikuwa na ubora zaidi yetu.

"Kwangu mimi ni heshima kubwa kufanya hili, lakini Per [Mertesacker, anayemsaidia Ljungberg] ni kocha wa makinda na anafanya kazi mbili. Nadhani inahitaji kusafisha mambo, hivyo kila mmoja anajua.

"Hilo ndilo nililolisema lakini kwa ujumla ni juu ya klabu. Ninaheshimiwa sana na nitafanya kile ninachoweza, lakini ninaamini tunahitaji kufanya uamuzi, bila kujali ni nini."

Mashabiki wengi walionekana kutoka Uwanja wa Emirates kabla ya mchezo kumalizika Jumapili, lakini Ljungberg alisisitiza ni mwenye fahari kutokana na sapoti wanayoitoa kwa timu.

"Mimi ni mtu wa Arsenal na tunajaribu kila kitu, lakini tunahitaji kuwa sawa na pia kuna pengo kati ya City na Liverpool na zilizobaki," Ljungberg alisema.

"Ni mwenye furaha na fahari ya mashabiki, wanajibu vizuri kwa wachezaji makinda waliokuja. Bila shaka wanaweza kuona kuna tofauti. Waliimba mwishoni na kukubali vijana wadogo wamejaribu.

"Tunajua miaka miwili iliyopita tulipata wakati mgumu dhidi ya City nyumbani. Tulipowahesabu ambayo ilikuwa moja ya mipango yetu kimchezo walionyeshwa kadi tano za njano

"Pengine tunaweza kujifunza kuwa na mbinu zaidi na si kuwaacha wapinzani wetu watudanganye. Ni udhaifu wetu kidogo. Tunahitaji kuchukua hizo adhabu."

## ZISIKUPITE

### COUTINHO LULU BAYERN

WACHEZAJI wa Bayern Munich wameitaka klabu hiyo kumsajili jumla kiungo wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho, ambaye anaichezea kwa mkopo akitokea Barcelona, kufuatia kuendelea kuonyesha kiwango cha juu huku Jumamosi akiipa ushindi dhidi ya Werder Bremen baada ya kutupia hat-trick. ***(Mirror)***

### ARSENAL, SANTO HAWAJATETA

ARSENAL hajazungumza na Wolves kuhusu ruhusu ya kuzungumza na Nuno Espirito Santo kwa ajili ya kwenda kuinoa. ***(Express and Star)***

### PELLEGRINI AVUTIWA PUMZI

KOCHA aliyepo kwenye presha kubwa, Manuel Pellegrini bado anatarajiwa kuendelea kuinoa West Ham katika mechi ijayo dhidi ya Crystal Palace Siku ya Kufungua zawadi ['Boxing Day']. ***(Guardian)***

### YATAFAKARI KWA MAJA

CHELSEA inatafakari kuhusu Januari kumfuata mshambuliaji wa Bordeaux, Mnigeria Josh Maja, 20, ambaye zamania aliichezea Sunderland. ***(90min.com)***

### FERGUSON KUTETA NA KEAN

KOCHA wa muda wa Everton, Duncan Ferguson atafanya mazungumzo na Moise Kean, 19, baada ya kumuingiza akitokea benchi na kumfanyia mabadiliko ndani ya dakika ya 19 - akidai mshambuliaji huyo wa Italia alishindwa kuhimili kasi wakati wakitoka sare dhidi ya Manchester United juzi. ***(Telegraph)***

### LIVER KUMNASA MCCALLUM

LIVERPOOL inajiandaa kushinda mbio za kumsajili beki wa kushoto wa Coventry, Muingereza Sam McCallum, 19, katika dirisha la Januari ikiwapiku wapinzani wao wa Ligi Kuu - na kisha kumtoa kwa mkopo kwa 'Sky Blues' hao kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki. ***(90min.com)***

### BREWSTER ANUKIA SWANSEA

SWANSEA City inapewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Rhian Brewster, 19, kwa mkopo, shukrani kwa kocha Steve Cooper kuwa na uhusiano mzuri na mshambuliaji huyo. Brewster alikuwa sehemu ya kikosi cha England U-17 kilichotwaa Kombe la Dunia chini ya Cooper mwaka 2017. ***(Telegraph)***

### CHELSEA YAMFUATILIA WHITE

CHELSEA imemuweka karika orodha yake ya wachezaji inaotaka kuwasajili, beki wa Brighton, Muingereza Ben White, 22, ambaye alivutia akicheza kwa mkopo Leeds United, huku ikiandaa pauni milioni 25 kwa ajili yake kuelekea dirisha la usajili la Januari. ***(Sun)***

### AMTOA GIROUD CHELSEA

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amemshauri mshambuliaji Olivier Giroud, 33, kuachana na Chelsea katika dirisha hili la Januari - lakini mazungumzo na kocha wa Inter Milan, Antonio Conte yamesitishwa. Giroud atamaliza mkataba wake majira ya joto. ***(Mirror)***

### MADRID YAMFUKUZIA TORRES

REAL Madrid inaendelea kumfuatlia winga wa Valencia, Mhispania Ferran Torres, 19. ***(AS)***

# KILIMANJARO STARS KUFA, KUPONA IKIIVAA UGANDA

**Na Somoe Ng'itu,** KAMPALA

HAKUNA kulala! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), Juma Mgunda, kuelekea katika mechi ya hatua ya nusu fainali dhidi ya wenyeji Uganda (The Cranes) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KCCA jijini hapa.

**Kilimanjaro Stars ilimaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi B wakati inakutana na vinara wa Kundi A, Uganda ambayo ilishinda mechi zake zote nne za hatua ya makundi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa pande zote mbili kwa sababu inachezwa kwa mtindo wa mtoano.

Mgunda alisema kuwa amekiandaa vema kikosi chake kukabiliana na ushindani huku akiyafanyia kazi mazuri na upungufu wa wapinzani wao ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya na hatimaye kutinga fainali.

Alisema kikosi chake kitaingia katika mchezo huo kikiwa na "mipango" tofauti kwa ajili ya kuwachanganya wapinzani na anaamini hamasa waliyonayo wachezaji wake, itasaidia kupata ushindi katika mechi hiyo ya "kufa au kupona."

"Nia yetu ni kuendelea kupambana, hapa Tanzania ilipofika ni mahali kwa kushindana, kila tunapokuwa ni jukumu letu kupambana, kikubwa tumeshayasoma mazuri yao, tunajipanga kuwazuia na upungufu wao utatusaidia kupata faida katika mechi hiyo ya nusu fainali," alisema Mgunda.

Kocha huyo wa Coastal Union alisema mchezaji ambaye ni majeruhi ni Miraji Athumani, lakini hatima ya kumtumia itajulikana leo asubuhi baada ya jana kupewa mapumziko maalumu na daktari wa timu.

"Ninachopenda kuwaambia Watanzania ni kuwa wazidi kutuombea dua, waweke uzalendo kwanza, naamini mwisho wa siku tutaruka pamoja na tutacheza pamoja," alisema kocha huyo.

Naye Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema Kilimanjaro Stars na timu ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Bara wanastahili kupongezwa kwa hatua ambazo wamefikia katika mashindano wanayoshiriki kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

"Tunaziombea timu zetu zifanye vizuri hapo kesho (leo), zote zinaweza kumaliza katika nafasi mbili za juu, huu ni wakati sahihi wa kuweka historia kwa kuchukua makombe yote mawili," alisema Karia.

Bingwa mtetezi wa mashindano hayo yanayotarajiwa kumalizika keshokutwa Alhamisi ni Kenya.

## Tanzania Bara U-17 njiapanda ubingwa

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

PAZIA la mashindano ya Kombe la Chalenji kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17 wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) linatarajiwa kufungwa leo kwenye Uwanja wa Njeru kwa wawakilishi wa Tanzania Bara kuvaana na Djibouti.

Tanzania Bara yenye pointi nane ipo njiapanda kuelekea kutwaa kombe hilo, kwani ili iweze kuibuka mabingwa wa mashindano haya yanayofanyika kwa mara ya kwanza, inatakiwa kupata ushindi wowote wakati pia ikiwaombea Kenya wawafunge wenyeji Uganda ambao wanaongoza katika msimamo wakiwa na pointi 10.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Tanzania Bara, Bakari Shime, alisema mechi hiyo ni muhimu na anaamini bado timu yake ina nafasi ya kushinda kikombe cha michuano hiyo.

Shime alisema amerekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi nne zilizotangulia kwa sababu mbali na kusaka ubingwa, michuano hii imeandaliwa kwa lengo la kuendeleza soka la wanawake.

Naye Kocha Mkuu wa Djibouti (U-17), Fatouma Moussa, amesema wachezaji wake wanaimarika kadri mechi za mashindano haya zinavyoendelea na watarejea kwao kujipanga zaidi kwa ajili ya michuano ya mwakani.

"Hata ukiangalia idadi ya mabao na kiwango cha wachezaji wangu vinabadilika, wamekuja kujifunza, tunaamini tutakuwa na kikosi imara hapo mwakani, hatutapoteza mechi nyingine kama mwaka huu, " alisema Fatouma.

## Mchezaji Bora apewa RAV4

**Na Mwandishi Wetu,** UGANDA

NAHODHA na mshambuliaji tegemeo wa timu ya wasichana ya umri chini miaka 17 ya Uganda, Julieth Nalukenge, ametangazwa kuwa mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora wa kike wa mwaka wa Uganda.

Nalukenge ambaye alikuwa pia katika kikosi cha timu ya Taifa ya Wanawake ya Uganda (She- Cranes), amekabidhiwa zawadi ya gari jipya kutokana na kuwashinda wachezaji wenzake wawili waliokuwa pia wanawania tuzo hiyo.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, katika sherehe zilizofanyika Jumamosi usiku, Nalukenge, alisema amefurahi kupata tuzo hiyo na anaahidi kuendelea kujituma kuisaidia nchi yake katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

Nalukenge, kutoka katika klabu ya Kawempe Muslim, alisema anaamini ubora wake unatokana na ushirikiano anaoupata kutoka kwa wachezaji wenzake na anaamini zawadi hiyo itamwongezea hamasa katika kuimarisha kiwango chake.

Kwa upande wa wanaume, Allan Okelo, ambaye anaichezea KCCA aliibuka kinara na yeye alikabidhiwa pia zawadi ya gari jipya aina ya Toyota RAV4.



Mshambuliaji wa Azam FC, Mzambia Obrey Chirwa, akichukua mpira kwa ufundi wa hali ya juu mbele ya beki wa Green Warriors katika mchezo wa kirafiki uliopigwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam juzi na wenyeji hao kushinda 5-1, mabao yakifungwa na Mzimbabwe Donald Ngoma (mawili), Muivory Coast Richard Ella Djodi na viungo Joseph Mahundi pamoja na Iddi Kipagwile kwa penalti. **PICHA: MTANDAO**

## TFF yatoa angalizo usajili dirisha dogo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dirisha dogo la usajili Tanzania Bara likifunguliwa rasmi jana, timu zinazoshiriki Ligi Kuu pamoja na Ligi Daraja la Kwanza zimepewa angalizo kali kwa kuhakikisha zinakamilisha usajili wao kwa wakati.

Dirisha dogo ambalo ni maalumu kwa ajili ya timu kuimarisha vikosi vyao hususan idara zilizopwaya ama kukabiliwa na majeruhi, litadumu kwa kipindi cha mwezi mmoja ambapo litafungwa rasmi Januari 15, mwakani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, imezitaka timu zote kukamilisha usajili wa dirisha dogo ndani ya muda uliopangwa.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa hakutakuwa na muda wa nyongeza baada ya Januari 15, hivyo ni muhimu kwa klabu zote kufanya usajili kwa kuzingatia tarehe iliyopangwa kwa dirisha hilo kufungwa.

Mbali na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara timu nyingine ambazo dirisha hilo linawahusu ni zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza (FDL), LIgi Daraja la Pili (SDL) na Ligi ya Wanawake Tanzania Bara.

Tayari baadhi ya klabu zimeshaanza kujiimarisha kwa kusajili nyota wapya, ikiwamo mabingwa wa kihistoria nchini, Yanga ambao wamemsajili mshambuliaji Tariq Seif aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Misri.

# Michezo

Jumanne Desemba 17, 2019

Nipashe




**Ljungberg: Arsenal tafuteni kocha haraka** HABARI UK.30

**OKOA...**




Kipa wa Arsenal, Bernd Leno akicheza mpira dhidi ya mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates na Arsenal kupigwa 3-0 juzi. Chini anayemkwepa ni beki Sead Kolasinac. **HABARI UK. 28**

# Simba, Yanga nje ndani Mapinduzi

●●● Bodi ya Ligi Tanzania yatoa masharti magumu kushiriki, huko Jangwani Lamine anogesha mambo...

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

SIMBA na Yanga ziko mguu nje ndani kwenda kushiriki mashindano ya kuwania Kombe la Mapinduzi mwakani kutokana na Bodi ya Ligi Tanzania kuweka masharti "magumu" kwa waandaaji wa michuano hiyo inayofanyika Zanzibar kila mwaka, imefahamika.

**Mashindano ya Kombe la Mapinduzi yamepangwa kufanyika kuanzia Desemba 31, mwaka huu na kumalizika Januari 13 mwakani, huku vigogo hao wakitarajiwa kukutana katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara ifikapo Januari 4, mwakani.**

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu mjini hapa, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Tanzania, Stephen Mguto, alisema kuwa mechi hiyo ya Ligi Kuu haitapanguliwa na bodi yake imewapa masharti waandaaji wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, endapo watawahitaji vigogo hao.

Mguto alisema sharti kubwa walilowapa ni kubadili aina ya mfumo wa mashindano hayo kwa kucheza mechi kwa mtoano na si makundi kama ilivyozoeleka.

Kiongozi huyo alisema kuwa wanataka kuona ratiba ya Ligi Kuu ambayo ilirekebishwa hivi karibuni haipanguliwi tena kutokana na mashindano hayo, kwa sababu tayari waliwapa taarifa ya siku ambazo wanaweza kushirikisha klabu za Tanzania Bara.

"Simba na Yanga wanaweza kwenda kushiriki Kombe la Mapinduzi endapo tu waandaaji watakubaliana na mapendekezo yetu, wakitaka kwenda tofauti nadhani watakuwa hawawahitaji, hii ni kutokana changamoto ya kubadili ratiba iliyotokana na ushiriki wa Taifa Stars na klabu kwenye majukumu ya kimataifa," alisema Mguto.

Aliongeza kuwa mapendekezo ambayo wametoa ni kwa ajili ya kuheshimu umuhimu wa michuano hiyo na kuhakikisha Simba na Yanga zinakwenda Zanzibar kuchuana na hatimaye kuwapa nafasi mashabiki wao wa visiwani kuwaona wachezaji walioko kwenye vikosi hivyo.

Mbali na Simba na Yanga, klabu nyingine ya Tanzania Bara inayotarajiwa kushiriki mashindano hayo ni mabingwa watetezi Azam FC kutoka jijini Dar es Salaam.

Katika hatua nyingine kuelekea mechi hiyo, mbali na Yanga kuzidi kujiimarisha kwa kumsajili Tariq Seif, inaelezwa beki wao kisiki, Lamine Moro, ambaye aliondoka hivi karibuni kutokana na madai ya mshahara na kurejea kwao nchini Ghana, amerejea Bongo kumalizana na mabosi wake hao.

Moro alikuwa bora kwenye mechi zake ambazo alizicheza akiwa na Yanga msimu huu, huku akihusishwa kutua ndani ya Simba ambao walifanya naye majaribio na kuamua kumuacha.

# Uefa sasa yampeleka Guardiola Real Madrid

**Nyon,** Uswisi

HATUA ya mtoano ya 16-bora Ligi ya Mabingwa Ulaya imemrudisha Hispania kocha Pep Guardiola kwa kikosi chake cha Manchester City kwenda kuivaa Real Madrid.

Kikosi cha Pep Guardiola kilimaliza kileleni mwa kundi lake huku Real Madrid ikishika nafasi ya pili nyuma ya Paris Saint-Germain katika Kundi A, ambapo miamba hiyo sasa itakutana mapema kuliko ilivyotarajiwa. Mechi za kwanza zikipigwa kati ya Februari 18/19 na 25/26, mwakani

Mabingwa watetezi Liverpool pia wamepangwa na miamba mingine ya La Liga, Atletico de Madrid wakati Chelsea wakitakiwa kuwavaa Bayern Munich - waliyoifunga fainali wakati wakitwaa kombe hilo mwaka 2012.

Mabingwa wa Ligue 1, PSG watavaa Borussia Dortmund, huku Tottenham ikiwa na kibarua kigumu dhidi ya RB Leipzig wakati Napoli ikivaana na Barcelona.

Mechi nyingine ni Atalanta vs Valencia, Lyon vs Juventus wakati, Jose Mourinho na Tottenham yake wakiwa na kibarua kigumu dhidi ya RB Leipzig.

Kwingineko kwenye michuano ya Europa katika hatua 32, Manchester United itavaana na Club Brugge ya Ubelgiji wakati Arsenal ikiwa na kibarua kigumu dhidi ya Wagiriki, Olympiacos huku Inter ikivaana na Ludogorets.

Timu nyingine ya England, Wolves itavaana na Wahispania, Espanyol huku Sporting Lisbon ikicheza dhidi ya Istanbul Basaksehir, Getafe vs Ajax, Bayer Leverkusen vs FC Porto, FC Copenhagen vs Celtic, Apoel vs FC Basel, Cluj vs Sevilla, AZ Alkmaar vs LASK, Eintracht Frankfurt vs FC Salzburg, Shakhtar Donetsk vs Benfica, Wolfsburg vs Malmo, Roma vs Gent na Rangers ikimenyana dhidi ya Braga, raundi ya kwanza ikipigwa Februari 20, mwakani.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >